MUUJIZA WA MASIHI

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

Muujiza wa Masihi

Tafsiri ya Kiswahili ya: I'jaazul Masihi (Kiarabu)
I'jāzul Masīḥ (Swahili Translation)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri:
Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani

Chapa ya Kwanza (Kiarabu): 1901
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2025

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:
Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031
Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

Cover design: Sabahat Ahmad Cheema

ISBN: 978-1-83596-501-6
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

من سرّه ان يقرء الفاتحة مع معارفها المخفية ۔ وحقائقها
الروحانية ۔ فليقرء تفسيرنا هذا بالتدبر وصحّة النية ۔
ولا يحسر عن ساعده للمقابلة ۔ فانه كتاب ليس له
جوابٌ ۔ ومَن قام للجواب وتنمّر ۔ فسوف يرى انه
تندم وتذمّر ۔ فطوبى لمن همّه ما اصطفيناه ۔ واخذ
ما اعطيناه ۔ وما كان كالذي لبس الصفاقة ۔ وخلع
الصداقة ۔ وهذا ردّ على الذين يُجهّلوننا ويصبّغون
التلبيس ۔ ويقولون ليس عندهم من علم بل عُصبةٌ
من مفاليس ۔ وانّا اقررنا بانّ كُتُبنا كلُّها من حولِ الله
ذي الجلال ۔ وما نحن الا كالجُهّال ۔ وانّ كتابي
هذا بليغ ۔ وفصيح ومليح ۔
واني
سمّيته

اِعجاز المسِيح

وقد طُبع
في مطبع ضياء الاسلام في سبعين يومًا من شهر الصيام وكان من الهجرة سنة ۱۳۱۸
ومن شهر النصارى ۲۰ فروری سنہ ۱۹۰۱ ۔ مقام الطبع قاديان ضلع گورداسپور باهتمام
قيمت عمر الحكيم فضل دين البهيروي ۔ جلد ۷۰۰

Jalada la chapa ya kwanza

Mtu apendaye kusoma Sura Al-Faatiha pamoja na maarifa yake yaliyofichika na hakika zake za kiruhania anapaswa ayasome maelezo yetu haya kwa makini na nia njema na asipanie mikono ya kanzu kwa kushindana. Kwani hiki ni kitabu kisichoweza kujibiwa. Na yeyote atakayekuwa tayari kukijibu na kujifanya chui, basi karibuni akajikuta anajuta na kunung'unika. Basi abarikiwe anayejichukulia maneo yetu mateule na anapokea tunayompatia, na hawi kama yule ajivaliaye joho la upujufu na kutupilia mbali vazi la ukweli. Kitabu hiki ni jibu kwa watu wanaotuita majahili na kuleta udanganyifu kwa kuupamba na kusema kwamba hao hawana elimu yoyote bali ni kundi la waliofilisika. Naam, twakiri kwamba vitabu vyetu vyote vimeandikwa kwa msaada wa Mungu Jalali, waila sisi tu kama wale wasiojua. Kitabu changu hiki kina balagha na fasaha ya hali ya juu na ni kizuri mno, nami nimekiita

Muujiza wa Masihi.

Kitabu hiki kimechapwa katika matbaa ya Dhiaul Islam – kikitayarishwa ndani ya siku sabini – katika mwezi wa Ramadhani 1318 Hijra sawa na 20 Februari 1901, kilichapwa mjini Qadian, Wilaya ya Gurdaspur, chini ya usimamizi wa Hakiim Fadhl Din wa Bhera.

Bei: Rupia moja Nakala: 700

NENO LA MWENEZI

Ni furaha yangu tele kuweka mbele ya wasomaji kitabu hiki, Muujiza wa Masihi (I'jaazul Masihi), kitoacho maelezo yenye kina ya Sura Al-Faatiha.

Hii ni tafsiri ya Kiswahili ya kitabu I'jaazul Masih kilichoandikwa na Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa lugha yenye ufasaha ya Kiarabu.

Sababu hasa ya kuandika kitabu hiki ni kwamba wapinzani wa Seyidna Ahmad[as] wakimpinga wakadai kwamba yenye hata hajui Kiarabu. Hapo yeye akawatupia mwito masheikh wote wapinzani, tarehe 20 Julai 1900, kukabiliana naye kuandika kwa lugha fasihi ya Kiarabu maelezo ya aya arobaini za Kurani Tukufu.

Akapendekeza kuitisha mkutano mjini Lahore ambamo aya 40 za Kuran Tukufu zitachaguliwa kwa kupigwa kura, na masheikh pamoja na Seyidna Ahmad[as] wataandika mumo humo mkutanoni maelezo ya aya hizo wakikaa ana kwa ana. Kila mmoja atapaswa kuandika kwa akali juzuu nne (yaani kurasa 64) kwa Kiarabu.

Ni ajabu kuwa waliodai kuwa wajuzi wa Kiarabu, hususan Pir Mehr Ali wa Golra, wote wakawa mahawafu. Wakafyata mkia.

Lakini baadaye Pir Mehr Ali pasipo kumwarifu Seyidna Ahmad[as] akafika Lahore na kutangaza kwamba ameishafika mjini Lahore, lakini kwanza tufanye mjadala.

Kwa ujanja huu akawalaghai watu kana kwamba yu tayari kuandika maelezo ya aya za Kurani Tukufu lakini kwanza wajadiliane kuhusiana na ukweli wa Seyidna Ahmad[as].

Seyidna Ahmad[as] akatoboa siri yake, kwani Seyidna Ahmad[as] alikwisha tangaza muda fulani hapo kabla ya kwamba sitafanya mjadala na mtu yeyote, kwani mijadala kila mara haikuleta matokeo mema. Uayari wake ulikuwa kwamba Seyidna Ahmad[as] kama atakuwa tayari kwa mjadala, Bwana Pir atamlaumu kuvunja ahadi yake; na akikataa, atatangaza kuwa Seyidna Ahmad[as] amekimbia kunikabili.

Seyidna Ahmad[as] alielewa kabisa unyonge wa sheikh, hivyo akamruhusu kuwastajiri masheikh wengine, hata kuajiri baadhi ya Waarabu walio waandishi hodari ili kumwaviza. Na kama hataweza kuchapisha maelezo yake katika mwia wa siku sabini unaoishia tarehe 15 Desemba 1900, hapo atahesabiwa mwongo.

Kisha Seyidna Ahmad[as] kwa upande wake akaandika tafsiri ya Sura Al-Faatiha kwa lugha yenye ufasaha ya Kiarabu na kuchapisha kwa sura ya kitabu ndani ya muda uliowekwa wa siku sabini.

Maelezo haya ya Sura Al-Faatiha ni muujiza wenye shani yaelezayo elimu ya ndani kabisa ya kiungu.

Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani anastahili kushukuriwa aliyefasiri I'jaazul Masihi kwa Kiswahili. Nimeidurusu tafsiri hii kwa uangalifu sana ili ilingane iwezekanavyo na aliyoeleza Seyidna Ahmad[as].

Shukurani kwa Sheikh Ansar Hussain aliyepanga herufi hizi kwa kompyuta na kutayarisha fomati.

Namwomba Mola Mtukufu Akifanye kitabu hiki kiwe chenye kuwanufaisha wasoaji kielimu na Kiroho. Amin.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 30 Desemba 2021

TAARIFA

Kwa kuwaarifu watu wote inaandikwa kwa Kiurdu kwamba Mwenyezi Mungu kwa fadhili na hisani yake Amekikamilisha kitabu hiki katika siku sabini, tarehe 20 Februari 1901. Ukweli ndio huu kwamba hii yote imefanyika kwa fadhili yake. Katika siku hizo nilishikwa pia na maradhi ya aina nyingi yaliyoleta shaka kwamba isije kazi hii isiweze kukamilika. Kwani, kwa sababu ya udhaifu wangu wa kila siku na maradhi hali haikufaa kuweza kushika kalamu. Hata kama ningekuwa na afya, ningekuwa na uwezo gani, mimi ndimi najijuaye vizuri. Lakini hatimaye nilitambua siri hii ya maradhi hayo ya kimwili kwamba ili jumuiya hii pia waliopo hapa miongoni mwa marafiki zangu wasifikiri kuwa hayo ni matokeo ya nguvu zangu za kiakili. Basi, Yeye Alithibitisha kwa maradhi hayo na vizuizi hivyo kwamba hiyo siyo kwa sababu ya moyo na akili yangu. Wapinzani wangu wapo ukwelini kufikiria kwamba hiyo siyo kazi yangu, bali yupo mwingine anayenisaidia kisirisiri. Basi, nashuhudia kwamba kwa kweli Yupo mwingine Anayenisaidia, lakini huyo si mwanadamu, bali ndiye Yule Mweza na Mwenye nguvu ambaye kwenye kizingiti chake kipo kichwa changu. Kama kuna mwingine pia anayeweza kusaidia katika kazi kama hii ambaye ana nguvu ya kimuujiza, hapo wasomaji wanapaswa kutarajia kwamba pamoja na kitabu hiki yatachapwa – au yameishachapwa – mamia ya maelezo mengine ya Sura

Al-Faatiha mithili yake katika hizo hizo siku sabini sawa na masharti yangu, kwani jambo hili ni msingi wa uamuzi. Hususan Seyid Mehr Ali Shah, ni yakini kwamba atakuwa lazima amejaribu kiasi fulani wakati huo kuandika maelezo ya Kurani, waila atawezaje sasa kukabili watu ambao waliambiwa kwamba yeye amefika Lahore kwa kuandika maelezo ya Kurani. Ni dhahiri kwamba kama hakuweza kuyaandika katika siku sabini, atawezaje kuandika katika masaa saba. Ilmuradi kwa watu waadilifu hii ndiyo ishara yenye shani kubwa kwa kuona msaada wa Mungu. Kwani kwa kuweka muda wa siku sabini mamia ya masheikh waliitwa kukabiliana nami. Sasa wanalo jibu lipi, kwa nini hawakuweza kuchapisha maelezo ya Kurani ya namna hii. Huu ndio muujiza, la sivyo muujiza ni kitu gani?

(Tafsiri ya shairi la Kiurdu)

Enyi marafiki mnaosoma Ummul Kitabu (Sura Al-Faatiha), sasa tazameni jua hili kwa macho yangu.

Tafakarini kwa kusoma dua ya Al-Faatiha mara kwa mara; hii yafichua uhakika wote.

Angalieni, Mungu Amewaambieni dua hii, Mpendwa wake pia amewasomesheni dua hii hii.

Mnaisoma nyakati tano; kwa kuipitia hii mnafikia mlangoni pa Yule Asiyehitaji.

Naapa kwa Yule Aliyemteremshia Sura hii yule mwenye moyo mtakatifu ambaye sura yake hupendeza.

Hii ndiyo shahidi wangu kutoka kwa Mola wangu, hii ni muhuri wa Allah juu ya ukweli wa madai yangu.

Hii ndiyo dalili juu ya kuwa kwangu Masihi; kwangu mimi hii ndiyo shahidi ya Mola Jalali.

Basi, baada yangu mwawangojeaje wengine? Tubuni, kwani kuna mategemeo gani ya kuishi!

Mwandishi:

Mnyenyekevu Mirza Ghulam Ahmad
kutoka Qadian, 20 Februari 1901

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ [1]

Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu Aliyemjaalia mtu nguvu ya kusema na kumfundisha ufasaha wa kujieleza na Akayafanya maneno ya mtu kuwa dhihirisho la uzuri Wake uliofichika; na Akaziboresha siri za watawa kwa ufunuo Wake. Alikamilisha roho za watu watakatifu kwa neema zake na kuwatimizia kila jambo lao kwa hisani yake na kuwapa kivuli cha usaidizi wake na kuwachukia wawachukiao mawalii Wake; hakuwaacha peke yao pasipo kuwasaidia wakati wa hofu. Akakubali maombi yao kila walipomwelekea kikamilifu na kuonyesha kwa ajili yao ghera Yake na Akawa kwao kama simba kwa shibli zake. Akawafadhili katika kila uwanja wa mapambano kama jamaa wa karibu. Na Hakujitenga nao katika mahali popote wala Hakuwasahau walipomwomba kwa kilio. Aliwalazimisha neno la takwa na kuwaimarisha katika njia za mwongozo na kuwavutia kwenye Dhati yake iliyo juu fika. Aliwajaalia macho ya kuonea na kuwapa mioyo ambayo wanaelewa kwayo na viungo ambavyo wanafanya kazi navyo na Akawafanya kuwa kimbilio la viumbe vyote na roho ya walimwengu. Kisha salamu na rehema ziwe juu ya Mtume[saw] aliyefika katika zama ambazo zilikuwa kama kiti cha enzi kisichokuwa na mwenyekiti wake au zilikuwa kama usiku

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

ambao mwezi mpevu wake umetua. Alidhihiri katika zama ambamo watu walihitaji pa kukimbilia na ardhi ilipatwa na ukame na kwa kukosa mvua ikawa maskini. Kisha Mtume huyu alimwagilia ardhi iliyokuwa imekauka kabisa kwa kukosa mvua kwa wakati wake na akaihuisha mioyo kama vile mvua kita inavyohuisha ardhi kame. Nyuso ziliangazwa, uzuri wao ukarudi na vipaji vya tabia vilivyofichika vikawa wazi na ukwasi wao ukadhihiri na waaminio wakatakaswa katika kila aina ya dhambi. Na baada ya kukatwa mabawa haya ya dhambi wakapewa mabawa ya kuruka mpaka mbinguni; na msingi wa kila kazi yao ukastawishwa juu ya takwa. Basi, hakubakia ndani mwao hata chembe ya ghairi ya Mungu wala tamaa za nafsi. Na ardhi ya Makka ambapo masanamu yalizungukiwa ikatakaswa kiasi hiki kwamba mpaka leo hakusujudiwa hapo yeyote minghairi ya Mungu, Mwingi wa rehema. Hivyo, msalieni Nabii huyu mhisani ambaye ni dhihirisho la sifa za Mungu Rahmani Aliye Mhisani mkubwa. Na malipo ya hisani ni hisani tu. Moyo ule usioitambua hisani Yake hauna imani au unaendelea kupoteza imani yake. Ee Allah, msalie Mtume huyu aliye Nabii Ummi aliyewanywesha wa baadaye jinsi alivyowanywesha wa awali na kuwafanya wafanane naye na akawaingiza katika waliotakasika. Kisha Mungu Aliwanurisha kwa mwanga wa mionzi ya mahaba na kuwanywesha mvinyo halisi mno (ya kiroho) na

Akawaunganisha na waliotangulia miongoni mwa waliojipoteza ndani ya Mungu. Na Akawajaalia ukaribu Wake na kukubali dhabihu zao. Akazifanya hisia zao kuwa nyepesi na kung'arisha mioyo yao. Vilevile Aliwapa kutoka kwake ufahamu wa wale waliokaribishwa, kuzitakasa nafsi zao na kuzisafisha nyoyo zao na kuzitakatisha, na kuzipamba roho zao na kuziokoa nafsi zao katika minyororo ya wafungwa. Na kama vile ilivyokuwa suna yake kwa waja wake walioteuliwa Akawa mdhamini wao katika mambo yao yote. Na sawa na suna yake inayoendelea kwa mawalii wake Akawapanulia vifua vyao. Aliwaita wamjie na mara moja Akawafungulia mlango kwa rehema yake na kuwajumuisha katika kundi lake na kuwaingiza wao pia ndani ya wakazi wa Pepo yake. Kisha wakaambiwa mmeijia nyumba yenu ya asili na mmeishakutana na ahli zenu, nao wakaingizwa ndani ya mahababu Wake. Na hayo yote ndiyo kwa baraka za Mbora wa Mitume, Khatamun Nabiyyin, Muhammad[saw]. Allah, Malaika, Manabii Wake na watu wema wote wamsalie yeye.

Baada ya hayo, enyi watafuta haki, waadilifu, wenye akili na wenye kutafakari, mjue vizuri kwamba mimi ni mtumishi miongoni mwa watumishi wa Mungu Rahmani ambao wanakuja kutoka kwa Mungu Aliye Mmoja na kushuka kwa amri ya Mola Mtukufu wakati wa haja kali na ambapo ujahili na bidaa zapata kuenea na takwa na

maarifa vyapungua ili wakijadidishe kilichochakaa na wajumuishe kilichosambaratika na kutafuta kilichopotea na kutimiliza kikamilifu kilichoahidiwa na Mola wa walimwengu. Na hivyo ndivyo ambavyo nimekuja, nami ndimi wa kwanza wa waaminio. Nimetumwa kwenye mwanzo wa karne hii tukufu ili nikusanye kilichosambaratika cha umati wa Kiislamu na nijibu mashambulio dhidi ya Kitabu cha Mungu, Kurani, na Mbora wa viumbe, Hadhrat Muhammad[saw] mtukufu; na nivunjilie mbali fimbo ya waasi na niziimarishe kuta za sheria. Nimeshaeleza kwa uwazi mara kwa mara na kuwadhihirishia watu kwamba mimi ndimi Masihi Mau'udi na Mahdi wa ahadi. Na kadhalika nimeamrishwa na sithubutu kuasi amri ya Mola wangu na kuungana na wahalifu. Basi msifanye haraka kunipinga, na tafakarini vizuri juu ya jambo langu ikiwa nyinyi ndio wamchao Mungu. Na huenda mkamkadhibisha mtu ilhali amekuja Kutoka kwa Mungu, na pengine kumchukulia kuwa fasiki naye ndiye miongoni mwa watu wema. Kwa yakini Mwenyezi Mungu Amenituma kuondolea mbali ghasia za zama hizi na kubainisha tofauti kati ya bustani takatifu na mimea iliyoota kwenye rundo la takataka na kuwaonyesha watu waliopotea njia ya haki. Na madai yangu haya siyo ya wakati usiofaa, bali nimekuja kama mvua ya masika inayonyesha barabara katika msimu wake na wakati wake. Ninayo mashuhuda kutoka kwa Mola

wangu kwa watafutao haki, ishara zilizo wazi kwa watambuzi na uso kama wa wakweli kwa wenye busara. Siku za ahadi za Mungu zimewadia na milango ya rehema imefunguliwa kwa wazitafutao rehema. Basi msiwe wa kwanza kukataa zile neema mlizokuwa mkingojea. Sasa umebakiaje mficho. Fumbueni macho enyi wenye akili. Ardhi na mbingu zimeshuhudia kwa ajili yangu. Maulamaa waaminifu wamenijia na mioyo ya watambuzi imenitambua. Katika vena za mioyo yao yakini imepenya kama vile maji safi yanavyotiririka katika mifereji ya bustani. Juu ya hayo baadhi ya masheikh wa nchi hii hawakunikubali kwa ubahili na kwa kujigamba. Hivyo hawakutudhulumu bali walijidhulumu nafsi zao kwa husuda na kiburi. Na waliridhia giza la ujahili na kujitenga na elimu na nuru. Basi juu ya kauli zao, mienendo yao na juu ya dhati yao zimegandama rusu nene za kiza kiasi hiki kwamba popo wamepata kujikalia mioyoni mwao na nyuni mwenye sauti nzuri hakutua juu ya matawi yao. Hao hapo kabla walikuwa wakitarajia ujio wa Masihi mwanzoni mwa karne hii na walikuwa wakimsubiri kama vile watu wanavyosubiri miezi ya idi au vyakula vitamu katika mwaliko. Lakini kitu walichotarajia walipotayarishiwa na kile walichotaka walipotolewa, walianza kulidhania Neno la Mungu kuwa uzushi wa kibinadamu na wakasema huyu ni mzushi anayewapoteza watu kama shetani. Na wakaanza kuishuku shani yake

bali hata imani yake pia. Wakamkadhibisha yeye pamoja na wafuasi na wasaidizi wake na kuwachukulia kuwa mafasiki na makafiri. Mungu Aliziteremsha ishara nyingi lakini hawakuzikubali. Akaonyesha misaada mingi mwanzoni na mwishoni, lakini hawakujali na kusema yu mwongo, lakini hawakutafakari hata kidogo kuhusu mwisho wa waongo. Walimwita mzushi, lakini hawakuwakumbuka wazushi walioishapita. Ni masikitiko, mamia ya masikitiko, kwamba wanasema lakini hawasikilizi; wanaleta upinzani lakini hawasikilizi jawabu; wanakosoa lakini hawahakikishi. Haki imeshadhihirika bayana lakini hawaoni. Wanapomkashifu mtu asiye na hatia, hucheka wala hawalii. Imekuwaje hawaogopi. Je, kuna dhamana katika maandiko kwamba wataachwa, sikuti hofu ya Mungu mioyoni mwao, bali wanawaudhi wakweli wala hawajali. Siwaoni kuwa wenye mioyo mipana. Wamejichagulia marafiki wafananao nao na wanawaaibisha wengine na kuwasengenya kwa kusudi. Mazungumzo yao ni kama kinyesi cha ndege. Au kama mgonjwa wa kifua kikuu anayetema hapa na pale. Hawakijui kiini cha jambo letu wala hawatambui uhakika wa siri yetu. Pasipo kufahamu Kitabu cha Mungu wanakufurisha na kutusi na kupayuka; lakini si kama mbwa wabwekavyo bali zaidi yake. Hawakubakiwa na ufahamu uwafikishao kwenye njia iliyonyoka wala hawana hofu iwavutiayo kwenye njia za ridhaa ya Allah,

Mwingi wa ukarimu. Wapo miongoni mwao wapendao hali ya wastani wanaokadhibisha kwa utovu wa ujuzi na wapo wengine ambao wanazizuia ndimi wala hawatusi. Lakini utawakuta wengi wao wanatumia midomo michafu dhidi yetu na kutukataa na wanatukana bila hofu. Basi, yapasa waliao waulilie msiba huu wa Islam na fitina za zama hizi. Kuna fitina gani kubwa zaidi kuliko fitina za maulamaa hao. Kwani, Maulamaa hao wameiacha dini bila msaada kama mashahidi wa Karbala. Huu ni moto ulioyeyusha mioyo yetu na kuvunja mbavu zetu na kuzifanya kazi zetu kuwa ngumu kwa jili yetu na kukipinga vikali Kitabu cha Mungu kwa maneno ya kijahili ya majahili. Twawaona wengi wao wanaficha haki wala hawajiepushi na uongo kama watu wema. Ndimi zao zinasema uongo wakati wa kutoa fatwa. Wameshaficha tabia zao katika mapazia ya giza, na wameitanguliza hiba ya nafaka juu ya huba ya sala. Wameitupa Kurani nyuma ya migongo yao kwa ajili ya dunia hii hakiri, na kuzielekeza tabia zao kwenye hazina ya kidunia. Uchoyo, uchu na tamaa zao vimezidi sana kwa ladha zisizodumu na uchoyo wao katika tamaa zao za nafsi umepita kila mpaka. Haikubakia ndani yao elimu ya Kitabu cha Mungu, Kurani wala takwa ya mioyo wala ladha ya imani. Na wamekwenda mbali na amali njema na vitendo vya unyofu na usuluhishi. Wakiachana na njia za ufaulu, wameshika njia za maangamio. Kaa la moto la

imani yao limekuwa majivu, na wema na heri kuwa ufisadi. Wameenda mbali sana na wema, na wema umeenda mbali nao kana kwamba wao ni kinyume cha heri, na heri ni kinyume chao. Kwa iblisi wakawa wafungwa waliotiwa minyororo miguuni. Walivutwa kwenye batili kana kwamba walisukumwa kwenye magereza. Wanahini katika fatwa zao wala hawashiki takwa. Wanaongopa wasijali hata kidogo. Na wanayakaribia yaliyoharamishwa na Mungu wala hawajiweki mbali nayo. Hawasikii kauli ya haki bali wanataka kumwaga damu ya msema kweli na kumwangamiza. Imamu alipowaletea mafundisho zisiyoyapenda nafsi zao, wakanuia kumwua hali wanajua. Kama mtu wa kawaida pia hawezi kufa bila idhini ya Mungu, basi wanawezaje kumwulia mbali Mjumbe wa Mungu! Kwa yakini Mungu Anawalinda waja wake Yeye Mwenyewe hata kama wailao njama wafanye hila nyingi namna gani. Wanadai kuwa watumishi wa Islam, lakini ukweli ndio huu kwamba wameshakuwa wasaidizi wa Wakristo katika itikadi zao nyingi. Wamekuwa kama mtego kwa kuwasaidia wawindaji wao. Husema tumeshasikiliza Hadithi pamoja na *isnaad* zake ilihali hawajui hata maana ya *Tauhiid*. Na pia husema kwamba twajua vizuri amri za sheria ilihali hawajakanyaga katika uwanja wa hoja za kidini. Wanaruka katika anga la tamaa za nafsi kama njiwa na hawafikirii wakati wa kifo.

Hujibidiisha sana kwa kiherehere kwa manufaa ya kidunia na wanatoa vichwa vyao kutoka katika kila tundu kama wanafiki. Huangukia kila sinia kwa tamaa hata kama ndani mwake mna nyama ya panya; isipokuwa wale walindwao na Mungu kwa mkono wa fadhili na rehema, watu hao hawahusikani na kauli iliyosemwa wala hawatiliwi hatiani, bila shaka hao ndio miongoni mwa waliosamehewa. Na miongoni mwa fitina adhimu na mabalaa makubwa makubwa ni shambulio la mapadri walilofanya kwa pinde za ukosoaji kama wawindaji. Pinde na mishale waliyotengeneza kwa kuijeruhi dini yetu msingi wake waliweka juu ya hila na ulaghai kama mwindaji, sio juu ya akili na analojia. Walitupulia mbali haki nyuma ya migongo yao na hawakuandika katika vitabu vyao isipokuwa uongo mtupu. Na nguvu zao zote zimejumuika kwa kuangamiza Islam, na maoni yao yaliafikiana kwa kufutilia mbali athari za Seyidna Mbora[saw] wa viumbe. Hao (Mapadri) wakitega mtego wanawaita watu kwenye moto uwakao bali kwenye sehemu zake za chini kabisa. Na wakatumia kila silaha waliyokuwa nayo ya hila na ulaghai na kutumia kila mbinu. Vita yao ikachemka na ustadi wao wa kupigana na mikuki na panga ukawa mkali. Ngoma zao zikavuma na baragumu zao zikalia. Farasi zao wakaonyesha wepesi wao na mafuriko yakaja, kwa nguvu walifikisha juhudi zao mpaka mwisho hata kwamba wakakusanya majeshi

ya ukafiri na wakainua bendera za ufisadi. Waislamu walipatwa na misiba na makazi yakawa ukiwa na kwa kujinywea wakazawadiwa machozi. Bidaa zilizidi kiasi hiki kwamba haikubakia Suna wala Jama'at. Kurani ikatoweka; haukubakia uwezo wa kuilinda na kuihifadhi. Kwa neno zima, Islam imejawa na mateso tele; duara la giza likaizunguka; zama zikaonyesha maajabu kwa kuzivunja kuta zake na zama zilileta mafuriko juu ya mafuriko kwa kufutilia mbali alama zake kwa kuzima nuru zake, takadiri ikatimiliza uamuzi wake. Na kwa kuwa haya yote yalitendeka sawa na takadiri ya Mola na masilahi yaliyofichika, hivyo mwanya wowote haukuweza kuingilia nia yao imara wala mikono yao haikupooza wala makali ya ndimi zao hayakusenea. Matokeo yake yakawa kwamba dini ikadhoofika na sheria ikawa haina nguvu na mafuriko makali yakang'olea mbali mzizi wake kiasi hiki kwamba hata mtambuzi pia hakuweza kutambua. Ufidhuli ulizidi na maarifa yakafutika, nuru zake (Islam) zikafifia na nyota zake zikapotea na dini ikakanyagwa chini ya miguu na zama za misiba yake zikarefuka. Na hiyo ilikuwa ni adhabu ya mioyo iliyotiwa kufuli na malipo ya vifua vilivyozibwa kwa sababu Waislamu wengi walipoteza takwa na kumkasirisha Mola wao. Na unawaona wengi wao kwamba huba ya mali, dhahabu na fedha imewavutia sana na tamaa ya mali na wanawake imeitawala mioyo yao na hamu ya mali na miliki

imeipindua mioyo yao na kwa sababu hiyo wameghafilika na Mungu Rahmani. Unaona wengi wao wanabeba kiriba cha wakana Mungu na kufuata sifa za makafiri kama farasi aliyefundishwa na wanadhani kwamba njia za kufikia serikali ni kufanya hila au kupigana vita. Na wanadhani kwamba uungwana hunyakuliwa kwa njia ya mishale tu. Kwao hakuna njia yoyote ya kusaidia dini isipokuwa kwa umwagaji wa damu kwa upanga na mkuki. Muda wote wanatafuta nafasi za jihadi hata kama masharti yake yasikwepo wala Kitabu cha Mola wa watu kisiamuru. Na jambo hili ni wazi kwamba huu sio wakati wa kukata kichwa kwa kueneza dini. Katika kitabu kilicho wazi kuna amri tofauti kwa kila wakati, bali matakwa ya hekima ya Mungu ndiyo haya kwamba dini ya haki isaidiwe kwa hoja na ishara na mambo ya dini yachunguzwe kwa akili na kuangaliwa kwa makini mizizi na matawi. Kisha ichaguliwe njia ambayo kwayo nuru ya ufunuo iongoze na ikubaliwe na akili, na yafanywe maandalizi jinsi maadui yafanyavyo. Upanga usenezwe na akili kunolewa. Ifuatwe njia ya uhakiki na utafiti na vinywewe vikombe vilivyojua tele kileo. Kwani maadui zetu hawachomoi upanga wala hawaenezi itikadi zao kwa nguvu ya upanga na mkuki, bali wanatumia hila nyepesi za aina aina na udanganyifi na huja kama mwindaji katika sura mbalimbali. Katika zama hizi Mungu Ametutakia hii tu kwamba tuvunje fimbo ya batili kwa hoja si kwa

mikuki. Basi Yeye Alinituma kwa ishara si kwa upanga na Ameifanya kalamu na kauli yangu kuwa chemchemi ya maarifa na elimu ya ndani. Yeye hakunipa upanga wala mkuki bali badala yake Amenipa hoja na ufafanuzi ili Azikusanye kauli mbalimbali kwa mkono wangu na Ajumuishe mambo yaliyotawanyika kunipitia na Aitulize mioyo itetemekayo na kunyamazisha ndimi zisambazo uongo na kunurisha nyoyo zenye giza na kuzitia nguvu hoja chakavu kiasi hiki kwamba lisibaki jambo lolote lisilonyooka wala njia iliyopindika. Kwa neno zima, maelezo haya na maarifa haya ni miongoni mwa miujiza yangu, na panga zangu ni ishara zangu na maneno yangu. Niliwakaribisha baadhi ya maadui zangu kwa kuonyesha muujiza huu huenda Mungu Akapanua vifua vyao kwa njia hii au Akawapatia sehemu katika nuru ya maarifa. Basi, niliwaambia kwamba mkikataa muujiza wangu na kunishambulia kama mpiganaji na kudhani kwamba mmepewa elimu ya Kurani na fasaha kama ya Sahbaan Wa'il, basi njooni, tuwaite wasaidizi wetu nanyi muwaite wasaidizi wenu, tuwaite maulamaa wetu nanyi muwaite maulamaa wenu, kisha tukae ana kwa ana na tuandike maelezo ya Sura fulani papo hapo kila mmoja peke yake bila kupata msaada. Lakini yeyote kati yao hakuthubutu kukubali sharti hili lililotolewa na kufuata jambo lililowekwa na kujitokeza kunikabili na kuandika maelezo kama yangu. Bali wakaanza kushika njia za kiujanja kwa

kuzima nuru na kumkadhibisha aliyetumwa. Mmoja wao aliyeitwa Mher Ali ambaye wenzake walimfikiria kwamba yu sheikh kamili na walii mkubwa, nilipomkaribisha kwa mwito huu baada ya madai yake kwamba anao ujuzi wa Kurani naye ndiye miongoni mwa wenye maarifa, basi alikataa kabisa kuandika maelezo kuyakabili maelezo yangu ya Kurani. Yu mzito wa akili, hata kama yeye angalikuwa kama Hamdani au Hariri asingaliweza kuandika mithili ya maandishi yangu. Pamoja na hayo yeye alikuwa akiwaogopa watu pia na alijua sana kwamba akirudi nyuma, katika hali hiyo hatapata ushindi wala hataweza kupambana na mshindani wake. Basi alikula njama na kasema, kama ilivyoashiriwa, kwamba mimi (Mehr Ali) karibuni nitaandika maelezo sharti ujadiliane nami kwanza sawa na nususi za Hadithi na Kurani na mwamuzi afanywe yule aliye adui yako na mwenye bughuda sana kuliko masheikh wote wa zama hizi.[2] Basi akinisadikisha na kukukadhibisha baada ya kusikiliza maelezo yetu sisi wawili, basi utalazimika kufanya baiati yangu kwa moyo wa kweli. Kisha tutaandika maelezo bila udhuru wowote na kuacha porojo. Tumekubali sharti lako kwa kuongezea kidogo. Ni hayo ndiyo aliyoniandikia na akayachapisha na kueneza baina ya watu. Na

[2] Muradi wake ulikuwa ni mtu anayeitwa Muhammad Husain wa Batala. Mwandishi

akatangaza kwamba ameshakubali masharti, lakini hii ilikuwa ni hila yake kwa kuwadanganya watu. Nilipopokea barua yake iliyochapwa na kujaa ujanja wake nilisema *Innaa lillahi* na kuyalaani maandishi aliyoyasambaza na kusikitikia uharibifu wa wakati. Kisha akatumia ujanja mwingine na akaondoka makazi yake na akisafiri kafika Lahore. Na akarusha vumbi kama fahali na watu walianza kufanya propaganda kwamba yeye amekuja hapa kwa kuandika maelezo ya Kurani tu. Basi, nilipoona kwamba watu wanamchukulia mdudu huyu kuwa chatu na mwiba kuwa bustani, nikasema moyoni kwamba haidhuru niende Lahore, huenda Mungu Akatoa uamuzi baina yetu, na watu wapate kusikiliza tuliyonena na aliyosema. Ndipo nikashauriana na marafiki zangu kuhusu jambo hili na kuwadhihirishia siri hii na kuuliza rai yao na nikawaelezea hali yote kutoka mwanzo mpaka mwisho. Hapo wakasema 'hatuoni sawa uende Lahore, na mji ule ni makao ya fitina na dhuluma. Na imeishabainika kwamba huyo hajakubali mashari na ameonyesha unyonge na udhaifu na dhiki yake na ameloa katika damu yake mwenyewe na ameona kukimbia ndiyo njia ya kusalimika. Yeye amedhulumu na kutoishukuru neema. Hakumchinja kondoo wa nafsi yake wala hakumtundika akifunga miguu yake wala hakumchuna. Na tumesikia kwamba hajaja huko kwa nia safi wala hana ukweli wa moyo hata kidogo. Huu ni ushauri wetu na

uamuzi ni wako. Na haki itakuwa ile tu Atakayokuonyesha Mungu na yatakayoiona macho yako. Basi, ndugu wa Jumuiya yangu waliendelea kunizuia na kunikataza na waling'ang'ania kunizuia kiasi hiki kwamba nikabadilisha nia yangu. Na ushauri wao ukanipendeza nami nikaukubali na sikuukatalia mbali na nikaacha niliyonuia na kujitenga na niliyoyakusudia. Hapo wapinzani wangu walianza kumsifu kwamba amepata ushindi na kumrukisha bila mbawa za elimu na maarifa. Walikuwa wakisema uongo wala hawakuona haya. Wanajigamba wala hawashiki takwa. Wanaongopa wala hawajizuii. Wanapiga chuku kumsifu pasipo yeye kustahiki. Wakamnasibishia maarifa na ujuzi asiokuwa nao. Kama vile ulivyo mwenendo wa majahili walinitukana na kunitaja vibaya na kunifanyia masihara. Na wakasema kwamba mtu huyu amemwogopa kiongozi wetu na kuchelea na ametishika kwa hiyo hakujitokeza uwanjani mwa mjadala na anakwepa kwa kuliogopa jambo kubwa na kutawaliwa na hofu. Lau kama angejitokeza kwa mashindano, kiongozi wetu angemjeruhi kwa maneno yake fasihi na kuponda kichwa chake kwa maneno yenye sifa za jiwe gumu. Na hivyo ndivyo wakapayuka na kunifanyia mzaha na kunitukana. Wallahi, sijioni nafsi yangu isipokuwa kama maiti iliyozikwa au kama nyumba isiyokaliwa na watu. Watu wananifikiria kitu ilihali mimi si kitu chochote. Mimi ni

kama kivuli cha Mola wangu. Sikuwa na uwezo wa kujitokeza medanini mwa mjadala na kuwaita maadui, lakini Mungu Amenitoa kwa vita hii. Sikutupa mshale nilipotupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye Aliyetupa. Na ninaye Mpendwa aliye Mweza na msaada wake unanitosha. Na nilipojifia, basi baada ya mimi kuoshwa na kukafiniwa Mpendwa wangu Akadhihiri ndani mwangu na baada ya kufa kwangu Akanijaalia maneno matamu na maongezi yaliyo safi zaidi kuliko maji yatiririkayo katika ardhi yenye changarawe na hoja thabiti inayoiuma batili kama nyoka wa kutilifikisha. Na hayo yote ni kutoka kwa Mola wangu. Mimi ni mikono mitupu nami nimeamrishwa kutumia mali hizi kwa watu wote, na kuzikarabati kuta za Islam kabla ya kubomoka. Na ajitokezaye kupigana nami, kwa hakika anajitokeza kupigana na Allah, Mola wa walimwengu wote. Mimi nimekuja katika mavazi ya maskini. Mimi kwa nguvu yangu siwezi kupita mwiniko wa ardhi wala bonde. Bali, Yupo pamoja nami Mweza Anayejificha Dhati yake lakini Anaonyesha hoja zake. Kwa hiyo maadui wameiepa njia yangu; makoo yao na shingo zao na vifua vyao vimefanywa vipande vipande na mtambo wangu wa kutupia mawe. Mtu hana uwezo wa kunikabili. Mkono wangu huu hufanya kazi chini ya kudura ya Mungu Rahmani. Baraka zimenishukia zilizo kimbilio la watu wema. Basi kwazo nikajipatia ngome madhubuti na sifa na

shukurani. Na katika karama zilizoadimika nilizojaaliwa ndiyo maneno yangu haya (kitabu hiki) yaliyo miongoni mwa miujiza. Kama mfalme yeyote atayarishe jeshi la maulamaa kwa kushindana nami katika kuandika maelezo ya Kurani kwa maandishi fasihi, basi Wallahi namtegemea Mungu Aliye Mkuu kwamba nitapata ushindi waziwazi juu ya maadui. Kwa lengo hili nilichapisha vitabu vingi na magazeti mengi mazuri na kuyaeneza duniani kote. Na nilimwelekeza kila mtu anayejiona shujaa katika uwanja huu kushindana nami. Masheikh wa nchi hii ni waoga, hawaweze kujitokeza kwa shindano ambalo kwalo nimewaita kwa amri ya Mungu Mwenye nguvu zote. Basi, ewe maskini Golarawii, u nani na una daraja gani? Ewe mpotevu, je unanuia kunishambulia ukiungana na wahuni na waovu wachache? Ewe uliyeghafilika, ujue kwamba mbingu imekuhudhurisha mbele yangu ili uwe mfano wa ibra kwa waishio ardhini. Takdiri imekuleta kwangu kwa kukuvuta ili Mola wangu Awaonyeshe watu heshima ya waliokubalika. Na tunaposhuka uani mwa kaumu, ndipo inakuwa asubuhi mbaya kwa wale walioonywa. Ee maskini, usiseme isipokuwa ukweli wala usishuhudie isipokuwa haki. Umche Mungu, usiwe na ujeuri. Je, unao uwezo wa kutoa maelezo ya Kurani kwa ufasaha na tamathali ya semi. *Subhanallah*, huo ni uongo dhahiri. Unajua vizuri kiwango cha elimu yako na vilevile wajua

elimu ya wenzako na wafuasi wako; juu ya hayo unajidai kuwa na fadhila kama wajanja. Maulamaa wanajua kwamba wewe si bingwa wa uwanja huu, lakini wanasitiri aibu zako kama vile ugonjwa wa ndani unavyofichwa na inajaribiwa kuweka katika siri. Basi, kwa neno zima, huna daraja hii. Mungu hakukufundisha elimu na ufasaha kutoka Kwake kama hiba wala hukujifunza maarifa hayo. Juu ya hayo ulipowasili Lahore ukadai kwamba bila kusita utaandika maelezo ya Kurani. Ulijifanya kipofu kwa kuruka mipaka yako au kwa kujasiri hukuweza kuona. Ukafanya uliyofanya. Ukajasiri katika kiburi chako na ukawadanganya watu kwa kuongopa na ukapenyeza ndani mwao uongo wako wa aina aina. Ukawalaghai sana kiasi hiki kwamba maneno yako ya kijahili yakaing'olea mbali kaumu na nyoka za hila yako wamewahiliki watu. Isitoshe, hukukosa nafasi yoyote ya kutukana na kuaibisha. U wa pekee katika ujeuri kutokana na kutusi na kufanya mzaha. Wewe ulikusudia kufika Lahore kwa tamaa ya kusifiwa na watu ili kwa nguvu ya mali na kushawishi uhesabiwe machoni pao miongoni mwa wasaidizi wa kaumu na waihurumiao dini na waponyaji wa huzuni, na kwamba kwa kitendo hiki usalimike na kulaumiwa na watu na usitawaliwe na mwisho mbaya na hasira; na ili watu wajue kwamba huna aibu ya kigugumizi, nawe si mwoga baina ya wenye ufasaha; na ili watu wa kawaida wafikiri kwamba umepewa elimu ya kila

aina na umejaaliwa neema mbalimbali za kielimu na umepewa busara inayofikia mwisho wa maarifa na rai sahihi ikamilishayo duara la maelezo. Na umejaaliwa ufahamu uuzuiao kila upotofu, na akili iwawindayo ndege za hoja kama furukombe; uneni uliosaidiwa na hoja zenye kukata shauri zing'aazo, na nafsi iliyopambwa na maarifa ya aina aina na ya uzuri wa batini, na kujaaliwa uwezo wa kuvutia kwenye mwongozo na ufunuo unaokufanya usimhitaji yeyote minghairi ya Mungu. Kisha kasoro iliyobakia katika majisifu walikamilisha marafiki zako kwa kukuunga mkono. Na nyimbo ziliimbwa kukusifu na haikubaki kasoro yoyote katika kupiga chuku kukusifu. Kisha baada ya kukuinua na kupandisha daraja wakanitusi na kunihakirisha. Yeyote waliyemwona au kutana naye wakanitaja mbele yake kwa dharau. Na wakala nyama yangu kwa kunisengenya na kwa kufanya hiyo wakala sumu ya kufisha. Basi kunihakirisha kwao kulipofikia kileleni na visu vya maneno yao vikaniumiza na hali ikafikia mwishoni mwake, na niliona kwamba wamefanya dhuluma ya kila aina na kurusha vumbi kama ng'ombe dume na wakaacha njia ya uadilifu na kufuata njia ya dhuluma, na umekithiri usemi wa ovyo na upayukaji, na mioyo na masikio vimechoka kusikia matusi na mawazo yamekuwa maovu na maarifa yamekadhibishwa na mambo ya kijinga yamesadikishwa, basi, ilitiliwa moyoni mwangu niwaokoe watu katika

uongo wao na nizime kwa kauli yangu ya kutoa uamuzi wa mwisho moto uliowashwa na upayukaji wao na niandike maelezo ya Kurani na kumwonyesha kila mdogo na mkubwa kwamba hao ndio waongo.

Kusudio la kufichua uongo wa huyu mdanganyifu lilinielekeza kwenye jambo hili (la kuandika Maelezo ya Kurani). Kwani alihadaa sana na kudhihirisha kwamba yu miongoni mwa masheikh wakubwa na kadai kwamba anajua elimu ya Kurani na anawashinda masheikh wenzake na wakati umewadia kwamba ashinde na asaidiwe. Lengo hasa la Maelezo yangu haya ya Kurani ni kupambanua baina ya giza na mwanga na kueneza harufu ya miski dhidi ya mzoga wa jangwani; na pia kudhihirisha udanganyifu wa mdanganyifu kuwahurumia wanaume kwa wanawake na kuwatendea kwa moyo wa upendo vipofu na wafuatao tamaa za nafsi ni shabaha ya maelezo haya ya Kurani. Kutekeleza jukumu hili la muhimu kulikuwa ni wajibu na deni la lazima ambalo halitanguki bila kulipa. Hii ndiyo sababu yenyewe iliyohamasisha mwito huu juu ya kuwa na shughuli zingine nyingi ili maelezo ya Kurani yapambanue kati ya waongofu na wapotevu. Kama huyu mwoga asingejifanya kuwa shujaa na asingetukana na kujigamba ningepita tu kama waungwana bila kumjali wala nisingemtupia mishale. Lakini kwa mikono yake mwenyewe amechana pazia

lake. Sasa msiba aliopata ni kutoka kwake mwenyewe tu. Alisema uongo mbaya na hakuogopa, bali alidanganya na akajaribu kuonyesha uongo kuwa ukweli na akawachochea watu duni dhidi yangu. Na akajiona kana kwamba yu mwenye kuonyesha miujiza na mtaalamu wa Kurani na mnywaji kutoka katika chemchemi ya maarifa na bingwa wa ujuzi wa elimu ya ndani. Hivyo, tukawajibikiwa kuwaonyesha watu hakika ya aliyoyadai na kuwadhihirishia haki aliyoficha, kwani ni vigumu kupambanua bila majaribio baina ya mfu na mzima. Na ninao uwezo wa kuonyesha farasi wake mlemavu kama farasi mwenye nguvu na punda zake kama farasi bora, lakini huu ni wakati wa vita sio wakati wa kusamehe makosa ya watu. Mwenye kiburi hapaswi kusamehewa makosa yake wala kusetiriwa aibu zake. Kadhalika haikumfaa mtu huyu kuepa mashindano haya na kujitoa wakati huu akijidai kuwa na elimu na kujihesabu miongoni mwa maulamaa waheshimiwa. Bali ilitakiwa kwamba akili yake itahiniwe na kujua uhakika wa shamba la elimu yake. Alidai kwamba amepakwa rangi ya ufasaha kama vile ngozi za wanyama zinavyopambwa kwa kutiwa rangi. Kama madai yake yalikuwa ya kweli na sahihi, basi alikuwa na hofu gani ya mashindano haya (ya kuandika maelezo ya Kurani) bali huu ulikuwa ni wakati wa raha na furaha sio wakati wa kuogopa na kutetemeka. Kwani, sifa zake zilizofichika zingedhihirika wakati wa mtihani wa

mashindano haya na maandishi na watu wote wangejua shani yake na daraja yake iliyofichika. Na ni dhahiri kwamba thamani ya mtu mkamilifu huzidi wakati wa kudhihirika ubora wake kama vile kisima kinavyopendwa wakati wa kunywewa maji yake matamu. Na siyo siri kwamba aliye stadi wa kueleza Kurani hufurahi sana anapoulizwa kuhusu baadhi ya maarifa ya Kurani, kwani anajua kwamba wakati umewadia wa kung'ara kwa nyota yake na saa imefika ya kutambulika kwake na maadui kufedheheka. Hivyo, hapatwi na huzuni wala ghamu anapoitwa na kukaribishwa kwenye mashindano bali huzidi kuchangamka na anaichukulia kuwa habari njema kwa ajili yake na fali njema kwa uongozi wake. Kwani thamani kamili ya mtaalamu hutambulika baada ya kuonekana mwanga wa mwezi wake mpevu; na shingo za watu zinamwinamia kikamilifu baada ya kudhihirika vipawa vyake vilivyofichika. Tumechagua Sura Al-Faatiha kwa mashindano haya kwani hii ndiyo asili ya kitabu na ufunguo wa Furkani na ni hazina ya lulu na marijani na ni kama kiota kwa ndege za maarifa. Hivyo, kila mmoja wetu anapaswa aandike maelezo yake ya Kurani katika ibara yenye ufasaha sana inurishayo moyo na zishabihiane na jua katika baadhi ya sifa zake za ndani ili watu wapate kuona waziwazi kwamba nani kati yetu amekaa kileleni pa ufasaha na yupi kati yetu ni bingwa wa umbuji, ili huyu mtaalamu ajulikane ambaye akili yake

imemleta kwenye lengo hili, na mwandish yule abainike ambaye ufahamu wake umemleta kwa kusukuma kwenye bustani ya Arabuni, na ili kila mmoja wetu awakondeshe farasi zake wa aina bora kwa kuwakimbiza katika mashindano ya mbio kwa kupata lengo lake; na apite kila njia ya bonde na mlima kwa masurufu ya kalamu yake na wino ili watu washuhudie kwamba nani amejaaliwa msaada wa Mungu na mkono wa ***Samadiyyat***[3] umemwauni nani. Na kwa yule anayedai kuwa mtaalamu wa mambo ya kiroho si vigumu kuandika maelezo ya ***Sab' Mathaani*** (Sura Al-Faatiha) kwa ufasaha na kuzingatia maana adimu za maadishi bora. Kisha nikamlegezea kabisa hatamu na nikamwachia nafasi katika mazungumzo ili aweze kuandika kwa urahisi. Hapo awali niliandika katika tangazo nililochapisha na katika barua niliyomwandikia kwamba kama huyu maskini haliwezi jambo hili basi ana hiari ya kulishirikisha pamoja naye kundi la masheikh au kuliita kundi la waandishi kutoka Arabuni au awaombe watawa wa kaumu yake kumwombea kufanya kazi hii ngumu. Nilisema kauli hii kwa lengo hili tu ili watu wajua kwamba hao wote ni majahili na yeyote kati yao hana uwezo wa kuandika maelezo mithili hii. Haitakuwa sawa kusema kwamba mtu huyu aliyeitwa kwa mashindano

---

[3] ***Samadiyyat*** ni sifa ya Mungu, inayomaanisha kwamba Mungu ndiye asiyehitaji lakini wote wanahitaji kwake. Mwenezi.

zamani alikuwa mtaalamu lakini sasa mara elimu yake imepotea kama vile barafu ipoteavyo ikiyeyuka na kwamba buibui za usahaulifu wametengeneza tando juu yake. Kwani, elimu anayodai na aliyoikumbuka kwa ghaibu na kuihifadhi na kuikariri-kariri ilikuwa lazima kwamba ingekuwa kwa ajili yake kama maziwa ya mama yaliyomstawisha, au ingekuwa kama taa iliyoangaza sana nyumba yake na kuimulika. Basi yawezekanaje elimu hiyo ipotee haraka hivyo na ubongo ubaki mtupu kama chombo kilichotoboka. Na yawezekanaje hisia na moyo vipate kufikiwa na maafa hata kwamba katika muda mfupi tu pasibaki moyoni hata herufi moja. Na yawezekanaje upepo mkali wa usahaulifu kuzivumia zile elimu zilizofunzwa kwa kutokwa jasho na kavumilia shida nyingi za muda mrefu! Hata kama tukifikiria kwamba maafa ya usahaulifu yameung'olea mbali mti wa elimu yake na ameangukiwa na radi za bahati mbaya kwenye busara yake, lakini tuwezeje kufikiria kwamba balaa hili limewaangukia maelfu ya masheikh walioamuliwa kuwa washiriki wake nao wanashirikiana naye kumsaidia kubeba mzigo wake. Bali aliruhusiwa kuwaita waandishi ambao aweza kuwapata, huenda wakaweza hivyo kuandika maandishi yenye ufasaha, na asihangaike kama ngamia kipofu. Kisha hili ni jambo la kukubalika kwamba Mungu huzidisha akili za watawa na kwa kuwaongoza kwenye njia za watu wa kiroho Huwafanya kuwa wenye

bahati njema; na Huwakumbusha wanaposahau maarifa ya Neno la Mungu Mtakatifu na huwateremshia utulivu mioyoni mwao na kuwasaidia kwa Roho takatifu kutoka kwake; na Huwasaidia kwa auni yake wakati wa kutoa maelezo na kusimamia mambo yao yote na kuwapambanua kwa akili na uthabiti na Huwaweka mbali na usafihi na kuwalinda na upotevu na kuwahifadhi katika usimilizi na uelewa. Basi (watu wema) hawapati kujuta wala hawaoni siku ya fedheha na hasara; nuru zao hazififii wala nyumba zao haziachwi, chemchemi zao hazikauki, wala kazi zao hazivurugiki. Husaidiwa katika nyanja zote na hujaaliwa kila aina ya maarifa na kuwekwa mbali na kila ujahili. Hawafi mpaka nafsi zao kujaaliwa utimilifu; na pindi zinapokamilishwa, hurejeshwa kwa Mola wao. Mungu ni nuru, hivyo huelekea kwenye nuru; suna yake ni kuwakimbilia waliokamilika. Kwa kuwa dasturi na suna ya Mungu ndiyo hii kwa mawalii, wasalihina na watawa wake, basi ni lazima kwamba mja wake aliyekubalika asione dhila wala asinasibishiwe udhaifu wala ila yoyote wakati wa kukabiliana na mtu wa dini yoyote, na awashinde wote wakati wa kutoa maelezo ya Kurani kwa elimu na maarifa yake ya aina aina. Na bila shaka imesemwa kwamba walii hudhihirika kutokana na Kurani na Kurani hudhihirika kutokana na walii. Na bila shaka hazina za Kurani zilizofichika hazidhihiriki isipokuwa kwa yule adhihiriye kwa mkono wa Mungu

Mjuzi Mtukufu. Hivyo, kama yupo mtu mwenye ufahamu mkubwa wa pekee, huyo ndiye kama yule aliyetoa dafina moja bila taabu wala wasiwasi, basi huyu ni walii wa Mungu na shani yake ni adhimu sana na dhati yake ni juu kabisa kuliko ukusoaji wa mkusoaji. Na yale maarifa ya Kurani anayopewa walii aliyejipoteza ndani ya huba ya Mungu, vitu atakavyohitaji safarini ndio muujiza bali ni bora kuliko kila aina ya muujiza. Niambieni muujiza upi ni mkubwa kuliko muujiza ulio kivuli cha Kurani na hushabihiana na Neno la Mungu kwa sababu ya kuzidi uwezo wa binadamu. Na daraja hii ni mahsusi kwa wacha-Mungu tu na milango hii hufunguliwa kwa watawa pekee. Mtu yeyote hawezi kuyagusa maarifa ya Kurani isipokuwa waliotakaswa. Na Mungu Haishindishi hila ya wahaini waliotumia ulaghai kuwa njia ya kujichumia riziki, na wameyafanya mambo yao ya uongo kuwa makimbilio yao. Nyoyo zao ni kama usiku mrefu sana na kama giza lililoenea mpaka upeo wa macho. Hawajui Kurani ni nini, elimu na maarifa ni kitu gani. Mtu asiye na elimu ya Kurani wala hakupewa tamathali ya usemi, huyu ndiye shetani au hushabihiana na shetani; yeye hakumtambua Mungu Rahmani. Na fasiki hawezi kufikia matamanio ya hali ya juu hata kama akiiharakisha kwayo nafsi yake duni; bali yeye hushika njia ya kukimbia akihofia fedheha ya kuaibika na kudhihirika kosa lake. Na ndivyo alivyofanya huyu mtu mjanja na mwindaji

mwongo. Tazameni namna alivyopamba uongo na kujiasiri na akasema kwamba nimeshakubali mwito ilihali hakuukubali. Na pia alisema kwamba nimeshatayarisha jeshi kwa mashindano ilihali hakutayarisha. Na hakujitokeza katika medani ya mashindano, bali alihadaa na kudanganya na kurejea katika shimo lake; amedhihirika kusinyaa na kufinyaa ilihali alijidai kuwa pande la mtu. Akagandama kwenye ardhi na kufanana na kenge. Hakupanda juu wala hakusimama imara, akawakusanya watu waovu, na hakumwita Mola. Alinihakirisha na kunitusi. Alifanya hila na hakujenga uhusiano wa ikhlasi na upendo kwa Mungu. Kwa ajili ya Mungu hakujitenga na wengine wala hakuachana nao. Na akadai kwamba yu mtaalamu ilihali nyota ya elimu yake imeshatua. Na kila alichopanga kimeangamia. Kama kweli yu mtaalamu, basi kuna shida gani kwa mtaalamu kueleza sura yoyote moja kati ya sura za Kurani na kuandika maelezo yake katika lugha ya Kurani. Bali angesifiwa kwa moyo wa kweli kama angefanya hivyo na ingejulikana kwamba yu miongoni mwa watu wa fadhila na elimu na ufasaha na kushukuriwa kwa kuwafaidisha watu kwa maarifa aliyofundishwa na Rahmani. Kwa hiyo, nasema kwamba anayedai kuwa kwenye kilele cha daraja ya juu yuapaswa ajibidiishe awezavyo na kuthibitisha kwamba yu kama farasi bora na madhubuti. Bila shaka kudhihirisha ukamilifu ni sera ya wanaume na mwenendo

wa mashujaa ili kwa njia hii watu wajifaidishe na mtu yeyote maskini atoke katika jela ya upotevu. Mtu yeyote mkamilifu hatavumilia kuishi kama mtu asiyejulikana bila kutambulika na kuwa mtu wa kawaida tu bila kuwa mtu maalumu. Fadhila yoyote haithibitiki bila ufasaha; jua haliwezi kutambulika pasipo kueneza mwanga ardhini. Na nimejilazimisha kuandika maelezo yangu ya Kurani kwa kuthibitishia ujumbe niliopewa na Mungu na kufungua milango hii kwa ufunguo wa sura Al-Faatiha kwa maelezo mepesi na adhama ya maandishi na kwa kuzingatia ufasaha wa Kiarabu. Jambo hili li wazi fika kwamba kuandika mambo mepesi ya dini na elimu zilizofichamana na kinaya na madokezo kwa maandishi yaliyopambwa, isitiara njema, tamathali nzuri za usemi, maelezo mema na madokezo mepesi, huhesabiwa kuwa ni jambo mushkili na kazi ngumu. Mambo haya mawili yanayokinzana yamejumuishwa na Kitabu cha Mungu kidhihirishacho aya bayana na kufutilia mbali mambo ya kijahili. Washairi hawawezi kuthubu katika uwanja huu wa ufasaha. Maneno yao hutawanyika kama nzige waliosambaratika. Lakini kitu nilichomwomba Mungu Akanipatia. Nilimfikia nikiwa mwenye kiu, Akanitosheleza. Sisi ndio tuliojaaliwa uwezo na kusaidiwa na Mungu. Kalamu zinatusaidia kana kwamba zi mshale na upanga. Tumejaaliwa kutoka kwa Mola wetu maneno matimilifu na kivuli kinene. Kila vazi tujivalialo

lapendeza. Na tuna tabia halisi ambako hata milima haiwezi kufikia na nguvu ambayo mizigo mizito pia haiwezi kuilemaza, na hali ambayo nguvu zozote haziwezi kuigeuza, na Mola ambaye kutoka Kwake matarajio hayakataliwi. Kwa neno zima, mimi nimetoka kwa Mungu na maneno yangu pia ndiyo kutoka kwa Mjuzi Huyu. Nimeandika madai yangu na hoja zake katika kitabu hiki kwa kumtimilizia mpinzani haja yake na kumwondolea wasiwasi. Kwani, baada ya mimi kumwita kuandika maelezo ya Kurani kwa ufasaha na kutumia istiara bora, yeye akaanza kuniita kufanya mijadala. Na nilipojitenga na mijadala akakuchukulia kukataa kwangu kuikimbia vita hii. Na hii ilikuwa ni hadaa na hila yake ili aepukane na lawama ya wanaume na wanawake wenye kulaumu. Alijua vizuri kwamba kujitenga kwangu na mijadala kulikuwa kwa sababu ya ahadi yangu ya zamani, nami si kama mtumwa mtoro. Lakini yeye alitaka kukimbia kwa udhuru mbovu ili watu wamwelewe kuwa shujaa na mwenye kutimiliza hoja. Basi, sasa tumenuia kumtimizia utashi wake na kumrudisha pasipo kunyimwa. Na tunurishe ukweli wetu kwa nuru ya hoja na tukate vipande vipande udhuru wake wote kwa upanga wa maelezo. Huenda kwa njia hii Mungu Akaondoa kutu za ufahamu wao na kuwafahamisha jambo ambalo hawakulifahamu kabla ya kuingia uwanjani. Basi hii ndiyo sababu ya kuandika madai na hoja ili usibaki udhuru

wowote kwa mwulizaji. Maelezo haya ya Kurani yamejumuisha mijadala yote kwa elimu nyepesi na maarifa. Hivyo, leo adui amepata yote aliyoyataka kutoka kwetu katika sura za mijadala; na juu ya hayo akatendea kunyima haki na kufanya hiana. Deni yetu imebakia, basi ni jukumu lake kurudisha deni kama amana zinavyorudishwa. Mimi nilimwahidi Mungu kwamba sitahudhuria mijadalani nami nimeshachapisha ahadi hii katika vitabu vyangu. Basi haikuwezekana kwangu kuvunja ahadi na kumwasi Mola wangu Mpenzi. Basi kwa hiyo nilifunga mlango wa mijadla, na sikumwendea mpinzani wangu kwa kujadili ingawa alinikosoa na kunisengenya. Na niliongea naye kama rafiki mwenye uhusiano mwema lakini aliniumiza kwa kunitusi. Nilimwita hapo kabla pia lakini alikimbia kuona heshima yangu kisha nilimwita mara ya tena lakini akaiogopa heba yangu. Na sasa ni mara ya tatu ili kumtimilizia hoja ya Mungu na hoja yangu. Yeye alielekea kwenye raha zake na tukaelekea kwenye majukumu yetu. Mambo ya maarifa tuyaelezayo ni kama majeshi kuwekwa mipakani na mfalme wa nchi. Kisha mjue kwamba kijitabu changu hiki ni ishara mojawapo kati ya ishara za Mungu, Mola wa walimwengu, na ni ujumbe wa kuangazia busara kwa watafutao haki. Hii ndiyo hoja imara na buruhani wazi kutoka kwa Mola wangu. Hii ndiyo ili kuwaonjesha kidogo waongo matokeo ya dhambi zao na kuwaonyesha

watu yatiririkayo kutoka katika ndoo yao na kuzivunjilia mbali mbavu zake kwa muujiza mkubwa, wasiweze kulala kibavu kwa amani na kuufutilia mbali utulivu wa uwongo wa nyoyo zao. Na hii ni haki, na haki tu ndiyo naisema, kwamba maneno haya ni kama upanga unaokata kabisa na bila shaka imeyakatakata mabishano yote na baada yake haukubaki ugomvi wowote. Na yule mtu ambaye anadhani kwamba yu fasihi na anayo maandishi kama mwezi mpevu, basi anapaswa kuleta mfano wake na kunyamaza kuwe haramu kwake. Na kama wakijumuika baba zao, wazao wao, wenzao, maulamaa wao, wataalamu wao na fakihi wao kwa kuleta mfano wa maelezo haya ya Kurani yaliyoandikwa katika muda kidogo , katu hawataweza kuleta mfano wake hata kama wasaidiane wao kwa wao. Niliomba kuhusu jambo hili na bila shaka dua yangu ilikubaliwa, hivyo hatapata uwezo wa kuandika jibu la maelezo yangu mwandisi yeyote, si mzee wala kijana. Na bila shaka maelezo haya ni hazina ya maarifa na mji wake na ni msingi wa kweli zisizoepukika. Na utaratibu wa maandishi yake ni mwepesi mno ni mzuri sana kwa tamathali ya usemi iliyojaa hekima nyingi, na maneno yake ni bora sana, maneno machache lakini yenye maana nyingi, maelezo bayana na adhimu. Na sikuyaandika maelezo haya ya Kurani kwa nguvu yangu. Mimi ni dhaifu na maandishi yangu pia. Lakini hayo yote ni kwa sababu ya Mungu na

ukarimu wake kwamba Alinipatia ufunguo wa hazina zake za maelezo. Na kutoka kwake Yeye nimejaaliwa siri za dafina zake. Nimekusanya ndani yake maarifa ya aina aina na kuyapanga kwa utaratibu. Nilisimamisha safu-safu farasi za maneno yenye hekima kuwavalisha hatamu. Aliyeyatambua basi akaitambua Kurani na aliyeyadhania kuwa uongo, akaongopa. Ndani mwake mna matunda mapya mapya ya maarifa na mambo mepesi ya sura Al-Faatiha na Furkani. Na ndani yake mna miji na ngome za madokezo na elimu iliyofichika, na nyanja na safu za milima ya elimu ya kweli na chemchemi za busara na macho yenye nadhari, na hupanda farasi wa hoja na rikabu zao. Na hayo yote ni baraka za Ummul Kitaab (Sura Al-Faatiha), nilizijua baada ya kufahamishwa na Mola wangu Mwenye kupokea toba. Hii ndiyo Sura ambayo uwanja wake hauwezi kuvukika hata kwa kuwakimbiza rikabu kwa mbio sana hata kuwakondesha. Nuru ya nyota pia haifikii nuru yake. Wakati wadhalimu waliponinasibishia ushinde, basi uongo wao ulinilazimisha kuandika maelezo ya Sura Al-Faatiha ili nijiokoe katika magego na machonge yao, kwani shambulio la mbwa si kali kuliko shambulio la mzushi kadhabu. Maelezo ya Kurani ndiyo kwa sababu ya fadhili ya Mungu na rehema yake ili yawe ishara kwa waaminio na majuto kwa wakanaji na hoja dhidi ya kila mpinzani mpaka siku ya kiama na mwongozo kwa wamchao

Mungu na ili watu wajue kwamba ushindi hupatikana kwa kusema kweli sio kwa kujivunia kama majahili. Ushindi hupatikana kwa utakaso wa moyo sio kwa maneno machafu kama mkojo na kinyesi; na urekebisho wa hali hupatikana kwa silaha ya elimu na ukamilifu sio kwa hila na ulaghai wala fahari na kiburi. Ole wao ambao walikusudia kupata ushindi kwa hila na udanganifu na kukaa mafichoni kama mwindaji. Na ushindi huja kutoka kwa Hakimu wa mahakimu; Humsaidia amtakaye na Huwatoshelezea watawa. Basi majeruhi wao hupona na waliochoka hupata raha. Heshima yao haipunguki na taa zao hazizimiki. Na asaidiwaye na Mungu hujazwa elimu ya Kurani Tukufu na lugha ya Kiarabu kama vile ndoo inavyojaa maji tele. Na huyo ndiye mimi na siyo fahari. Dua yangu huyeyusha mwamba. Siku yangu hii ni siku ya ushindi na siku ya mwanga baada ya usiku wa kiza totoro. Leo wenye midomo michafu wamepigwa na bumbuazi na mikono yao imefungwa vikali mpaka siku watakapofufuliwa. Nilikuwa nikitufu kurasa za Kurani kama vile mwombaji azungukavyo katika mitaa. Basi, Mungu akanionyesha aliyonionyesha na kuninywesha alichoninywesha. Na jinsi alivyoniongoza nikapata sawa nayo njia hizi (za Kurani), na akanipatia nilichomwomba na nilifunguliwa nami nikaingia. Na niliyoyaandika ni kwa sababu ya maneno matukufu ya Mungu Mjuzi, sio kwa kukimbiza farasi za kalamu. Sina haki ya kusema kwamba

najua zaidi kuliko wengine au juhudi zangu zimezidi juhudi zao wala sisemi kwamba roho yangu imeungana na roho za vijana waliokuwa waandishi hodari au kwamba nimejipatia ustadi mkamilifu juu ya mazuri yote ya uandishi. Wala sidai kwamba nimefika kileleni katika ufasaha au kwamba nimekula matunda yote mapya ya maana bora na teule. La, bali niliwaita waandishi wakaao paziani, hapo wanawali wa maandishi wakaja kwangu na kijana wa maandishi akawapokea kwa tabasamu na uchangamfu. Basi msiniulize habari za mwandishi. Mimi ni kama msafiri katika mji wa uandishi, na yote muyaonayo kwangu ni kwa msaada wa Mola wangu na ni kutoka kwa Yule ambaye nimeweka shingo yangu mbele yake na kumpelekea mahitaji yangu yote. Yu mahabubu wangu katika akhera na katika dunia hii. Kwa yakini mimi ni Masihi wake na ngome ya ulinzi wangu ndiyo rikabu yangu na rehema Yake ndiyo saruji yangu. Kama isingalikuwa fadhili ya Mungu na rehema yake, maneno yangu yangalikuwa kama takataka ya mkusanya kuni wakati wa usiku au kama taka za mafuriko. Na wallahi, sikuweza kuandika maelezo haya kwa sababu ya sifa yangu hasa ing'aayo, bali hii ndiyo fadhili ya Mungu na bahati njema. Uso wa aliyejivalia hijabu haukufunuliwa kwa mikono yangu mifupi, bali hilo limefanyika kwa fadhili ya Mungu na ukarimu Wake usio na mipaka. Kwani Aliiona Islam kama mgonjwa anayekaribia kufa na

aliyeko juu ya jiwe kama matawi makavu ya jangwani, dhila iko juu yake na joho lake limeraruka. Hapo Mungu Akaja wakati wa ukame kama mvua kuisaidia Islam na Akauosha uso wake na kuuondolea mbali uchafu wa miaka na miaka Akiumwagia maji safi. Basi, alimtuma mtumishi mmoja kati ya watumishi wake kwa kutimiliza hoja na Akaweka muujiza katika maneno yake ili yawe kivuli cha muujiza wa Nabii[saw], maelfu ya rehema na salamu ziwe juu yake. Na kwa muujiza huu, utukufu wa Neno la Mola wa walimwengu haukupungukiwa kitu kwani karama huwa kivuli tu cha miujiza. Na kadhalika Mungu Akaangamiza kila walichopanga maadui kama mwindaji hodari na Akaharibu kila njama waliyoifanya na kubatilisha kila hila na hadaa waliyoipanga na kila mkuki walioupeleka mbele Akaurudisha nyuma na kuitangua kila hila waliyofanya na kubomolea mbali ngome zote madhubuti walizozijenga na kuzima ule moto waliouwasha, na kufunga njia zote walipotaka kukimbia. Basi haikuwa katika uwezo wao kujitokeza kama mashujaa wa uwanjani mwa mapigano wala kujitoa katika kifungo kuruka mahandaki na kuta. Wakati wowote waliposonga mbele wakarudishwa nyuma kwa adhabu za aina aina mpaka ukawadia wakati wa kuandika maelezo haya ya Al-Faatiha ambayo ni mshale wa mwisho katika mishale ya podo. Tumeshakamilisha maelezo haya kwa fadhili ya Allah Jalali nayo ndiyo madhubuti na imara zaidi kuliko

milima, yakawa kama ngome madhubuti iliyojengwa na mawe mazito, yamefikia eneo la muujiza kutoka kwa Allah Mtendaji sana nayo yamelindwa pia na nia mbaya ya adui mpotevu aliyefukuzwa kizingitini pa Mola. Na kwa njia ya hayo tumeshalipiza kisasi kiasi fulani na tumeyang'olea mbali mahema na kanopi walizokuwa wamepigilia katika medani ya vita. Kazi hii ilikuwa ngumu sana lakini Mungu Akairahisisha kwangu, na Akasogeza karibu nami iliyokuwa mbali na kuihamisha faraja ya adui kwenye dhiki. Akapofusha macho yake na Akamwondolea uwezo wake wa elimu na maarifa na kuwatilia heba mioyoni mwao na kuwakamata kwa madhambi yao. Hapo wakasarenda na kuwaacha ngamia zao wenye kutoa maziwa na wakamaliza maji yao pia yaliyosalia na kuangusha mahema yao na kufanya mapodo yao kuwa matupu na kutupilia mbali ala zao na wakawa hawajiwezi ilihali waliruhusiwa waje na majeshi yao yote yaani wapanda rikabu, waenda kwa miguu, magenge, jeshi kubwa, vikosi na kombania. Lakini wakawa kama maiti aliyezikwa au kama mafuta ya taa yaliyokwisha teketea na hayakubakia na mwanga wake. Na tuliwanyamazisha wale waliotukabili, wadogo kwa wakubwa wao. Na tuliweka saruji juu ya punda zao wote waliao ili wasiweza kutikisika pale walipo au wasiweza kuelekea kwenye mkuki baada ya kuzinduka katika kusinzia. Bali, tumejaribu tangu mwanzo mpaka wakati huu kwamba watu hao hawana moyo wa

kutukabili katika mashindano. Hawana chochote isipokuwa kutukana wakikaa vyumbani kama wanawake. Huikimbia kila hali ngumu na hatari ilhali nguo zao zilizochakaa zaonekana chini ya mavazi yao ya juu. Kisha hawakiri wala hawajuti, hawamwogopi Mungu wala hawajizuii. Maelezo haya ya Al-Faatiha ni mshale kwake na jeraha la maneno huenda wakatanabahika na kuelekea kwa Mungu wakitubu. Na tumeyawekea maelezo haya sharti kwamba kundi lolote kati yetu lisichukue siku zaidi ya sabini na atakayechukua siku zaidi, basi maelezo yake hayatakubaliwa naye atapaswa kulaumiwa. Na vilevile lilikuwa sharti kwamba maelezo yasipungue juzuu[4] nne, na masharti haya yalikuwa sawa baina yangu mimi na mpinzani wangu. Nasi tumeshatangaza masharti haya hapo kabla na baada ya kuyachapisha tumeshawafikishia kimaandishi marafiki na wapinzani. Sasa twaanza kuandika maelezo (ya sura Al-Faatiha) kwa msaada wa Mungu Msaidizi na Mweza. Na tumeyapanga katika milango michache ili yasiwe yasiyovumilika kwa watafutao haki. Isitoshe, tumefuata njia ya wastani, si kwa muhtasari uvurugao madhumuni wala si kwa urefu umchoshao msomaji.

Maelezo haya kwake (Mihr Ali) kutoka kwangu ni kama mtoto wa mwisho wa mzee, aliyetolewa kutoka tumboni

[4] Juzuu, moja katika istilahi ya uchapaji ya zamani ilimaanisha kurasa 16. Basi Juzuu 4 ni kurasa 64.

mwa kudura kwa rehema ya Mungu Mwenye shani, katika siku za saumu na mausiku ya rehema, nami nimeyaita

“اِعْجَازُ الْمَسِيْحِ فِيْ نَمَقِ التَّفْسِيْرِ الْفَصِيْحِ”

yaani ‘Muujiza wa Masihi katika sura ya maelezo fasihi’. Nilionyeshwa ruya itoayo habari njema, usiku wa Jumanne, nilipomwomba Mwenyezi Mungu kwamba Ayafanye maelezo haya muujiza kwa maulamaa. Pia niliomba dua kwamba mwandishi yeyote asiweze kuleta mithili yake wala wasijaaliwe uwezo wa kuandika. Basi dua yangu ikakubaliwa katika usiku huo huo uliobarikiwa na Mwenyezi Mungu, na Mola wangu Akanipa habari njema akisema “Mzuiaji kutoka mbinguni Amemzuia”. Hapo nikaelewa kwamba hii inaashiria kwamba maadui hawatayaweza, wala hawataleta mithili yake wala maelezo yenye sifa mbili (ufasaha na kweli za ndani). Na bishara hii nilipewa kutoka kwa Mungu Manani katika kumi la mwisho la Ramadhani ambamo Kurani ilishushwa. Kisha baada yake ndani ya muda huo maelezo haya yaliandikwa kwa msaada wa Mungu Mweza. Ee Mola wangu, Uielekeze mioyo ya watu kwayo na kuyafanya kuwa kitabu kilichobarikiwa na Ukiteremshie baraka kutoka kwako. Tumekutegemea, basi tuletee msaada kutoka Kwako na Utusaidie kwa mikono yako. Na tutoshelezee mambo yetu jinsi Ulivyowatoshelezea watawa waliopita mahitaji yao na Utukubalie maombi yetu yote haya. Twahudhuria mbele Yako kwa unyenyekevu basi Uwe wetu katika dunia na dini. Amin.

MLANGO WA KWANZA

(Majina ya Sura hii na mambo mengine yahusianayo nayo)

Ujue kwamba Sura hii ina majina mengi. Jina la kwanza ni Faatihatul Kitab, na imeitwa jina hili kwani Kurani, sala na kumwomba dua Mola wa mabwana wote vyaanzia nayo. Na kwangu mimi, hii imeitwa Al-Faatiha kwa sababu Mungu Ameifanya kuwa 'mwamuzi' kwa Kurani na humo mmejazwa na Mungu Manani habari na elimu za ndani, na imejijumuishia kila anachohitaji mwanadamu kwa utambuzi wa mwanzo na mwisho, kwa mfano, uthibitisho juu ya uwepo wa Mwumbaji wa kweli, haja ya unabii na ukhalifa baina ya waja wa Mungu. Na habari yake adhimu na kubwa zaidi ni hii kwamba sura hii yabashiria zama za Masihi Mau'udi na wakati wa Mahdi wa ahadi; tutaieleza habari hii katika mahali pake kwa kuwezeshwa na Mungu Wadudi. Na katika habari zake, mojawapo ni hii kwamba inabashiria umri wa dunia hii duni, nasi tutaiandika pia kwa kujaaliwa uwezo na Mwenyezi Mungu. Na hii hii ndiyo Al-Faatiha aliyoitolea habari yake nabii mmoja miongoni mwa manabii. Yeye akanena: Mimi nilimwona malaika mwenye nguvu akishuka kutoka mbinguni, mkononi mwake mna Sura Faatiha kwa sura ya kijitabu. Kwa amri ya Mola Mweza, akaweka mguu wake wa kulia juu ya bahari na wa kushoto juu ya nchi. Na akatoa sauti kubwa kama vile simba angurumavyo na kwa sauti yake radi saba

zikadhihirika na katika kila radi mlikuwa na maneno na ikasemwa yatie muhuri yaliyosemwa na radi hizo, wala usiyaandike. Hivyo ndivyo alivyosema Mola Wadudi. Na malaika aliyeshuka akaapa kwa Mungu Mzima wa milele Ambaye nuru yake imeangaza bahari na biladi kwamba hazitakuwa zama zenye shani kama hii baada ya zama hizi. Waelezaji wa Kurani wameafikiana kwamba bishara hii inazihusu zama za Masihi Mau‘udi wa Mungu. Basi zama zile zimeishawadia na sauti saba za aya saba zikaririwazo (Sura Al-Faatiha) zimeshadhihirika. Na zama hizi kwa heri na mwongozo ni kama zama za mwisho na baada yake hazitakuwa zama zozote mithili yake katika fadhili na daraja. Na tutakapoaga dunia hii, hakutakuwa na Masihi yeyote baada yetu mpaka siku ya kiama, hatashuka yeyote kutoka mbinguni wala hatajitokeza kutoka pangoni isipokuwa yule mtu ambaye kuhusu dhuria [5] yake Mola wangu Ameishatangulia kusema. Bishara hii ndiyo haki. Na aliyetakiwa kushuka kutoka kwa Mungu ameishashuka, mbingu na ardhi zamshuhudia, lakini nyinyi hamna habari ya ushahidi huo;

---

[5] اِلَيْهِ اِشَارَةٌ فِيْ قَوْلِهٖ عَلَيْهِ السَّلَامُ: يَتَزَوَّجُ وَيُوْلَدُ لَهٗ۔ منه

Kwenye hii hii imeashiriwa katika kauli yake, amani juu yake: Masihi Mau‘udi ataoa na atajaaliwa kizazi.

Hadithi ya Mtume[saw] inaiashiria kwamba Masihi Mau‘udi ataoa na atapewa kizazi. Mwandishi

na baada ya kupita wakati huu mtanikumbuka. Lakini mwenye bahati njema ni yule aliyepata fursa na hakuipoteza kwa uzembe. Sasa twarejea kwa somo letu la awali. Basi enye wenye akili, nisikilizeni. Sura Faatiha ina majina mengine pia, mojawapo ni *Suratul Hamd*, kwani inaanzia na hamdu ya Mola Mtukufu. Na jina lake lingine ni *Ummul Kur'aan* kwani hii imejumuisha masomo yote ya Kurani kwa maelezo mazuri sana na imejikusanyia ndani yake lulu zote za Kurani Tukufu kama chaza, na kwa nyuni za maarifa ni kama kiota. Kwa yakini Kurani imejikusanyia elimu zote za aina nne katika miongozo yake: elimu ya mwanzo, elimu ya akhera, elimu ya unabii na elimu ya Tauhid ya dhati na sifa za Mungu. Na hakuna shaka kwamba elimu hizo zote za aina nne zimo katika sura Al-Faatiha na zimezikwa katika vifua vya maulamaa wengi wa umati huu; wanaisoma Al-Faatiha lakini haipiti kooni mwao kuingia tumboni. Hawaitiririshi mito yake saba, kwa kuipasua, bali wanaishi kama wapujufu. Na yumkini Sura hii imeitwa *Ummul Kitaab* kwa sababu mafundiho yote makamilifu yanapatikana katika Sura hii, kwani safari ya wasafirio kwenda kuungana na Mungu haikamiliki mpaka itawaliwe mioyo yao na heshima ya Umola wa Mungu na unyenyekevu wa kibinadamu. Na hutapata kabisa mwongozi katika jambo hili kutoka kwa Mungu Mmoja kama Sura hii. Je, huoni kwamba kuanzia اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ mpaka مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ namna

gani Mungu Amedhihirisha heshima na adhama Yake. Kisha katika aya اِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسۡتَعِيۡنُ Amedhihirisha dhila ya mtu na unyonge na udhaifu wake. Na pia yumkini kwamba sura hii imeitwa Ummul Kitaab kwa kuzingatia mahitaji yote ya asili ya kibinadamu na lengo lenyewe ni kuashiria kwenye yale zinayotaka tabia za asili kupitia juhudi ya mtu au mvuto wa Mungu. Kwani, mtu hupenda kwa kujikamilisha nafsi yake kwamba apate ujuzi wa dhati, sifa na kazi za Mungu na anataka hii pia kwamba apate elimu ya radhi Zake kwa kupitia amri zake ambazo hakika yake hudhihirika kwa kauli zake. Na kadhalika ruhania yake yahitaji kwamba ukarimu wa Mungu umsaidie na apate kwa msaada Wake utakaso wa batini, mianga na kashfi za Mungu. Na Sura hii tukufu imejijumuishia maana hizo, bali kwa uzuri wa maelezo yake na nguvu ya ufafanuzi wake inavutia kwenye maana hizo. Na jina lingine la Sura hii ni *Assab'ul-mathaani*. Sababu ya jina hili ni kwamba hii ina sehemu mbili: nusu yake ni ya mtu kumsifu Mola wake, na nusu ya Mola kumkarimu mja wake ajipotezaye ndani Yake. Na imesemwa kwamba imeitwa *Al-mathaani* kwa sababu haimo ndani ya Vitabu vingine vyote vya Mungu wala haipatikani mithili yake katika Torati wala katika Injili wala katika Vitabu vingine vya Manabii. Na hii pia imesemwa kwamba imeitwa *Mathaani* kwa sababu ina aya saba kutoka kwa Mungu Mtukufu na usomaji wa kila aya

ni sawa na usomaji wa sehemu ya saba ya Kurani Tukufu. Na imesemwa pia kwamba imeitwa ***Saba*** kuashiria kwenye milango saba ya jahanamu. Kila mlango umewekewa sehemu maalumu ya sura inayoondoa mwako wa moto kwa idhini ya Mungu Rahmani. Kwa hiyo anayetaka kupita kwa usalama katika milango hiyo saba ya jahanamu, basi ni jukumu lake kwamba aingie katika aya hizi saba na kuzipenda na kumwomba Mungu Mweza Amwimarishe juu yao. Yale maovu yahusianayo na hulka, amali na itikadi, yanayoingiza motoni, ndiyo saba kimsingi yaangamizayo. Na aya hizi saba zaokoa katika taabu hizo. Katika Hadithi kuna majina yake mengine pia lakini kiasi hiki chakutosha. Basi, Sura hii ni hazina ya mambo yaliyofichika. Isitoshe, kuiwekea mpaka idadi hii kunaashiria kwenye miaka ya zama tangu mwanzo hadi mwisho; namaanisha kwamba aya zake saba zinaashiria kwenye umri wa dunia, ambao ni miaka elfu saba. Na kila aya kati ya hizo yaeleza hali ya miaka elfu. Na elfu ya mwisho imezidi sana katika upotevu. Na sehemu hii inahitaji maelezo haya, kwani Sura hii yatosheleza kueleza habari za tangu mwanzo mpaka mwisho. Kwa neno zima, Sura Al-Faatiha ni ngome imara na nuru dhahiri na mwalimu na msaidizi. Na hii yalinda amri za Kurani na mazidisho na mapunguzi kama vile mipaka inavyolindwa kwa usimamizi bora. Mfano wake ni kama yule ngamia jike ayabebaye mahitaji yote na

humpeleka mpandaji wake kwa mahabubu, aliyebebeshwa kila aina ya masurufu, nafaka, nguo na mavazi. Au mfano wake ni kama bwawa dogo lenye maji mengi sana kana kwamba ni mahali zinapokutana bahari au ni mahali ipitapo bahari iliyofurika. Naona kwamba manufaa na sifa za Sura hii tukufu ni nyingi sana zisizohesabika na binadamu hana uwezo wa kuzihesabu zote hata kama atimize umri wake wote katika matakwa haya.

Wapotevu na wenye bahati mbaya hawakuithamini (sura hii) ipasavyo kwa sababu ya ujahili na uzito wa akili. Wakaisoma lakini hawakutambua uzuri wake juu ya kuisoma mara kwa mara. Sura hii yawashambulia vikali makafiri, yaziathiri haraka nyoyo njema. Na yeyote atakayeizingatia kama mtafiti na kuitalii kwa fikira ing'aayo kama taa iwakayo, basi ataikuta kuwa nuru ya macho na ufunguo wa siri. Na bila shaka hii ndiyo haki sio kubahatisha. Na ikiwa una shaka basi inuka ukajaribu na achana na uvivu na uzembe, wala usiulize maswali yasiyo na maana. Na miongoni mwa maajabu ya Sura hii ni kwamba imetoa maarifa ya Mungu kiasi hiki kwamba mtu yeyote hawezi kuongeza juu yake. Basi twamwomba Mungu kwamba Yeye Aamue baina yetu sisi na kaumu yetu kwa njia ya Al-Faatiha, nasi twamtegemea Yeye. Amin ya Rabbal 'Aalamiin.

MLANGO WA PILI

Maelezo ya maneno yanayosomwa kabla ya usomaji wa Sura Al-Faatiha na Kurani Tukufu أَعُوذُ بِاللهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ

Ee mtafuta maarifa, ujue kwamba anayetaka kusoma Sura Al-Faatiha na Kurani Tukufu analazimika, jinsi ilivyomo katika Kurani, kujikinga kwa Mwenyezi Amlinde na shetani afukuzwaye. Kwani shetani huingia malishoni mwa Mungu kama wezi na kuingilia patakatifu pawalindapo maasumu. Hivyo, Mwenyezi Mungu Akataka kuwaokoa waja wake katika shambulio la shetani aendaye kisirisiri kwa hila pindi wasomapo Sura Al-Faatiha na Neno la Mola wa watu na kumfukuza kwa silaha yake na kumpiga shoka la kichwani na kuwazindua walioghafilika katika kusinzia. Basi Akafundisha maneno ya kumfukuzilia mbali shetani afukuzwaye mpaka siku ya kiama. Na siri ya jambo hili lililofichika ni hii kwamba shetani ndiye adui ya mtu tangu dahari na hutaka kumwangamiza kwa mbinu za siri; na kumwangamiza mtu ndiyo shughuli aipendayo zaidi. Kwa lengo hili amejilazimisha kutega masikio kwa kila amri inayoshuka kutoka kwa Rahmani kwa kuwaita watu kwenye Pepo, na kujibidiisha kuwapoteza watu kwa fitina. Basi Mungu Alimpangia ushinde na kuhuzunika kwa njia ya kuwainua manabii. Hakumwua bali Akampa muhula mpaka siku wafu watakapofufuliwa kwa idhini ya Mungu Mwenye heshima na utukufu. Akatoa habari ya kuuliwa kwake

katika kauli الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ (shetani arujumiwaye) na haya ni maneno yanayosomwa kabla ya kauli yake: بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ Na rajimi ndiye yule aliyetolewa onyo, yaani dajali ambaye Masihi mwangamizi atamwua. Na رَجْم maana yake ni kuua kama ilivyobainishwa katika vitabu vya lugha ya Kiarabu. Basi rajimi ni dajali atakayeuawa katika zama fulani zijazo. Hii ni ahadi ya Mungu Anayesimamia waja wake mambo yao, na hakuna mabadiliko katika maneno ya Mungu. Hii ni bishara kwa Waislamu kutoka kwa Mungu Mwingi wa ukarimu na ni ishara kwamba Atamwua dajali wakati fulani kama limaanishavyo neno الرَّجِيْم.

BETI

Maana ya اَلرَّجْم sehemu hii jinsi nilivyofundishwa na Mola wa viumbe –

Ni kuvunja moyo, yaani kuwavunja moyo watu dhalili na kuwanyamazisha maadui ambao ndio pango la giza.

Na ni pigo liukatalo mzizi wa ugomvi, wala hatumaanishi pigo la upanga.

Unaona kwamba Islam imevunjwa kama mifupa, na wapo wengi wasiojulikana ambao wamewazidi waadhamu.

Basi, wakati uliziita siku za Imamu, ili Waislamu waokolewe na mishale.

Hivyo, usifanye haraka bali utafakari maneno haya, je, wakati huu sio wakati wa kulipiza kisasi.

Laja jeshi la malaika watakatifu wanaoongozwa na Mtume[saw] Mteule.

Sasa zimewadia zama utakapotilifika ulaghai wote na hautabaki uongo wala giza na dini zote zitaangamia isipokuwa Islam, na ardhi itajaa uadilifu, insafu na nuru kama hapo kabla ilivyokuwa imejaa dhuluma, kufuru, uonevu na uongo. Hapo ndipo litakapouawa kundi la dajali sawa na ahadi iliyotangulia kuliangamiza. Na maana ya kuuawa ni kuvunja nguvu yake na kuachisha uhuru wafungwa wake. Basi kimuhtasari, aliyeitwa اَلشَّيۡطٰنِ الرَّجِيۡمِ ndiye dajali mlaumiwa na mdanganyifu wa zamani aendaye kisirisiri, na kuuawa kwake kulikuwa ni jambo na kusudio lililoahidiwa. Kwa hiyo, Mungu Aliwalazimishia Waislamu wote usomaji wa neno "الرَّجِيۡم" (yaani ***audhubillahi minash-Shaitanir-Rajiim***) kabla ya kusoma Sura Al-Faatiha na kabla ya ***bismillahi***, ili msomaji azingatie kwamba wakati wa dajali hautazipita zama za kaumu ile waliotajwa katika aya ya mwisho ya aya hizi saba. Na tangu mwanzo takdiri hii ya Mungu ilikwishaandikwa kwamba rajimi (dajali) atauawa katika zama za mwisho na watu wataokoka katika kuumwa na chatu huyu. Basi leo zama zimefikia mwisho wa duara lake na umri wa dunia pia umefikia elfu ya saba sawa na

hesabu ya jua na mwezi kama vile Sura Al-Faatiha yenye aya saba. Leo huyo shetani rajiim amedhihiri katika umbo lililo kama badala ya mavazi yake; na upotevu umeishia kwa kaumu ile iliyotajwa katika neno la mwisho la sura Al-Faatiha. Mwenye busara tu aweza kuelewa dokezo hili. Dajali atauawa kwa silaha ya kimbingu tu yaani kwa fadhili ya Mungu sio kwa nguvu ya kibinadamu. Basi haitakuwa vita wala mapambano bali jambo hili ndilo litakaloshuka kutoka kwa Mungu Mmoja. Dajali huyu aliendelea kutuma baadhi ya dhuria yake katika kila karne ili kuwapoteza waaminio, wafuasi wa Mungu Mmoja, watu wema, walioimarika katika haki na watafutao ukweli, ili kubomoa misingi ya dini na kuvifanya vitabu vya Mungu kuwa mkusanyiko wa uongo. Hii ilikuwa ahadi ya Mungu kwamba dajali atauawa katika zama za mwisho. Hasanati itaushinda ufisadi na uasi. Ardhi itabadilishwa na watu wengi wataelekea kwa Mungu Rahmani na ardhi itang'aa kwa nuru ya Mola wake na mioyo itatoka katika giza la shetani.

Basi, hayo ndiyo mauti ya uongo na kifo cha dajali na uuaji wa chatu huyu. Je, watu wanasema kwamba dajali ni mtu mmoja atakayeuawa wakati fulani? La, hasha; bali baba ya maovu yote ni shetani rajimi, atakayerujumiwa katika zama za mwisho kwa kuondolewa ujinga na kung'olewa mbali maovu. Hii ni ahadi ya kweli kutoka

kwa Mungu Rahimu kama ilivyodokezwa katika kauli yake ٱلشَّيۡطَٰنِ ٱلرَّجِيۡمِ (shetani rajimi). Katika zama zetu hizi maneno ya Mola wetu yametimia kwa ukweli na uadilifu. Mungu Akaiangalia Islam kwa rehema baada ya kuangukiwa na balaa na misiba. Basi, Mungu Akamteremsha Masihi wake kwa kumwua dajali aendaye kisirisiri na kumaliza ugomvi. Na shetani aliitwa rajimi sawa na mtindo wa habari za ghaibu kwani bila shaka maana ya ٱلرَّجۡمُ ni kuua. Na kwa kuwa uamuzi wa kuuliwa kwa huyu dajali wakati wa ushukaji wa Masihi wa Mungu Jalali uliishatolewa tayari, kwa hiyo Mungu Alitangulia kuhabarisha kabla ya tukio hili kwa kutuliza na kubashiria kaumu walioziogopa siku za upoevu.

MLANGO WA TATU

Kuhusu Maelezo ya aya

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwingi wa ukarimu.

Mwenyezi Mungu Akujaalie elimu ya majina Yake na kukuongoza kwenye njia za ridhaa yake. Ujue kwamba neno اِسْمٌ limetokana na وَسْمٌ ambalo katika lugha ya Kiarabu lamaanisha kutia alama kwa chuma chenye moto. Ikisemwa اِتَّسَمَ الرَّجُلُ , inamaanisha kwamba mtu huyo amejichagulia alama fulani anayojulikana kwayo na kutambulika baina ya watu. Na sawa na wanalugha kutokana na neno hili hili (وَسْمٌ) kuna سِمَةُ البَعِيْرِ na وِسَامُ البَعِيْرِ yamaanishayo kumtilia ngamia alama fulani kwa chuma chenye moto ili isaidie kumtambua. Na kutokana na hilo hilo inasemwa اِنِّيْ تَوَسَّمْتُ فِيْهِ الْخَيْرَ وَمَا رَاَيْتُ الضَّيْرَ yaani nilitafakari na sikuona alama ya shari usoni mwake wala athari yoyote ya uovu katika maisha yake. Na kutokana na neno hilo hilo kuna وَسْمِيٌّ yaani mvua ya kwanza ya majira ya kuchipua kwani kwa kunyesha kwa nguvu huacha alama za mtiririko wake ardhini kama chechemi. Kadhalika yasemwa اَرْضٌ مَوْسُوْمَةٌ kwa ardhi inapopigwa na mvua ya kwanza ya majira ya kuchipua kwa wakati wake na kuituliza kwa wingi wake mioyo ya wakulima. Na kutokana na neno hilo kuna مَوْسِمُ الْحَجِّ majira ya Haj, مَوْسِمُ السُّوْقِ majira ya soko na مَوَاسِمُ الاِجْتِمَاعِ majira ya mikutano, kwani

hizo ni sehemu maalumu ambapo watu hujumuika kwa lengo hili au lingine. Na kutokana na hilo kuna مِيْسَم ambalo hutumika kwa uzuri na urembo na mara nyingi hutumika kuwahusu wanawake wazuri. Jambo hili lathibitika kwa kutalii vitabu vya Kiarabu na diwani zake kwamba walikuwa wanatumia neno hili sana kwa mambo ya heri ya dunia na dini yao. Na unajua kwamba kwa watu wa kawaida اِسْمُ الشَّيئِ ni jina la kitu ambalo kwalo hutambulika kitu kile. Lakini kwa watu muhtasi na wenye maarifa jina ni kivuli tu cha uhakika wa kitu chenyewe. Bali, hakuna shaka kwamba majina yanayonasibiwa na Mungu kwa vitu ndiyo mahali pa sifa mahususi za vitu hivyo. Majina hayo kwa ajili ya 'ndege' za maana na elimu zenye hekima ni kama viota. Kadhalika katika aya hii tukufu kuna jina Allah, Rahman na Rahim. Basi, kila moja katika hayo huashiria kwenye sifa zake na hali zake zilizofichika. Allah ni jina la dhati yake aliyejikusanyia sifa zote kamilifu, na Rahman na Rahim hueleza kwamba sifa hizi mbili zinahakiki kwa jina lile lijikusanyialo kila aina ya ujamali na ujalali. Kisha اَلرَّحْمٰن lina maana maalumu isiyopatikana katika اَلرَّحِيْم , nayo ndiyo kwamba kwa idhini ya Mungu Karima sifa hii ya Rahmani huendelea kuwabariki wanadamu na wanyama wengine sawa na hekima yake tangu kale kulingana na vipawa vyao sio kwa usawa kwa kila moja. Sifa hii ya Urahmani haiingiliwi na matendo, amali na bidii ya nguvu yoyote ya mtu au

mnyama. Bali hii ndiyo hisani maalumu ya Mungu ambayo tendo la mtendaji halikuitangulia. Hii ndiyo rehema yake kwa wote, siyo natija ya juhudi ya mtu mpungufu au mkamilifu yeyote. Kwa neno zima, baraka ya sifa ya Urahmani siyo matokeo ya amali yoyote au tunda la haki fulani, bali hii ndiyo fadhili tu ya Mungu pasipo utii au ukaidi, na baraka hii hushuka daima sawa na matakwa na utashi wa Mungu bila sharti la utii, ibada, takwa na kujitolea. Na msingi wa baraka hii upo hata kabla ya uwepo wa viumbe na vitendo vyao na juhudi na ombi lao. Ndiyo sababu alama za baraka hii zinapatikana hata kabla ya uwepo wa watu na wanyama, ingawaje baraka hizi zinaendelea katika hatua zote za uwepo wa viumbe, wakati, mahali, utii na uasi. Je, huoni kwamba Urahmani wa Mwenyezi Mungu umeenea kwa wote, wema na wadhalimu. Unaona mwezi wake na jua lake huwaangazia wote, watiifu na waasi. Naye Akampa kila kitu umbo lake na kusimamia mambo yao yote. Hakuna mnyama yeyote isipokuwa riziki yake iko juu ya Mungu hata kama yupo mbinguni au ardhini. Yeye ndiye Aliumba kwao miti na kutoka humo akatoa matunda, maua na harufu nzuri. Hii ni rehema Mungu Aliyowaandalia watu hata kabla ya kuumbwa kwao, na humo imo nasaha kwa wamchao Mungu. Na neema hizi zimetolewa na Mungu, Mwingi wa rehema, Mwumbaji Mkuu bila amali na bila haki yoyote. Kuna neema zingine

nyingi za Mungu zisizohesabika, mathalan kuziumba sababu ziletazo afya, tadbiri zote na dawa ya kila maradhi na kuwainua mitume na kuwateremshia manabii vitabu. Hayo yote ni Urahmani wa Mola wetu Aliye Mrehemevu kuliko warehemevu wote, na ni fadhili mahususi isiyosababishwa na kitendo cha mtendaji wala maombi wala dua yoyote.

Ama Urahimu, basi hii ndiyo baraka mahususi kuliko baraka za sifa ya Urahmani na huhusikana na ukamilifu wa kibinadamu na kukamilisha tabia ya asili ya mtu, lakini kwa sharti la kufanya juhudi, kutenda matendo mazuri na kuachana na tamaa za nafsi. Bali rehema hii hushuka kikamilifu baada ya kufanya juhudi barabara katika vitendo, kujitakasa nafsi na kufikisha ikhlasi mpaka ukamilifu wake kwa kuondoa athari za unafiki, kwa kutakasa moyo na kukubali mauti kwa kutaka radhi ya Mungu Jalali. Basi ni mwenye bahati njema yule aliyepata hadhi katika neema hizi, bali yeye ndiye mtu na wengine wote ni kama wanyama tu. Hapa pana swali gumu tunaloliandika katika kitabu hiki pamoja na jibu lake ili mwenye akili alizingatie, nalo ni kwamba kwa nini Mungu Amezichagua sifa mbili tu, Rahmani na Rahimu, katika *Bismillahi* kati ya sifa zake zote na hakutaja sifa nyingine katika aya hii ilihali jina lake adhimu linastahiki sifa zote zilizokamilika kama ilivyotajwa katika Kurani Tukufu.

Tena kutaja sifa nyingi wakati wa usomaji wa Kurani hulazimu kuleta baraka nyingi. Basi aya بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ inayo haki zaidi ya kupata daraja na heshima hii. Na imesisitizwa kuisoma wakati wa kuanza kufanya kila jambo la muhimu kama ilivyokuja katika Hadithi za Mtume[saw], nayo hukaririwa sana na midomo ya Waislamu. Na aya hii imerudiwa mara nyingi zaidi katika Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Basi, kwa hekima na masilahi gani sifa zingine hazikuandikwa pamoja na aya hii tukufu? Jibu lake ni hili kwamba hapa Mwenyezi Mungu alitaka kutaja pamoja na jina lake adhimu kabisa sifa zile mbili ambazo ni muhtasari kikamilifu wa sifa zake zote adhimu. Na sifa hizo mbili ni Rahmani na Rahimu kama akili timamu pia huongoza kwenye jambo hili. Kwani, Mwenyezi Mungu hujidhihirisha katika dunia hii mara kwa shani ya Mpendwa na mara nyingine kwa sura ya Mpenzi. Na Amezifanya sifa hizi mbili kuwa mwanga ushukao kutoka kwa jua la 'Umola' kwenye ardhi ya 'utumishi'. Hivyo, pengine Mola Anakuwa Mahabubu, na mtumishi anakuwa mpenzi wake; na wakati mwingine mtumishi anakuwa mahabubu na Mola Awa Mpenzi wake na Anamfanya kama matilaba yake. Na bila shaka asili ya mtu iliyojaaliwa upendo, urafiki na uchungu wa moyo, hutaka sana kuwa na mpendwa yeyote ambaye aivute kwake kwa kudhihirisha ujamali, neema na hisani yake; na pia iwe na mpenzi mwenye

kuifariji ambaye aje kuiondolea mbali hatari na hali za mahangaiko na aihifadhi katika upotevu wa amali na kuifikishia matakwa yake. Basi Mwenyezi Mungu Alinuia kuipa tabia ya asili kile inachohitaji na kuitimizia neema zake kwa ukarimu wake mwingi. Hivyo, Akajidhihirisha kwake kwa sifa zake mbili, Rahmani na Rahimu.[6] Hakuna shaka kwamba sifa hizi mbili ni njia ya mwunganisho baina ya Umola na Utumishi na kwa hizi mbili duara la juhudi za kumkaribia Mungu na maarifa ya kibinadamu hukamilika. Hivyo, sifa zote zilizosalia zaingia ndani ya nuru za hizi mbili na ni tone la bahari zao. Kadhalika kama vile Mwenyezi Mungu Anavyotaka kwa dhati yake kuwa Mahabubu na pia Mpenzi, ndivyo hivyo Awatakiavyo watumishi wake wakamilifu wawe kwa wanadmu wenzao mithili ya dhati yake kihulka na kisera

[6] Bila shaka unajua kwamba Mungu, kwa sifa yake Rahmani, Huwashushia mtu, mnyama, kafiri na mumini hisani na fadhili za aina aina bila wao kufanya amali yoyote yenye kuwastahikisha mbele ya Mungu Dayani kupewa hizo. Hakuna shaka kwamba kufanya ihsani kwa njia hii kunamfanya mara moja mhisani kuwa mahabubu, hivyo imethibitika kwamba kumfadhili kwa njia ya Urahmani kunadhihirisha shani Yake ya kuwa mahabubu machoni pa waliofadhiliwa. Na ama sifa ya Urahimu, hii imejilazimishia shani ya kuwa Mpenzi. Basi, Mwenyezi Mungu Hamdhihirikii yeyote kati ya waaminio kwa ukarimu huu isipokuwa wakati Ampendapo na kumridhia kikauli na kiamali. Mwandishi

na wazifanye sifa hizi mbili kwa ajili yao kama libasi na mavazi ili utumishi ujichukulie khulka za Umola na isibaki kasoro yoyote katika ukuaji wa kibinadmu. Ndiyo maana Aliwaumba manabii na mitume, na Akawafanya baadhi yao dhihirisho la sifa yake Rahmani na baadhi wengine dhihirisho la sifa yake Rahimu ili nao wawe mahabubu na wapenzi na kuishi kwa kupendana kwa fadhili Yake adhimu. Basi Akawapa baadhi yao hadhi kubwa katika sifa ya kupendwa na wengineo sehemu kubwa katika sifa ya kupenda na hivyo ndivyo Akataka kwa fadhili Yake nyingi na ukarimu Wake wa kudumu. Na zilipofika zama za Khatamun Nabiyyin, Seyidi wetu Muhammad[saw], Seyidi wa mitume wote, Allah Subhanahu Akataka Ajumuishe sifa hizi mbili katika nafsi moja. Basi Akazijumuisha hizi mbili katika dhati yake, malaki ya rehema na baraka ziwe kwake. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu kataja hususan sifa za kuwa mahabubu na kuwa mpenzi mwanzoni mwa sura hii ili kuashiria kwenye matakwa haya. Na Akamwita nabii wetu jina Muhamad na Ahmad kama vile Alivyojiita Rahmani na Rahimu katika aya hii. Basi hii ni ishara kwenye jambo hili kwamba hakuna mkusanyaji wa sifa hizi mbili kwa njia ya kivuli isipokuwa dhati ya Seyidi wetu, Mbora[saw] wa viumbe. Na umeshajua kwamba sifa hizi mbili ni sifa kuu kati ya sifa za Mungu Mmoja, bali hizo mbili ni kiini halisi na hakika hasa ya majina Yake yote ya kisifa. Na

hizo mbili ni kigezo cha ukamilifu wa kila anayetaka kukamilika na kushika khulka za Mungu. Na mtu yeyote hakupewa sehemu kamili katika sifa hizi mbili isipokuwa Nabii wetu[saw] aliye Khatam wa silsila ya unabii. Hii ndiyo sababu kwamba alipewa majina mawili kwa fadhili ya Mola wa dunia na Akhera kama sifa hizi mbili; la kwanza ni Muhammad na la pili Ahmad. Ama Muhammad, basi hili limejivalia shuka la sifa ya Rahmani na limedhihirika katika mavazi ya ujalali na Umahabubu na amesifiwa kwa wema wake na ihsani yake. Na ama jina la Ahmad, basi hili limedhihirika katika mavazi ya Urahimu na Upendo na ujamali kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu Awalindaye waaminio kwa auni na nusura. Hivyo, majina haya mawili (Muhammad na Ahmad) ya Nabii[saw] wetu yakawa kwa mkabala wa sifa mbili (Rahman na Rahim) za Mola wetu Manani, yaliyo kama sura zinazoakisiwa vinazodhihirisha vioo viwili vinavyokabiliana. Maelezo yake ni haya kwamba kwa wenye maarifa, hakika ya Urahmani ni kwamba huu humfikishia kila mwenye roho, binadamu au asiye binadamu, heri tele bila amali yoyote iliyotangulia kwa ihsani halisi. Hakuna shaka wala hitilafu katika jambo hili kwamba ihsani halisi ya namna hii ambayo siyo malipo ya kitendo cha mtendaji yeyote kati ya viumbe, huvutia mioyo ya waaminio kwenye kutukuza, kusifu na kuhimidi. Basi wanamhimidi na kumtukuza Mhisani wao kwa ikhlasi ya mioyo na nia safi. Hivyo basi

Rahmani anakuwa Muhammad bila wasiwasi wowote unaosababisha kushuku. Kwani, mwenye kuwaneemesha watu kwa neema za aina nyingi anayewafanyia hisani bila haki yoyote, basi kila mmoja aneemeshwaye anamhimidi. Na hii ndiyo sifa ya maumbile ya kibinadamu. Kisha sawa na neema kukamilika, hamdu inapokamilika, basi huuvutia upendo kamili. Hapo mhisani kama huyo anakuwa Muhammad na mahabubu machoni pa wampendao. Basi, hayo ni matokeo ya sifa ya Urahmani. Kwa hiyo, utafakari kama wenye akili. Hapa imembainikia kila mwenye maarifa kwamba Rahmani ni Muhammad, na Muhammad ni Rahmani. Na hakuna shaka kwamba natija ya majina yote mawili ni moja tu. Basi aliyekataa hakutambua haki.

Ama hakika ya sifa ya Urahimu na iliyofichika humo hali ya kiroho, basi hii ni baraka ya neema na heri juu ya amali ya Waislamu, sio watu wengine; na ni kukamilisha amali ya watendao wenye ikhlasi, na ni kurekebisha kilichoharibika kama wanavyofanya wasaidizi na wafidiao kilichopunguka. Baraka hii ni kama Mungu Rahimu kutoa sifa, kwani Hamteremshii rehema yake hii mtendaji yeyote ila baada ya kumsifu kwa njia yake imara na kumridhia kwa amali yake na kumwona kwamba anastahiki kupata fadhili nyingi. Je, huoni kwamba Hakubali amali ya makafiri, washirikina, wanafiki na

wenye kiburi, bali Huzifanya amali zao zipotee bure wala Hawaongozi kwake wala Hawasaidii, bali Huwaacha kama watu walioachwa pasipo kusaidiwa. Hakuna shaka kwamba Hamwelekei yeyote kwa sifa yake ya Urahimu wala Hamtimizii amali yake kwa nusura na auni isipokuwa baada ya kuziridhia amali zake na kumhimidia kwa hamdu inayoulazimu ushukaji wa rehema. Kisha kwa ukamiifu wa amali za wenye ikhlasi, hamdu kutoka kwa Mungu inapofikia ukamilifu, hapo Mungu Anakuwa Ahmad, na mtumishi anakuwa Muhammad. Basi Ametukuka Mungu Aliye Muhammad wa kwanza na Ahmad wa kwanza. Wakati huo mtumishi mwenye ikhlasi katika amali anakuwa mahabubu kwa Mungu, kwani Mungu Humsifu kutoka arshi yake, na Mungu Humhimidi mtu baada ya kumpenda. Basi, kwa kifupi, ukamilifu wa Urahmani unamfanya Mungu kuwa Muhammad na Mahabubu na kumfanya mtumishi kuwa Ahmad na mpenzi anayemtafuta mahabubu. Na ukamilifu wa Urahimu unamfanya Mungu kuwa Ahmad na mpenzi anayemtafuta mahabubu. Na ukamilifu wa Urahimu unamfanya Mungu kuwa Ahmad na Mpenzi na kumfanya mtumishi kuwa Muhammad na mahabubu. Na hapo utajua shani ya Nabii[saw] wetu aliye Imamu mkarimu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amemwita Muhammad na Ahmad; Hakuwawita Isa na Musa majina haya mawili. Akamshirikisha katika sifa zake mbili, Rahmani na

Rahimu, kwa sababu fadhili Yake adhimu ipo juu yake. Na Akataja sifa hizi mbili katika ***Bismillahi*** ili watu wote wajue kwamba sifa hizi mbili ni kama Isimu Kuu kwa Mungu, na kwa Nabii Mtukufu[saw] ni kama joho la heshima kutoka kwa Mungu. Mwenyezi Mungu Akamwita Mtume[saw] jina Muhammad kwa kuashiria kwenye sifa yake ya kuwa mahabubu, na kamwita jina Ahmad kuashiria kwenye sifa yake ya kuwa mpenzi. Ama jina Muhammad, basi ni kwa sababu wasifu hawawezi kumsifu sana mno mtu yeyote mpaka mtu huyo awe mahabubu. Na Ahmad, kwani msifu hawezi kumsifu sana mtu isipokuwa akimpenda sana na kumfanya kuwa mpendwa wake. Basi hakuna shaka kwamba katika jina Muhammad lazima imo maana ya Umahabubu. Na kadhalika katika jina Ahmad imo maana ya Upendo kutoka kwa Mungu Mwenye fadhili na neema. Na hakuna shaka kwamba Nabii[saw] wetu aliitwa Muhammad, kwani Mungu Alitaka kumfanye mpendwa machoni Pake na machoni pa watu wema. Na vilevile Alimwita jina Ahmad, kwani Mungu Subhanahu Alikusudia kumfanya mpenda wake na mpenda wa waumini Waislamu. Basi Yu Muhammad kwa shani moja, na Ahmad kwa shani nyingine. Jina moja kati ya haya mawili Akaliweka mahususi kwa zama moja na lingine kwa zama nyingine.

Mungu Mtukufu Ameashiria kwenye habari hii katika kauli yake دَنَا فَتَدَلّٰى[7] na قَابَ قَوْسَيْنِ اَوْ اَدْنٰى[8]. Kisha ilipoweza kudhaniwa kwamba kumwekea mahususi Nabii huyu, atiiwaye na watu na Mwenye ibada sana, sifa hizi za Mola wa watu kunaweza kuwaelekeza kwenye shiriki kama vile kwa itikadi ya namna hii Isa[as] akafanywa Mungu, basi Mwenyezi Mungu Akataka kuufanya umati huu uliorehemiwa kurithi majina haya mawili kwa njia ya kivuli ili yawe kama baraka za kuendelea kwa umati, na ili kwa kuondoa shaka ya ushirikiano wa mtu maalumu katika sifa za Mwenyezi Mungu, basi Akawafanya masahaba[ra] na wawafuatao kuwa dhihirisho la sifa ya Muhammad kwa shani ya Urahmani na ujalali. Akawapa ushindi na kuwasaidia kwa fadhila za kufululiza. Na Akamfanya Masihi Mau‘udi dhihirisho la jina Ahmad na kamtuma kwa shani za Urahimu na ujamali. Na Akatia rehema na upole moyoni mwake na kamjaalia hulka bora tukufu. Huyu ndiye Mahdi wa ahadi ambaye kumhusu yeye wanabishana ilhali wameona ishara zilizo wazi lakini hata hivyo hawaongoki, bali huing'ang'ania batili na hawarejei kwa haki. Huyu ndiye Masihi Mau‘udi, lakini hawatambui. Wanamwona lakini hawana busara. Bila shaka jina Isa na jina Ahmad yapo namna moja katika

---

[7] Akakaribia na akateremka.

[8] Umbali wa pinde mbili au karibu zaidi.

kufanana na huafikiana kitabia na kwa hali hudhihirisha ujamali na kuacha kitali. Na jina la Muhammad ni jina la nguvu na la ujalali na hayo yote mawili ni kama vivuli vya Rahmani na Rahimu. Je, huoni kwamba jina Rahmani ambalo ni chanzo cha hakika ya Umuhammad hutaka ujalali kama vile hutaka shani ya umahabubu. Na huu ni Urahamani wa Mwenyezi Mungu kwamba Amemtiisha kila mnyama kumhudumia binadamu, kama vile ngombe, mbuzi, ngamia, nyumbu na kondoo. Na amemwaga damu nyingi kwa kulinda mwanadamu mwenyewe. Na hili ndilo jambo la ujalali na natija ya Urahmani wa Rahmani. Basi imethibitika kwamba Urahmani unataka nguvu na ujalali. Na juu ya hayo, hii ni ihsani ya Mahabubu kwa yule Amtakaye kumpa fadhili. Wako wadudu wengi wa majini na wa hewani wanaohilikishwa kwa ajili ya mtu. Na wako wanyama wengi wanaochinjwa kwa ajili ya wanadamu kama neema kutoka kwa Rahmani. Basi muhtasari wa somo ni huu kwamba masahaba walikuwa madhihirisho ya hakika ya Umuhammadi ya kijalali. Ndiyo sababu waliwaua watu waliokuwa kama wanyama mbuai na wanyama mwitu ili waachiliwe huru watu wengine gerezani mwa dhalala na upotevu na kuwapeleka kwenye wema na mwongozo. Na umeshajua vizuri kwamba hakika ya Umuhammad ni dhihirisho la hakika ya Urahmani. Na hakuna hitilafu baina ya sifa hii ya ihsani na ujalali, bali Urahmani ni

dhihirisho kamili la ujalali na nguvu ya Mwenyezi Mungu. Na hakika ya Urahmani ni hii tu kwamba kilicho duni kitolewe dhabihu kwa kilicho aula. Na hivyo ndivyo iendeleavyo suna ya Rahmani tangu kuumbwa kwa mwanadamu na viumbe vingine. Je, huoni jinsi vijidudu vya majeraha ya ngamia huangamizwa kwa kulinda uhai wa ngamia; ngamia wanachinjwa ili watu wafaidike na nyama zao na ngozi zao, na watengeneze mavazi mazuri na ya kupendeza kutokana na manyoya yao. Na hayo yote ni kutokana na Urahmani kwa kuhifadhi kufululiza uwepo wa binadamu na wanyama. Tena kama vile Rahmani alivyo Mahabubu hivyo ndivyo Yu dhihirisho pia la ujalali. Na jina Muhammad ni mithili yake katika ukamilifu huu. Kisha masahaba walipolirithi jina Muhammad kutoka kwa Mungu Mpaji na wakadhihirisha ujalali wa Mungu na kuwaua wadhalimu kama wanyama, basi kadhalika Masihi Mau‘udi akarithi jina Ahmad ambalo ni dhihirisho la urahimu na ujamali, na Mwenyezi Mungu Alimchagulia jina hili yeye na wafuasi wake na walio kama ali zake. Basi Masihi Mau‘udi kutoka kwa Mwenyezi Mungu yu dhihirisho la sifa Zake za Urahimu na Uahmad kwa ajili ya Jumuiya yake, ili kauli ya Mwenyezi Mungu وَاٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ[9] itimie. Na hakuna awezaye kuyazuia Anayotaka Mola, ili uhakika wa madhihirisho ya

[9] Na Akamtuma kwa wengineo (Al-Jumu‘a, 62:4).

Nabii[saw] utimie. Na hiyo ndiyo sababu mahususi ya kueleza sifa za Urahmani na Urahimu pamoja na *Bismillahi* ili ziashirie kwenye majina mawili ya Muhammad na Ahmad na wale wajao walio madhihirisho yao, yaani masahaba na Masihi wa Mungu aliyekuwa aje katika mavazi ya Urahimu na Uahmad.

Twarudia tena muhtasari wa maelezo ya بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ . Basi ujue kwamba jina Allah ni اسم جامد (nomino tuli). Mtu yeyote hajui maana yake halisi isipokuwa Mwenyezi Mungu, Mwenye habari na Alimu. Mungu Mwenye enzi Amehabarisha hakika ya jina hili katika aya hii, na Akaashiria kwamba Dhati yake inazo sifa za Urahmani na Urahimu, yaani ina sifa ya rehema iliyo ihsani na rehema iliyoambatana na hali ya imani ya mtu. Na rehema hizi mbili ni kama maji safi na chakula kitamu zitokazo katika chemchemi ya Umola. Sifa zingine zote minghairi ya hizi mbili ni matawi ya sifa hizi. Asili yenyewe ni Urahmani na Urahimu tu, na hizi mbili ni dhihirisho la siri ya Dhati ya Mungu. Na Nabii wetu aliye Imamu wa njia iliyonyoka akapewa hadhi kamili katika sifa hizi mbili. Basi akalifanya jina lake Muhammad kuwa kivuli cha Rahmani na jina lake Ahmad kivuli cha Rahimu. Na siri iliyomo ndani yake ni hii kwamba mtu mkamilifu hawezi kuwa mkamilifu bila kushika hulka za Mungu na sifa za Rabi. Na waelewa kwamba sifa zote ni natija ya rehema hizi

mbili tulizoziita Urahmani na Urahimu. Na wajua kwamba Urahmani ni rehema bila sharti lolote kwa njia ya ihsani na baraka yake inamfikia kila mumini na kafiri bali kila mwenye uhai. Ama Urahimu, basi huu ndio rehema mahasusi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji inayowahusu waaminio pasipo wenye uhai wengine na makafiri. Basi imelazimika kwamba mtu kamili yaani Muhammad[saw] ndiye dhihirisho la sifa hizi mbili. Na ndiyo sababu akaitwa na Mola wa dunia na Akhera jina Muhammad na Ahmad, na Mwenyezi Mungu Akasema kumhusu yeye:

لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُوْلٌ مِّنْ اَنْفُسِكُمْ عَزِيْزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيْصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِيْنَ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ[10]

Basi Mwenyezi Mungu Ameashiria katika kauli yake ‘ عَزِيْز ’ na kauli yake ‘ حَرِيْص ’ kwamba Mtume[saw] kwa fadhili Yake adhimu yu dhihirisho la sifa Yake ya Rahmani,[11] kwani yu rehema kwa walimwengu wote yaani kwa wanadamu, wanyama, makafiri na waaminio. Kisha Akisema بِالْمُؤْمِنِيْنَ رَءُوْفٌ رَّحِيْمٌ Amemfanya rahmani na rahimu kama isivyofichika

---

[10] Bila shaka amewafikieni Mtume kutoka miongoni mwenu; yanamhuzunisha yanayowataabisheni, anawahangaikieni, kwa waaminio ni mpole, mrehemevu. (At-Tauba, 9:128)

[11] Mwenyezi Mungu Amesema: وَ مَا اَرْسَلْنٰكَ اِلَّا رَحْمَةً لِّلْعٰلَمِيْنَ (Al-Ambiyaa 21:108). Nasi Hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu. Maana hii inaafikiana na Urahmani tu, kwani Urahimu unauhusu ulimwengu mmoja tu wa waaminio. Mwandishi

kwa kila mwenye ufahamu. Yeye Akamsifu na kumnasibishia hulka adhimu kwa adhama na heshima kama vile ilivvyotajwa katika Kurani Tukufu. Na kama ukiuliza hulka zake adhimu ni zipi, tutasema yu rahmani na rahimu naye ndiye aliyejaaliwa nuru hizi mbili hata wakati Adamu alipokuwa bado baina ya maji na udongo. Naye alikuwa nabii wakati Adamu alikuwa bado hana alama ya dhati yake wala uwepo wake. Mwenyezi Mungu ndiye nuru na Aliamua kuumba nuru, basi Akamwumba Muhammad[saw] ambaye ni kama lulu ya pekee na Akatia majina yake mawili (Muhammad na Ahmad) katika sifa zake mbili (Rahmani na Rahimu). Hivyo, Mtume[saw] akawashinda wote waliomfikia Mungu kwa moyo safi. Majina haya mawili yametameta katika mafundisho ya Kurani Tukufu. Na Nabii[saw] wetu jinsi alivyofanyizwa na nuru ya Musa na nuru ya Isa ndivyo alivyofanyizwa na sifa mbili za Mola wetu Mtukufu. Basi kufanyizwa huku kulitaka kwamba yeye apewe daraja ya pekee. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Alimwita jina Muhammad na Ahmad. Hivyo, akairithi nuru ya ujalali na ya ujamali na kwa nuru hii akawa wa pekee. Na akajaaliwa shani ya mahabubu na moyo wa wapenzi kama vile jambo hili lilivyomo ndani ya sifa mbili za Mola wa walimwengu. Basi yu mbora wa wasifiwa na mbora wa wasifu. Na Mwenyezi Mungu Amemshrikisha katika sifa zake hizi mbili na kampa hadhi kubwa katika rehema zake hizi mbili na

kumnywesha kutoka katika chemchemi zake mbili na kumwumba kwa mikono yake miwili. Basi akawa kama chupa iliyomo mvinyo njema au kama kishubaka kilichomo taa; na mithili ya sifa Zake hizi mbili Akamteremshia Furkani na Akajumuisha humo ujalali na ujamali na kufanya maelezo yake kujijumuishia mambo yote na kuifanya iwe ariki ya Torati na Injili na kioo kwa kuona uso Wake jalili na jamili. Kisha Akaupa umati huu hadhi kubwa kutoka katika bilauri ya huyu karimu na kuwafundisha kutokana na maneno matakatifu ya huyu aliyefundishwa na Alimu. Basi baadhi yao walikunywa katika chemchemi ya jina Mumhammad iliyobubujika kutoka katika sifa ya Urahmani, na wengineo wakajinywea kwa kujaza vitanga vya mikono yao katika chemchemi ya jina Ahmad iliyo na hakika ya Urahimu. Tangu mwanzo hii ilikuwa ni takdiri iliyowekwa na ahadi iliyofanywa kutimia kwa wakati maalumu iliyotajwa na ndimi za manabii kwamba jina Ahmad halitadhihirika kikamilifu ndani ya yeyote katika wairithi isipokuwa Masihi Mau'udi ambaye Mungu Atamleta wakati wa kutokea siku ya malipo na kukusanyika kwa waaminio. Na Mwenyezi Mungu Atawaona Waislamu kama wanyonge na Islam kama mtoto aliyetupwa jangwani. Hivyo, Atawafanyia maajabu kutoka Kwake na Atashuka Mwenyewe kutoka mbinguni. Ndipo Ufalme wake utaimarika ardhini kama vile ulivyopo mbinguni. Batili

zitaangamia bila kukata vichwa. Njia zote zitakatika na mambo yote yatarejea kwa Mmiliki wa miliki zote. Na hii ni ahadi ya kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama ahadi ile iliyotimia katika zama za mwisho za wana wa Israeli alipoinuliwa Isa mwana wa Mariamu baina yao, naye alisambaza dini bila kuwaua waasi wa Mola Jalali. Na ilikuwa katika mpango wa Mungu Mtukufu Alimu kuufanya mwisho wa umati huu kama mwisho wa makhalifa wa Musa[as]. Kwa hiyo, Aliufanya mwisho wa silsila hii usitegemee msaada wa wasaidizi wengine na uwe dhihirisho la hakika ya مٰلِكِ يَوۡمِ الدِّيۡنِ , kama maelezo ya aya hii yatakavyokuja baada ya muda kidogo. Na nyongeza ya somo hili ni hii hii kwamba Nabii[saw] wetu ndiye mbora wa viumbe wote. Kwa kuwa yu Khatamun Nabiyyin, Mtukufu wa watakatifu na Mpendwa wa Mwenyezi Mungu kuliko watu wote, hivyo Allah subhanahu Alitaka Ajumuishe ndani yake sifa Zake mbili adhimu kwa njia ya kivuli, basi Akampa jina Muhammad na Ahmad ili yawe kama vivuli kwa Urahmani na Urahimu. Ndiyo sababu Aliashiria katika kauli yake اِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسۡتَعِيۡنُ kwamba mwababu kamili hupewa sifa za Mola wa walimwengu baada ya kuingia katika waabudu waliojipoteza ndani ya Mungu. Wajua kwamba kila ukamilifu kati ya ukamilifu wa hulka zote za Mungu unakutegemea kuwa kwake Rahmani na Rahimu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu Alizitaja sifa hizi mbili

mahususi katika *Bismillahi*. Na umejua kwamba jina Muhammad na Ahmad ndiyo mibadala ya Rahmani na Rahimu, na Mungu Alimu na Mwenye hekima Ameyapatia majina haya mawili kila ukamilifu uliofichika katika sifa hizi mbili. Basi hakuna shaka kwamba Mwenyezi Mungu Ameyafanya majina haya mawili kuwa vivuli vya sifa Zake mbili na madhihirisho ya hali Zake mbili ili Auonyeshe uhakika wa Urahmani na Urahimu katika kioo cha Umuhammadi na Uahmadi. Tena kwa kuwa wakamilifu wa umati wake ni sehemu zake za kiroho na ni kama viungo kwa uhakika wa unabii, basi Mwenyezi Mungu Akanuia kwa kudumisha athari za Nabii[saw] huyu maasumu kwamba Awarithishie majina haya mawili kama vile Alivyowafanya kuwa warithi wa elimu zake. Hivyo Akawaingiza masahaba chini ya kivuli cha jina la Muhammad ambalo ni dhihirisho la ujalali na Akamweka Masihi Mau'udi chini ya kivuli cha jina Ahmad lililo dhihirisho la ujamali. Hao wote hawakupata ubora huu ila kikivuli. Hivyo, kwa hakika hamna mshiriki yeyote hapa. Kwa kutenga majina haya mawili, makusudio ya Mwenyezi Mungu yalikuwa kukasimu umati na kuwafanya makundi mawili. Basi Akalifanya kundi moja kati yao dhihirisho la ujalali mithili ya Musa[as], nao ndio masahaba wa Nabii[saw] waliojitokeza kwa kitali. Na Akalifanya kundi lingine dhihirisho la ujamali mithili ya Isa[as], na kuwafanya wapole wa moyo na kutia amani

vifuani mwao na kuwadumisha juu ya tabia njema; na kundi hili ni Masihi Mau‘udi na wafuasi wake, wanawake kwa wanaume. Basi hivyo yakatimia aliyoyasema Musa[as] na yaliyonenwa na Isa[as], na ikatimia ahadi ya Mola Mweza. Bila shaka Musa[as] alitoa habari kuwahusu masahaba waliokuwa dhihirisho la jina Muhammad[saw] Nabii wetu Mteule na maonyesho ya ujalali wa Mungu Mwenye nguvu sawa na kauli Yake اَشِدَّآءُ عَلَى الْكُفَّارِ[12] . Na Isa[as] alitoa habari ya "اٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ" (wengine miongoni mwao) na Imamu wa watawa hao, yaani kumhusu Masihi ambaye ni dhihirisho la Ahmad aliye mrehemevu, msitiri na chanzo cha ujamali wa Mungu Aliye Rahimu na Msamehevu sawa na kauli Yake [13] كَزَرْعٍ اَخْرَجَ شَطْـَٔهٗ yaani yu kama chipuko linalofurahisha wakulima. Na kila mmoja wao alitoa habari ya sifa zilinganazo na sifa zake mwenyewe na kuchagua jumuiya ambao hulka zao zinafanana na hulka zake alizoridhia. Musa[as] aliashiria katika kauli yake اَشِدَّآءُ عَلَى الْكُفَّارِ kwenye masahaba ambao walipata heshima ya kusuhubiana na Nabii wetu Mteule[saw]. Na wakaonyesha uimara na nguvu katika medani na kudhihirisha ujalali wa Mungu kwa upanga mkali na wakawa kivuli cha jina la Muhammad[saw] Mtume wa Mungu Mwenye nguvu. Zimwie rehema za Allah na

---

[12] Ni wenye imara mbele ya makafiri. (Al-Fat'h 48:30)

[13] Kama mmea uliotoa chipuko lake. (Al-Fat'h 48:30)

maombi ya watawa na wateule wa mbinguni na ardhini. Na aliashiria Isa[as] katika kauli yake: [14] كَزَرۡعٍ اَخۡرَجَ شَطۡـَٔهٗ kwenye kundi lingine la watu wengine na Imamu wao Masihi Mau'udi, bali akataja waziwazi jina lake Ahmad na kaashiria ndani ya mfano huu uliopo katika Kurani Tukufu kwamba Masihi Mau'udi atadhihiri kama mmea laini si kama kitu kigumu sana. Tena hii pia ni miongoni mwa maajabu ya Kurani Tukufu kwamba imetaja jina la Ahmad kusimuliwa na Isa[as], na jina la Muhammad

---

[14] Ee mtafuta maarifa, ujue vizuri kwamba haimo kabisa katika Kitabu cha Mungu, Furkani, kwamba masahaba walikuwa warehemevu kwa waasi na maadui. Ama kutendeana wao kwa wao kwa rehema, basi huku hakuwatoi katika eneo la ujalali bali kuwa kwao katika umoja kunaongeza nguvu ya ujalali, kwani mbele ya Mwenyezi Mungu hao ni kama mtu mmoja na kama viungo kwa Mtume Mtukufu[saw]. Mtu yeyote asipate dukuduku moyoni mwake kwamba mfano wa shamba umo katika Torati na Injili zote mbili. Hapana, kwani mfano huu katika Kurani umehusishwa na kitabu cha Isa[as] tu, tena hatuupati katika Torati, bali twaupata kwa kirefu katika Injili. Na inatambulika kwamba karii wakubwa wa Kurani wanafanya wakfu kwenye kauli ya Mungu مَثَلُهُمۡ فِي التَّوۡرٰىةِ , wala hawaiunganishi na mfano huu wakati wa kusoma aya hizi, bali wanauhusisha na Injili kwa yakini bila wasiwasi. Na hii ndiyo sababu kwamba katika misahafu yote inayotumika imeandikwa juu ya neno Taurat **وقف جائز** yaani ***kukifu*** hapa kunajuzu. Na kama bado una shaka, tazama hapo kwa kujiongezea elimu. Mwandishi

kusimuliwa na Musa[as], ili msomaji ajue kwamba nabii mwenye ujalali, yaani Musa[as], alichagua jina liafikianalo na shani yake mwenyewe, yaani Muhammad, ambalo ni jina la kijalali. Na hivyo ndivyo Isa[as] akachagua jina Ahmad ambalo ni jina la ujamali, kwani yeye mwenyewe alikuwa nabii mwenye ujamali ambaye hakupewa nguvu ya dhahiri wala uwezo wa kupigana. Kwa kifupi ni kwamba kila mmoja wao aliashiria kwenye mithili yake kamili. Basi uzingatie jambo hili la kielimu kwani hili litakuondolea wasiwasi na kukubainishia jiha zote mbili za Ujalali na Ujamali na baada ya kuondoa pazia litakuonyesha uhakika wenyewe. Na utakapolikubali hili, utaingia katika ulinzi na uhifadhi wa Mwenyezi Mungu dhidi ya kila dajali na utaokoka katika kila upotevu.

MLANGO WA NNE

Kuhusu maelezo ya

ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ. ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ. مَٰلِكِ يَوۡمِ ٱلدِّينِ.

Ujue kwamba hamdu ndiyo kumsifu mtu kwa kitendo chake kizuri anayestahiki kusifiwa; na مَدَح ni kumsifu yule anayeneemesha kwa kusudi na kufanya hisani kama anavyotaka. Na hamdu huthibitika ipasavyo kwa yule ambaye ni chanzo cha baraka na nuru zote na ambaye hufanya hisani kwa nia sio kwa kutotambua wala kulazimika. Basi, maana hii huthibitika kwa Mungu pekee Aliye Mwenye habari Aonaye, naye ndiye Mhisani na hutokana kwake hisani zote za mwanzo na za mwisho. Na hamdu ya kweli ni Yake tu katika dunia hii na Akhera. Na kila hamdu inayonasibishwa kwa wengine hurejea Kwake Yeye. Na neno 'hamdu' ni kitenzijina kuhusiana na Mwenyezi Mungu kitumikacho kwa kauli tendi na pia kauli ya kutendwa, na kwa mtenda na kwa mtendwa. Na yamaanisha kwamba Mungu ndiye 'Muhammad' na 'Ahmad' kwa ukamilifu. Na karina inayoashiria kwenye muradi huu ni kwamba Mwenyezi Mungu baad ya hamdu Amezitaja sifa zinazoilazimu maana hii sawa na rai ya wenye maarifa. Allah Subhanahu Ameashiria katika neno hamdu kwenye sifa ambazo zipo katika nuru yake ya azali. Kisha Akaeleza neno hamdu na kulieleza kuwa kama yule bi-arusi akaaye nyuma ya pazia ambaye anafunua uso wake wakati wa kutajwa Rahmani na

Rahimu. Kwani, Rahmani huongoza kwenye 'hamdu' kuwa kauli tendi na Rahimu ni kauli ya kutendwa kama vile isivyofichika kwa wataalamu.

Na Allah Subhanahu Ameashiria katika kauli yake رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ kwamba Yu Mwumbaji wa kila kitu, na vinatoka kwake vyote vilivyomo mbinguni na ardhini, na makundi yote yaliyomo ardhini, ya waongofu na wakosefu na wapotevu, huwemo ndani ya walimwengu. Wakati mwingine hali ya upotevu, kufuru, ufasiki na kuacha njia ya katikati yazidi kiasi hiki kwamba ardhi inajaa dhuluma na uonevu. Watu huachana na njia za Mungu Jalali, hawaelewi hakika ya utumishi. wala hawatoi haki ya Umola. Hapo zama zinakuwa kama usiku wenye kiza totoro na dini inakanyagwa chini ya mkasa huu. Kisha Mwenyezi Mungu Huleta ulimwengu mwingine, ndipo ardhi inabadilishwa kuwa ardhi nyingine na hushuka kutoka mbinguni takdiri mpya. Hapo watu hujaaliwa moyo wenye utambuzi na ulimi utoao shukrani ya neema. Ndipo wafanya nafsi zao kuwa kama njia iliyokanyagwa kumwendea Mwenyezi Mungu na wanamwendea kwa hofu na tumaini na macho yainamayo kwa haya na kwa uso uelekeao kwenye kibla kitimizacho mahitaji na kwa hima katika ibada ifikiayo kileleni. Na hali inapofikia upotevu kamili na watu kwa mabadiliko ya hali wanapokuwa kama wanyama mbuai au wanyama wa

kufuga hapo haja ya watawa inazidi. Wakati huo rehema ya Mungu na ihsani yake ya azali yataka kwamba kihulukiwe kitakachotowesha giza na kubomoa majengo yaliyojengwa na mahema yaliyopigwa na iblisi. Ndipo anashuka Imamu kutoka kwa Rahmani ili kufukuzilia mbali majeshi ya shetani. Na daima majeshi haya mawili yanaendelea kupigana – na anayaona yule tu aliyejaaliwa macho mawili – mpaka pingu zinatiwa shingoni mwa batili na yatoweka hoja ionekanayo kama sarabi. Na Imamu yule daima huwashinda maadui, huwasaidia walioongoka, na kunyanyua vibao viashiriavyo kwenye mwongozo na kuhuisha misimu ya takwa, mpaka watu wapate kujua kwamba Imamu huyu ameishawakamata mashetani wa kufuru na kufunga mikono yao nyuma ya migongo yao na kukamata wanyama mbuai wa uongo na kutia pingu shingoni mwao na kuvunja majengo ya bidaa na makuba yao na kajumuisha neno la imani na kupanga sababu zake na kuuimarisha ufalme wa mbinguni na kuhifadhi barabara mipaka yake na kurekebisha hali yake na kuboresha mambo yote na kuituliza mioyo itetemekayo na kufumba midomo ienezayo uongo na kunurisha mioyo yenye giza na kuutilia nguvu utawala uliochakaa. Na hivyo ndivyo Mungu Mweza Hufanya mpaka giza na upotevu kuondoka. Hapo maadui wanarudi kwa visingino vyao na kuvunjilia mbali mahema yao waliyopiga na kufundua mafundo yao waliyoyapiga.

Watu bora wa walimwengu na wapendwa wa mahuluku ndio manabii na mitume na waja wa Mungu walio wema na wakweli. Kwani, hao wanawashinda wengine katika kueneza hulka bora na kuondoa giza na kuboresha hulka na kuwatakia heri watu wao na wengine waishio duniani na kueneza wema na heri, kung'olea mbali ufisadi na shari, kuimarisha mema, kukataza maovu na mwelekeo kwenye matamanio ya nafsi kama wanyama, kuelekeza kwa Mola wa watumishi, kujitenga na mali iliyochumwa sasa au zamani, kudumu kumtii Mwenyezi Mungu kwa nguvu zote na matayarisho kamili, kushambulia dhuria za shetani kwa majeshi yaliyojumuishwa na makundi yaliyokusanywa, na kujitenga na dunia kwa ajili ya mpendwa na kujiweka mbali na mahali pake penye rutuba, na kujitenga na maji yao na malisho yao kama kuhajiri na kujitupa kwa Mwenyezi Mungu. Hao ni watu wasiopata usingizi isipokuwa katika hali ya kumpenda Mungu na kuwaombea watu. Dunia hii machoni pa waipendao ndiyo nzuri na ya kupendeza, lakini machoni pa waja wa Mungu ni chafu zaidi kuliko kinyesi na inanuka vibaya zaidi kuliko mzoga. Wanamkaribia Mwenyezi Mungu kitimilifu na kuelekea Kwake kikamilifu kwa moyo wa kweli na kama vile msingi wa nyumba hutangulizwa juu ya kuba na sebule zilizojengwa. Kadhalika waheshimiwa hao wanatangulizwa katika dunia hii juu ya watawa wa tabaka zote. Na nimeonyeshwa

katika kashfi kwamba mkamilifu zaidi na mbora zaidi na arifu wao zaidi na mjuzi zaidi kuliko wote hao ndiye Nabii wetu Mteule[saw], zimwie baraka, rehema na amani katika ardhi na mbingu zilizo juu. Na wenye bahati mbaya kuliko wote ni wale waliomshambulia wakimtusi na kukosoa bila kujua siri ya ghaibu. Na wengi walioje wanaolaaniwa ardhini lakini huko mbinguni Mungu Anawasifu; na wengi walioje wanaoheshimiwa katika dunia hii lakini watadhalilishwa siku ya malipo! Kisha Allah Subhanahu Ameashiria katika kauli yake رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ kwamba Yu Mwumbaji wa kila kitu naye Huhimidiwa mbinguni na ardhini na kwamba wamhimidiao wanadumu kumhimidi na wamejitolea kumkumbuka. Na kila kitu kinamtukuza na kumhimidi wakati wote. Na mja anapoachana na matamanio yake na kujitenga na mivutano ya nafsi yake na kujipoteza ndani mwa Mungu na njia zake na ibada zake na kumtambua Mola wake ambaye Alimlea kwa fadhili zake na kumhimidi kila wakati na kumpenda kwa moyo wake wote bali kwa chembe zake zote (za mwili wake), hapo yeye anakuwa ulimwengu mmoja miongoni mwa walimwengu. Kwa hiyo Ibrahim[as] ameitwa ‘umati’ katika Kitabu cha Mjuzi wa walimwengu wote. Kisha katika walimwengu kuna zama ambapo Khatamun Nabiyyiin[saw] alitumwa ndani yao. Tena kuna zama nyingine ambapo Mwenyezi Mungu Ataleta watu wengine katika zama za mwisho kama

rehema kwa waitafutao haki. Na Ameashiria kwake katika kauli yake hii [15] لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُوْلَىٰ وَ الْاٰخِرَةِ. Hapa Ameashiria kwenye ma-Ahmad wawili na Amewafanya wote wawili miongoni mwa neema zake zilizokithiri. Wa kwanza wa hawa wawili ni Ahmad Mteule Mtume[saw] wetu Mchaguliwa. Na wa pili ni Ahmad wa zama za mwisho ambaye Mungu Manani Alimwita Masihi na Mahdi. Na nimepata elimu hii kutokana na kauli hii ya Mungu[16] اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ . Basi atafakari aliye miongoni mwa wenye kutafakari. Na unajua kwamba 'walimwengu' humaanisha kila kilichopo – isipokuwa Mungu Mwumbaji wa mahuluku – kiwe cha ulimwengu wa kiroho au cha ulimwengu wa kimwili, kiwe kiumbe cha ardhini au kitu cha angani kama vile jua na mwezi na vinginevyo. Basi, kila kilichomo walimwenguni kimo chini ya ulezi wa Mungu. Kisha rehema ya ulezi ni pana, kamilifu na timiilfu zaidi kuliko kila rehema inayoweza kufikiriwa nyoyoni au kutajwa midomoni. Kisha baada yake kuna rehema kwa wote – na huhusiana na wanyama na wanadamu – nayo ndiyo rehema ya sifa ya Urahmani Aliyoitaja Mwenyezi Mungu katika kauli yake 'الرَّحْمٰنِ' na Akaihusisha na wenye roho

---

15 Sifa zote njema – mwanzoni na mwishoni – ni Zake tu. (Al-Qasas 28:71)

16 Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu. (Al-Faatiha 1:2)

kwa kuacha vitu visivyo na uhai na mimea. Kisha baada yake kuna rehema maalumu nayo ni rehema ya sifa ya Urahimu. Na rehema hii inamshukia yule tu anayejibidiisha sana kwa kupata rehema zilizotarajiwa. Kwa hiyo, rehema hii huhusiana tu na walioamini na kumtii Mola Karima kama vile ilivyobainishwa katika kauli ya Mwenyezi Mungu [17] وَ كَانَ بِالْمُؤْمِنِيْنَ رَحِيْمًا . Basi imethibitika kwa nususi ya Kurani kwamba Urahimu unahusikana na waaminio tu. Ama Urahmani, huu unahusikana na wenye uhai wote hata shetani pia alipata hadhi katika huo kwa amri ya Mola wa walimwengu. Kwa kifupi, Urahimu unahusikana na baraka zilizo natija ya vitendo na huhusiana na waaminio tu sio makafiri na wapotevu. Kisha baada ya Urahimu kuna baraka nyingine nayo ndiyo baraka ya malipo kamili na ya matokea ya matendo na ya kuwafikisha watu wema kwenye natija ya wema na vitendo vizuri. Kwenye hii hii Mwenyezi Mungu Ameashiria katika kauli yake [18] مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ . Na hii ni baraka ya mwisho kutoka kwa Mola wa walimwengu, na baada yake baraka yoyote haikutajwa katika Kitabu cha Mungu Mjuzi wa walimwengu. Na tofauti kati ya baraka hii na na baraka ya Urahimu ni kwamba Urahimu unamfikishia msafiri amwendaye Mungu mahali palipo

---

[17] Naye ni Mrehemevu kwa waaminio. (Al-Ahzaab 33:44)

[18] Mmiliki wa siku ya malipo. (Al-Faatiha 1:4)

njia ya kupata neema. Ama baraka ya Umaliki, hii inamfikisha amwendaye Mungu kwenye neema yenyewe na kwenye mwisho wa matunda na lengo la matakwa na mwisho wa makusudi. Hivyo, ni dhahiri kwamba baraka hii ndiyo baraka ya mwisho kutoka kwa Mungu Mmoja na ni kama lengo hasa la uumbaji wa mwanadamu. Na kwa sifa hii (ya Umaliki) neema zote zinakamilika na kwayo duara la maarifa na duara la silsila hukamilika. Je, hujaona kwamba silsila ya makhalifa wa Musa[as] iliishia kwenye مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ , na Isa[as] alidhihiri mwishowe. Na ujeuri na dhuluma vikabadilishwa kwa uadilifu na ihsani bila ya vita na wapiganaji vita kama vile ifahamikavyo kwa neno la dini, kwani neno hili limetumika kumaanisha uvumilivu na upole katika lugha ya Waarabu na sawa na maoni ya waandishi wao wote. Hivyo, mfanano wa Mtume[saw] wetu kwa Musa[as] ***Kalimullah*** na mshabaha wa makhalifa wa Musa[as] kwa makhalifa wa Mtume wetu Mtukufu[saw] ulitaka kwamba adhihiri mwishoni mwa silsila hii mtu afananaye na Masihi[as] na awaite watu kwenye Mungu kwa upole na kuondoa vita na kuweka upanga mkali katika ala yake na kujumuisha watu kwa ishara kutoka kwa Rahmani, si kwa upanga na mkuki. Hivyo, zama zake zitafanana na zama za kiama na siku ya malipo na ufufuo. Na ardhi itajaa nuru kama vile ilivyokuwa imejaa dhuluma na uongo. Na Mwenyezi Mungu Aliamua kuonyesha mfano wa siku ya malipo kabla ya

siku ya malipo na kuwafufua watu baada ya mauti ya takwa. Na huu huu ndio wakati wa Masihi Mau'udi na hizi ndizi zama zangu mimi mnyenyekevu. Kwenye hii hii Mungu Aliashiria katika aya يَوْمِ الدِّيْنِ . Basi atafakari aliye miongoni mwa wenye kutafakari. Kwa kifupi ni kwamba katika sifa hizi zinazomhusu Mungu Mwenye fadhili na ihsani mna uhakika uliofichikana na habari iliyofichiwa kutoka kwa Mungu Manani, nayo ndiyo kwamba Mwenyezi Mungu kwa kutaja sifa hizi Alitaka kumwambia Mtume[saw] wake uhakika wa sifa hizi, basi Akamdhihirishia uhakika wake kwa misaada ya aina aina. Hivyo, Akamlea Nabii[saw] wake na masahaba zake na Akathibitisha kwa njia hii kwamba Yu Mola wa walimwengu. Kisha Akawatimilizia neema zake kwa Urahmani wake bila kitendo chochote cha watendaji na hivyo Akathibitisha kwamba Yu Mrehemevu zaidi kuliko warehemevu wote. Kisha Akaonyesha hisani za ulinzi wake kwa rehema yake wakati wa amali yao na kawasaidia kwa roho kutoka kwake kwa hisani yake na kawajaalia nafsi zilizotulia na kawateremshia utulivu wa kudumu. Kisha Alitaka kuwaonyesha mfano wa مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ , basi Akawapa utawala na ukhalifa na Akawaangamiza maadui zao. Akawahilikisha makafiri na kuwamaliza kabisa kabisa. Kisha Akaonyesha mfano wa ufufuo na kawatoa kutoka makaburini, nao wakaingia katika dini ya Mungu makundi-makundi. Wakaikimbilia mmoja mmoja na

makundi makundi. Basi masahaba wakaona wafu kuhuika na wakaona mvua kita baada ya ukame. Na zama zile zikaitwa siku ya malipo, kwani haki ikadhihirika na majeshi ya makafiri yakaingia katika dini. Kisha Akanuia kuonyesha mfano wa sifa hizi katika watu wengine wa umati huu ili mwisho wa dini hii kihali iwe mithili ya mwanzo wake na ili mfanano wake na nyimati zilizopita utimie kama vile ilivyoashiriwa katika sura hii, yaani kauli Yake صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ[19] . Basi uzingatie maneno ya aya hii. Na zama za Masihi Mau'udi ziliitwa يَوْمِ الدِّيْنِ kwani hizi ni zama ambamo dini itahuishwa na watu watakusanywa ili wakubali kwa yakini. Hakuna shaka wala hitilafu kwamba Yeye Amezielea zama zetu hizi kwa kila aina ya ulezi na Ametudhihirishia baraka nyingi za Urahmani na Urahimu kama vile Alivyowadhihirishia manabii na mitume na mawalii na marafiki waliopita. Iliyobaki ni sifa ya nne kati ya sifa hizi, yaani dhihirisho litakalodhihiri katika sura ya Mfalme au Mmiliki katika siku ya malipo kwa kutoa thawabu au adhabu. Basi Akalifanya dhihirisho hili kama miujiza kwa Masihi Mau'udi na Akamfanya yeye kuwa mwamuzi na dhihirisho la utawala wa kimbingu kwa misaada kutoka kwa ghaibu na ishara mbalimbali. Na utajua uhakika huu wakati wa kutoa maelezo ya اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ . Na sikusema hayo kutoka kwa nafsi yangu bali

[19] Njia ya wale Uliowaneemesha. (Al-Faatiha 1:7)

nimejaaliwa elimu hizi za ndani kutoka kwa Mola wangu. Na atakayetaamali ipasavyo na kutafakari katika ishara hizi atajua kwamba Mwenyezi Mungu Ametoa humo habari kuhusu Masihi Mau'udi na zama zake zilizo zama za baraka. Tena ujue kwamba aya hizi zimetokea kama ndio ufafanuzi uliowekewa mpaka wa kujulisha elimu ya ndani kumhusu Mungu Mwumbaji wa walimwengu, ingawa Mwenyezi Mungu ameepukana na mipaka. Na kwa fundisho hili na habari hii yabainika maana ya ***kalima ya shahada*** ambayo ni msingi wa imani na wema. Na kwa sifa hizi Mungu Anastahiki kutiiwa na kuwa mahususi kuabudiwa. Kwani Yeye ndiye Aziteremshaye neema hizi kwa kusudi, kwani unaposema لَآاِلٰهَ اِلَّا اللهُ , maana yake kwa wenye akili ni hii kwamba hapaswi yeyote, wa kiumu wala wa kike, kuabudiwa isipokuwa Yule tu asiyefahamika ajijumuishiaye sifa hizi, yaani Urahmani na Urahimu, ambazo ndizo sifa mbili zilizo sharti la kwanza kwa Yule Anayestahiki kuabudiwa. Tena ujue kwamba Allah ni ***Ism Jaamid*** (nomino tuli), uhakika wake haufahamiki kwani ni اِسْمُ الذَّاتِ (jina la Dhati), na kwa hiyo sio vitu vinavyofahamika. Na kila linalosemwa kuhusiana na maana yake ni batili na upuuzi, kwani uhakika wa Mwenyezi Mungu ni juu kuliko kuwazika na mbali kukisika. Na usemapo مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللهِ basi maana yake ni hii kwamba Muhammad[saw] ndiye dhihirisho la sifa za Dhati huyu na Khalifa wake katika ukamilifu na atimizaye duara

la kivuli na Khatam wa Utume. Basi matokeo ya kuona na kushuhudia kwangu ni kwamba Nabii[saw] wetu aliye Mbora wa viumbe amezirithi sifa hizi mbili (Rahman na Rahim) za Mola wetu Mtukufu; kisha Masahaba wakaurithi uhakika wa Umuhammadi wa kijalali kama ulivyojua katika maelezo yaliyopita. Na upanga wao unatambulika kung'olea mbali mzizi wa washirikina. Wanayo kumbukumbu wasiyoisahau waabudu mahuluku. Wakatimiliza haki ya sifa ya Umuhammadi na kuwaonjeshea wengi mwonjo wake vitani. Sasa baada yake ilibaki sifa ya Uahmadi iliyopakwa rangu za ujamali na kuunguzwa na moto wa upendo. Basi, Masihi Mau'udi akairithi (sifa hii ya Uahmadi) aliyetumwa katika zama za kukatika njia za ustawi na kuvunjwa-vunjwa dini kwa magego ya maadui, kuadimika kwa wasaidizi na marafiki, utawala wa maadui na shambulio la makundi ili Mwenyezi Mungu Aonyeshe mfano wa 'Mmiliki wa siku ya malipo' baada ya mausiku ya giza na baada ya kuvunjika nguvu ya Islam na heba ya masultani (Waislamu) na baada ya dini kuwa kama wanyonge. Basi, leo dini yetu imekuwa kama wageni na haukubaki popote utawala wake isipokuwa huko mbinguni tu. Watu wa ardhi hawakuitambua na wamesimama dhidi yake kama maadui. Basi wakati wa udhaifu huu na kutoweka kwa heshima Akamtuma mja wake mmoja ili kama mvua azimwagilie maji zama za ukame. Basi yeye ndiye Masihi

Mau'udi aliyekuja wakati wa udhaifu wa Islam ili Mwenyezi Mungu Aonyeshe watu ambao baada ya kifo (cha kiroho) wakawa kama wanyama, mfano wa kujumuika, kufufuka, kusimama na mfano wa siku ya malipo kama neema yake. Basi, ujue kwamba zama hizi ni siku ya malipo, na utajua ukweli wetu walau baada ya muda fulani. Hapa kuna elimu ya ndani ya kikashfi isiyopata kusikika hapo kabla, basi sikiliza kwa kutega masikio kwa utulivu, nayo ndiyo hii kwamba Mwenyezi Mungu katika sehemu hii Amejichagulia sifa nne ili Aonyeshe mfano wa sifa hizi katika dunia hii hii kabla ya mauti. Ndiyo maana Aliashiria katika kauli yake لَهُ الْحَمْدُ فِي الْأُوْلٰى وَ الْاٰخِرَةِ[20] kwamba mfano huu walipewa watu wa mwanzoni mwa Islam kisha watapewa watu wengine wa umati huu uliofedheheka. Kadhalika Alisema katika sehemu nyingine, naye ndiye Mkweli wa wakweli wote, ثُلَّةٌ مِّنَ الْاَوَّلِيْنَ ـ وَ ثُلَّةٌ مِّنَ الْاٰخِرِيْنَ[21]. Hivyo Aligawa zama za mwongozo, auni na msaada kati ya zama za Nabii[saw] wetu na zama za mwisho ambazo ni zama za Masihi wa umati huu. Na kadhalika Alisema وَ اٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ لَمَّا يَلْحَقُوْا بِهِمْ[22]. Humo Ameashiria kwenye Masihi Mauudi, Jumuiya yake

---

[20] Sifa zote njema – mwanzoni na mwishoni – ni Zake tu. (Al-Qasas 28:71)

[21] Jamii kubwa ni miongoni mwa watu wa kwanza. Na jamii kubwa ni miongoni mwa (watu) wa mwisho. (Al-Waaqi'a 56:40-41)

[22] Na kwa wengine miongoni mwao walio bado kuungana nao. (Al-Jumu'a 62:4)

na wafuasi wake. Basi imethibitika kutokana na nususi zilizo wazi za Kurani Tukufu kwamba sifa hizi ziliishadhihirika katika zama za Nabii[saw] wetu, tena zitadhihiri katika zama za mwisho pia, nazo ndizo zama ambamo utakithiri ufasiki na ufisadi, na utapungua wema na ukweli, Islam itang'olewa jinsi mti unavyong'olewa, hali ya Islam itakuwa kama ya yule aliyeumwa na nyoka, Waislamu watakuwa kana kwamba ni maiti na dini itakanyagwa chini ya misiba ifurikayo. Na hivyo ndivyo mnavyoona katika zama hizi na kushuhudia ufasiki, kufuru, ushirikina na uasi wa aina aina. Na mwaona wafisadi wamekithiri na wasuluhishi wahurumiao wamepungua na wakati umewadia kwa sheria kufutiliwa mbali na umati kukomeshwa. Hii ndiyo balaa iliyoshuka ghafla, ni msiba ulioshambulia, ni shari iliyoibuka na ni moto uliowateketeza Waarabu na wasio Waarabu. Hata hivyo, wakati wetu sio wakati wa jihadi wala zama za panga kali wala za mauaji na kutia minyororo na kala za chuma shingoni wala zama za kutolewa amri za kuua na kuhilikisha. Kwani wakati huu ni wakati wa ushindi wa makafiri na ukuu wao, na Waislamu wakadhalilishwa kwa vitendo vyao. Na jihadi itakuwaje ilihali yeyote hazuiliwi kufunga saumu na kusali wala kuhiji na kutoa zaka wala kufanya wema na kushika takwa, wala kafiri yeyote hajachomoa upanga dhidi ya Waislamu kwa kuwaritadisha au kuwakata-kata. Na uadilifu ni huu

kwamba upanga uchomolewe kuukabili upanga na kalamu kuzikabili kalamu. Na hatulii juu ya majeraha ya upanga na mkuki, bali twalia juu ya uongo wa ulimi. Na kwa kutumia uongo tu vitabu vya Mungu vilikadhibishwa na kufichwa mafundisho yao bora na jengo la dini likashambuliwa na nyumba yake ikabomolewa. Basi ikawa kama mji uliovunjwa kuta zake, au kama bustani iliyoteketezwa miti yake au kama kiunga kilichotilifikishwa maua na matunda yake na kuanguka matumba yake, au ni kama nchi takatifu iliyokauka mito yake, au kama kasri imara zilizofutwa hata alama zake na wavunjao wamezivunjilia mbali. Na ikasemwa kwamba (umati huu) umekufa na waletao habari ya mauti wameishaleta habari ya kufa kwake, na habari za kifo chake zikachapishwa na waenezaji wamezieneza. Kila ukamilifu lazima ufifie siku moja, na kila ustawi lazima udhoofike kama unavyoona mafuriko yafikiapo mlima imara yanatulia, na usiku unapofikia asubuhi yenye mwanga, giza huondoka kama vile Mwenyezi Mungu Alivyosema: وَالَّيْلِ إِذَا عَسْعَسَ ۝ وَالصُّبْحِ إِذَا تَنَفَّسَ[23] . Basi Amekufanya kupambazuka asubuhi kuwa jambo la lazima baada ya giza la usiku. Na hivyo ndivyo katika kauli Yake يَٰٓأَرۡضُ ٱبۡلَعِي مَآءَكِ[24] ilivyofanyiwa ukamilifu wa mafuriko

[23] Na kwa usiku uondokapo na kwa asubuhi inapopambazuka. (At-Takwiir 81:18-19)

[24] Ewe ardhi! meza maji yako. (Huud 11:45)

kuwa alama ya kumalizika kwake. Basi, Mwenyezi Mungu Alitaka Awarudishie waaminio siku zao za awali na kuwaonyesha kwamba Yu Mola wao na Yu Rahmani na Rahimu na Mmiliki wa siku ya malipo ambamo wafu watafufuliwa. Na bila shaka mnaona katika zama hizi ulezi wa Mungu Manani na Urahmani wake kwa wanadamu na wanyama unaoihusu miili. Na mwaona jinsi alivyoumba njia kadhaa mpya na njia zenye manufaa na viwanda ambavyo mfano wake haukuonekana katika zama zilizopita na maajabu ambayo mithili yake haikupatikana katika karne za awali. Na mtaona upya katika kila kitu kinachohusiana na msafiri, mgeni, mkazi, mpita njia, mwenye afya, mgonjwa, mpiganaji, msuluhishi, hali ya kukaa na kusafiri, neema zote za aina aina na matatizo, kana kwamba dunia nzima imebadilika kabisa. Na hakuna shaka kwamba hayo yote ni Ulezi adhimu na Urahmani mkubwa. Kadhalika utaona Ulezi, Urahmani na Urahimu katika mambo ya dini. Kwa hakika mambo yote wamerahisishiwa wanafunzi wa elimu za kiroho, na kazi ya mahubiri na uenezaji wa elimu za kiroho imerahisishwa. Na ameteremshiwa ishara kila anayemwabudu Mungu na kutaka utulivu kutoka Kwake. Mwezi na jua vimeshapatwa katika Ramadhani na ngamia wameachwa, sasa hutumiwa kwa nadra tu. Na karibuni utaona chombo kipya cha usafiri kupita baina ya Makka na Madina. Wataalamu na wanafunzi wamesaidiwa kwa

wingi wa vitabu na njia za elimu ya aina aina. Na miskiti yaendewa na watu na mwabudu amepewa ulinzi; milango ya amani na mahubiri imefunguliwa; na hayo yote ni baraka ya Urahimu. Basi twawajibika kushuhudia kwamba hizi ni mbinu ambazo haupatikani mfano wake katika karne za awali. Na hii ndiyo taufiki na urahisi ambao mfano wake halikusikia sikio wala halikuona jicho mithili yake. Basi uuone Urahimu wa Mola wetu Mtukufu. Na huu ndio Urahimu wake kwamba tumeweza kuchapa vitabu vingi vya dini yetu katika siku chache ambavyo haikuwa katika uwezo wa watu wa awali kuviandika kiasi hiki katika miaka. Leo twaweza kupata habari za maeneo ya mbali katika masaa machache[25] ilihali watu wa zamani walikuwa wakizipata kwa taabu na kujibidiisha sana kwa miaka na miaka. Na tumefunguliwa kwa kila heri milango ya Ulezi, Urahmani na Urahimu na ziko njia zake nyingi ambazo kuzihesabu ni nje ya uwezo wa kibinadamu. Ulikuwa wapi urahisi huu kwa wahubiri wa zamani! Ardhi ilitetemeshwa sana kwa ajili yetu, basi ikatoa nje mizigo yote, mifereji ikatiririshwa, mito ikakaushwa, zikaundwa njia mpya za usafiri na ngamia wakaachwa. Watu wa zamani hawakuziona neema tulizoona. Kwenye kila hatua kuna neema zisizohesabika.

---

[25] Tanbihi: Kama Alivyosema Mwenyezi Mungu يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا .
Yaani, Siku hiyo (ardhi) itahadithia habari zake. (Az-Zilzaal 99:5)

Lakini pamoja na hayo kifo cha moyo na ugumu wa mioyo vimekithiri kana kwamba watu wote wamekufa na haikubaki ndani mwao roho ya maarifa isipokuwa kidogo tu kana kwamba haipo kwa sababu ya kuwa nadra. Na tumefahamu kwa kudhihirika sifa hizi tulizotaja nyuma, kwa dhihirisho la Ulezi, Urahmani na Urahimu kama ishara zing'aazo, tena kwa wingi wa vifo na mauti ya watu kwa sumu ya upotevu, kwamba siku ya ufufuo i karibu, bali ipo mlangoni kama ilivyo wazi kwa dhihirisho la alama na sababu hizo. Kwani, Ulezi, Urahmani na Urahimu vimefura kama mawimbi ya bahari na kudhihirika na kufululiza na kutiririka kama mito. Basi, hakuna shaka kwamba wakati wa kufufuka umewadia na suna hii imeshapita katika masahaba wa Mbora[saw] wa viumbe. Bila shaka zama hizi ndiyo siku ya malipo na siku ya ufufuo na siku ya Umiliki wa Mola wa mbingu na ya kudhihirika kwa athari za sifa hizo mioyoni mwa wakazi wa ardhi. Na hakuna shaka kwamba zama hizi ndizo zama za Masihi mwamuzi kutoka kwa Hakimu wa mahakimu wote. Na huu ni ufufuo baada ya hilaki ya watu, na mfano wake umeshapita katika zama za Isa[as] na zama za Khatamun Nabiyyiin[saw]. Basi tafakari wala usiwe miongoni mwa waliokughafilika.

MLANGO WA TANO

Kuhusu maelezo ya

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

Ujue kwamba hakika ya ibada Anayoikubali Mola kwa hisani Yake ndiyo kujinyenyekeza kikamili kwa kuona adhama Yake na utukufu wa shani Yake, na kumsifu kwa kushuhudia rehema Zake a hisani Zake za aina aina, na kumtanguliza juu ya kila kitu kwa huba Yake na kwa kufikiria sifa Zake na uzuri Wake na nuru Zake, na kutakasa moyo katika ushawishi wa mashetani kwa kufikiria Pepo Zake. Na ibada bora zaidi ni hii kwamba mtu ahifadhi sala tano kusali katika nyakati za awali, na kujitahidi kwa kutia moyo ndani yake na kwa upendo, shauku na kwa kujipatia baraka zake kwa kujidumisha juu ya kutekeleza faradhi zake na suna zake. Kwa hakika sala ni rikabu amfikishaye mja kwa Mola wa waja wake. Basi, kwa sala hizi mja hufikia pale asipoweza katu kufikia hata kwa kupanda farasi wenye mbio sana. Na windo la sala haliwezi kuwindwa kwa mishale na siri yake haidhihiriki kwa kalamu. Na aliyeshikilia njia hii, amefikia haki na uhakika na akampata mahababu aliyeko mapaziani mwa ghaibu na kujiokoa katika shaka na wasiwasi. Basi utaona siku zake zinang'aa na maneno yake ni lulu na uso wake mwezi mpevu na mahali pake pako mbele. Na anayemnyenyekea Mungu katika sala zake, Mwenyezi Mungu Huwainamisha wafalme mbele yake na kumfanya

yule mtumwa Wake kuwa mmiliki. Tena ujue kwamba Mwenyezi Mungu Alihimidi dhati Yake kwanza katika kauli yake اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ[26] kisha Amewahimiza watu juu ya ibada sawa na kauli Yake اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَ اِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ[27] . Humo imeashiriwa kwamba kwa hakika mwabudu ni yule tu anayemhimidi Yeye ipasavyo. Basi matokeo ya dua na ombi hili ni kwamba Mwenyezi Mungu humfanya yule anayedumu kushughulikia ibada kuwa Ahmad. Kwa hiyo, ilikuwa lazima kwamba kwenye mwisho wa umati huu awepo Ahmad kwa kufuata nyayo za Ahmad[saw] wa kwanza aliye Seyidi wa walimwengu ili ieleweke kwamba dua ile imekubaliwa na Mungu Atakabaliye maombi na ili kudhihirika kwake kuwe kama alama kwa kukubaliwa maombi. Basi, huyu ndiye Masihi ambaye kudhihiri kwake kuliahidiwa katika zama za mwisho ilivyoandikwa katika Sura Al-Faatiha na katika Kurani Tukufu. Kisha katika aya hii kuna ishara kwamba mtumishi yeyote hawezi kutekeleza ibada isipokuwa kwa kuwezeshwa na Mungu. Hii ni sehemu ya ibada kwamba umpende akufanyiaye uadui jinsi unavyoipenda nafsi yako na wana wako, na kwamba uwasamehe makosa ya wengine na

[26] Sifa zote njema zinamhusu Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu. (Al-Faatiha 1:2)

[27] Wewe tu twakuabudu na Wewe tu twakuomba msaada. (Al-Faatiha 1:5)

kuachilia kuteleza kwao na uishi kwa takwa, usafi, moyo safi na utakaso wa ndani, na uwe mwaminifu halisi mwenye kuepukana na mienendo mibaya. Na uwe mtu wa kuwanufaisha mahuluku wa Mungu kwa sifa ya asili kama baadhi ya mimea, bila kujikalifisha na kujisingizia; na kwamba usimwudhi ndugu yako kwa kiburi chako wala usimjeruhi kwa maneno, bali unawajibika kumjibu ndugu aliyekasirika kwa upole wala usimhakiri katika mazungumzo na ufe kabla ya kufa na ujihesabu katika wafu. Na umheshimu kila anayekujia ingawa aje akivaa nguo zilizoraruka, si mavazi yenye thamani. Na umsalmie kila mtu unayemtambua au humtambui na usimame ukiwa tayari kuhurumia.

MLANGO WA SITA

Kuhusu maelezo ya aya

اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ ۔ صِرَاطَ الَّذِيۡنَ اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ [28]

Ujue kwamba aya hizi ni hazina iliyojaa maarifa ya ndani na hoja ing'aayo dhidi ya wapinzani wanaume kwa wanawake. Nasi tutazieleza waziwazi na kukuonyesha dalili na hoja Mwenyezi Mungu Alizotufahamisha. Basi nisikilize kwa makini maelezo yake ili Mwenyezi Mungu Akuokoe katika mawazo batili. Ama kauli hii ya Mwenyezi Mungu اِهۡدِنَا الصِّرَاطَ الۡمُسۡتَقِيۡمَ , basi tafsiri yake ndiyo hii kwamba Ee Mungu, Utuonyeshe njia iliyonyoka na utuimarishe juu ya njia ifikishayo kwako na iokoayo katika adhabu yako. Vilevile ujue kwamba kwa kupata mwongozo kuna njia kadha sawa na masufii zitokanazo na Kitabu na Suna. Ya kwanza katika hizo ni kutafuta maarifa kwa dalili na hoja. Ya pili ndiyo kutakasa batini kwa mazoezi ya aina mbalimbali ya kiroho. Na ya tatu ni kujielekeza kwa Mungu pekee na uhalisi wa mahaba na

---

[28] Tanbihi: Ujue kwamba katika aya اَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ kuna bishara kwa waaminio na ishara hii kwamba Mwenyezi Mungu Amewatayarishia vyote alivyowapa manabii wa zamani. Kwa hiyo Alifundisha dua hii ili iwe habari njema kwa watafutao haki. Basi imelazimu kwamba mlolongo wa makhalifa wa Muhammad[saw] uishie kwa mithili ya Isa[as] ili kushabihiana kwake kutimie kwa mlolongo wa Musa[as]. Na karima anapoahidi, huwa anaitimiliza. Mwandishi

kuomba msaada wa Mwenyezi Mungu kwa mwafaka mkamilifu na kutofarakana, kwa kutubia kwa Mungu, maombi kwa kujinyenyekeza na dua na kwa azimio imara. Kisha kwa kuwa njia ya kutafuta mwongozo na utakaso wa nafsi haitoshi kwa kumfikia Mungu bila kupitia maimamu na waja wa umati huu walioongozwa na Mungu, kwa hiyo Mwenyezi Mungu hakuridhika kwa kufundisha tu dua hii اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ , bali kwa kauli yake صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ Amehimiza kutafuta waongozi miongoni mwa wenye bidii na wateule, yaani mitume na manabii. Kwani, hao ndio watu walioitanguliza nyumba ya haki juu ya nyumba ya uongo na ulaghai na wakavutwa kwa Mungu Aliye bahari ya nuru kwa kamba za huba na wakatolewa katika ardhi ya batili kwa wahyi wa Mungu na kivutio kutoka kwake. Na kabla ya kupata unabii walikuwa kama msichana mzuri asiye na mapambo. Hao hawatamki ila kutamkishwa na Mola. Na hawakitangulizi kitu isipokuwa kilicho bora mbele Yake. Hujibidiisha sana kuwafanya watu kutekeleza sheria ya Mola na kusimamia malezi yao kama mjane amleaye mwanaye. Nao hujaaliwa umbuji unaowasikilizisha viziwi na kuwateremsha kulungu wenye mikono myeupe. Na hujaaliwa moyo unaovuta nyimati kwa bidii. Na wanaposema, mshale wao haukosi lengo na wakazapo fikira huwahuisha wafu waliokosa kupata matumaini. Wanajibidiisha kuwatoa watu katika hatia na kuwapeleka

kwenye mema na kuwahamisha kutoka katika makatazo na kuwapeleka kwenye wema, na kuwaondoa katika ujahili na kuwafikisha kwenye heshima, staha na akili, na kuwaokoa katika uovu na uasi na kuwaelekeza kwenye unyofu na takwa. Na awakataaye, amepoteza neema kubwa aliyoletewa na kaenda mbali na chemchemi ya heri na nuru ya macho yake. Na uvunjaji wa uhusiano huu ni mkubwa zaidi kuliko uvunjaji wa uhusiano na jamaa wa damu na kabila. Hao (mitume) ndio matunda ya Peponi. Basi, ole wake anayetengana nao na kuelekea kwenye maakuli. Na hao ndio nuru ya Mwenyezi Mungu na kuwapitia hao mioyo hupewa nuru na kiuasumu kwa sumu ya dhambi na utulivu wakati wa kukaribia kifo na gharighari ya mauti na uthabiti wakati wa kuondoka na kuacha dunia hii duni. Je, wadhani kwamba yeyote minghairi yao aweza kuwa kama kundi hili takatifu? Hasha, naapa kwa yule aliyeotesha mtende kutoka katika kokwa. Kwa lengo hili Mwenyezi Mungu Alifundisha dua hii kwa rehema yake ya hali ya juu na Akawaamuru Waislamu watafute njia ya wale walioneemeshwa na Mwenyezi Mungu, yaani manabii na mitume. Kwa aya hii imemdhihirikia kila mwenye busara kwamba umati huu umetumwa juu ya nyayo za manabii. Na hakuna nabii ila mja mithili yake yupo katika umati huu. Na kama usingekuwa mshabaha na mfanano huu, kungekuwa bure kujitakia ukamilifu wa waliopita zamani na ingebatilika

dua hii. Basi Mwenyezi Mungu ndiye Aliyetuamuru sote kusema اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ tukisali na kuomba jioni na asubuhi na kutafuta njia ya wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu, yaani manabii na mitume. Na Ameashiria kwamba Amepanga tangu mwanzo ya kuwa Atawatuma baadhi ya watawa katika umati huu juu ya nyayo za manabii na kwamba Atawafanya makhalifa kama Alivyowafanya makhalifa hapo kabla katika wana wa Israeli. Hii ndiyo haki, basi uachane na mabishano ya bure. Kusudio la Mungu lilikuwa kujumuisha katika umati huu sifa kamilifu mbalimbali na huluka za aina aina. Hivyo basi, suna Yake ya zamani ilitaka kwamba Afundishe dua hii kisha Afanye Atakayo. Ameuita umati huu kuwa umati bora katika Kurani Tukufu. Na heri hii hupatikana ambapo amali, imani, elimu na maarifa vyaongezeka na radhi ya Mungu Rahmani yatafutwa. Na ndivyo hivyo alivyowaahidi wale walioamini na kutenda vitendo vizuri kwamba Atawafanya makhalifa katika ardhi kwa fadhili na rehema zake kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao miongoni mwa watu wema na wamchao Mungu. Basi imethibitika kutokana na Kurani Tukufu kwamba makhalifa miongoni mwa Waislamu wataendelea kutokea mpaka siku ya kiama na kwamba hakuna atakayekuja katu kutoka mbinguni bali watatumwa kutoka katika umati huu huu. Umekuwaje huamini yaliyoaridhiwa na Kurani Tukufu. Je, umekiacha

Kitabu cha Mungu, au haikubakia ndani mwako hata chembe ya maarifa? Mwenyezi Mungu Amesema miongoni *mwenu* wala hakusema miongoni mwa *wana wa Israeli*. Na hii tu inakutosha kama unataka haki na kutafuta dalili. Ee maskini, soma Kurani wala usitembee kama mwenye maringo. Usiende mbali na nuru ya haki ili Sura Al-Faatiha na Sura An-Nuur zisikushtaki mbele ya Mungu. Umche Mungu, tena umche Mungu, wala usiwe kafiri wa kwanza wa aya za Sura An-Nuur na Sura Al-Faatiha ili zisisimame hizi mbili kushuhudia dhidi yako mbele ya Mwenyezi Mungu. Nawe unasoma kauli Yake وَعَدَ اللّٰهُ الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا مِنْكُمْ[29] na unasoma pia kauli Yake لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ[30]. Basi zingatia kauli yake 'miongoni mwenu' ndani ya Sura An-Nuur na uachane na wadhalimu na dhana yao. Je haukuwadia wakati kwa ajili yako kuelewa usomapo aya hizi kwamba Mwenyezi Mungu Amewafanya makhalifa wote kutoka katika umati huu kwa hisani zake? Hivyo basi, Masihi Mau'udi atakujaje kutoka mbinguni. Je, kwako Masihi Mau'udi hayuko miongoni mwa makhalifa? Basi umemdhaniaje kutoka katika wana wa Israeli na miongoni mwa manabii wao. Je waiacha Kurani ilihali maponyo yote yamo ndani ya Kurani Tukufu, au bahati yako mbaya imekushinda kiasi hiki kwamba unaacha kwa

---

[29] (An-Nuur 24:56)

[30] (An-Nuur 24:56)

kusudi njia ya mwongozo? Je, huzingatii kauli Yake Mwenyezi كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِيْنَ مِنْ قَبْلِهِمْ[31] katika Sura hii. Kwa hiyo, Masihi ajaye sharti awe kutoka miongoni mwa umati huu huu sio lazima awe kutoka miongoni mwa wengine wao. Kwani, neno كَمَا (kama) hutumika kwa kufananisha na kumithilisha. Mfanano unahitaji tofauti kiasi kidogo. Kama ilivyodhahiri shahiri kwamba kitu chochote hakifanani na hicho hicho chenyewe. Basi imethibitika kwa nunusi hasa kwamba Isa[as] angojewaye atatokana na umati huu na jambo hili ni la yakini na halina shaka kabisa. Haya ndiyo Kurani Tukufu imeyasema na maulamaa wanayajua. Basi baada ya hakika hii mtaliamini jambo gani! Kurani Tukufu inasema kwamba Isa[as], nabii wa Mungu, ameshafariki. Basi uzingatie kauli Yake فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِيْ[32] wala usiwahuishe wafu wala usiwasaidie Wakristo kwa mambo ya uongo na upuuzi. Fitina zao si chache, basi usizizidishe kwa ujahili. Na kama unapenda uhai wa nabii yeyote basi uuamini uhai wa Nabii wetu[saw] mbora kuliko viumbe wote. Umekuwaje, unamfikiria kuwa mfu aliye Rehema kwa walimwengu na una itikadi kwamba mwana wa Mariamu yu miongoni kwa walio hai bali miongoni mwa wafufuaji. Iangalie sura ‘An-Nuur’ kisha

[31] Kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao. (An-Nuur 24:56)

[32] Basi Uliponifisha. (Al-Maaida 5:118)

iangalie sura 'Al-Faatiha' kisha rejesha jicho ili jicho lirejee kwa hoja madhubuti. Je, husomi صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ[33] katika Sura hii. Basi unageuzwa wapi baada yake. Je, umesahau dua yako au unaisoma kwa kughafikia? Kwani, ulimwomba Mola wako katika dua hii na ombi hili kwamba Asimwache nabii yeyote wa wana wa Israeli isipokuwa Amwinue mithili yake katika umati huu. Ole wako, je ulisahau dua yao haraka kiasi hiki ilihali unaisoma nyakati tano kila siku. Nimekustaajabia sana; je hii ndiyo dua yako na hizo ndizo fikara zako? Iangalie Sura Al-Faatiha na uiangalie Sura An-Nuur za Furkani; baada ya ushahidi wa Kurani Tukufu shahidi yupi atakubaliwa. Basi usiwe kama yule aliyeacha hata kuhisi hofu ya Mungu kidhahiri na kibatini, Akajivalia libasi ya upujufu na vazi la ndani pia la upujufu. Je, utaacha Kitabu cha Mungu kwa wale walioenda kombo wala hawakukamilisha utafiti na tafakuri. Njia yao haifikishi kwenye shabaha, ni kinyume cha Tauhidi na njia za Mungu Mpendwa. Basi usiione njia ngumu kuwa rahisi ingawa imesawazishwa kwa kukanyagwa sana na ingawa kwale[34] wameelekea huko makundi kwa makundi. Kwani mwongozo wa kweli ni mwongozo wa Mungu. Kurani

---

[33] (Al-Faatiha 1:7)

[34] Kwale katika matini ya Kiarabu ni قَطا na قطاkwa Kiingereza aitwa sandgrouse – aina fulani ya kwale.

Tukufu imeshuhudia kifo cha Masihi[as] na imemwingiza katika wafu kwa maneno yaliyo wazi. Umekuwaje huizingatii kauli Yake فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِىْ[35] na kauli Yake قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ[36]. Umekuwaje hujichagulii njia ya Furkani na unafurahia njia zingine ilhali Amesema فِيْهَا تَحْيَوْنَ وَ فِيْهَا تَمُوْتُوْنَ[37]. Mmekuwaje hamtafakari. Pia Amesema kao lenu litakuwa katika ardhi na posho kwa muda. Basi kao la Isa[as] limekuwaje huko mbinguni au kwenye arshi ya Mola wa walimwengu? Huu ndio uongo wazi. Mungu Subhanahu Amesema اَمْوَاتٌ غَيْرُ اَحْيَآءٍ[38], basi kwa msingi gani mnamdhania Isa[as] kuwa miongoni mwa wazima. Aibu, aibu! Enyi watu wa Rahmani, shikeni Kurani, shikeni Kurani. Mcheni Mungu wala msiiache Furkani. Hiki ni Kitabu ambacho juu yake kila mtu na jini ataulizwa. Nanyi mnasoma Sura Al-Faatiha katika sala, basi enyi wenye akili itafakarini. Je, hamkuti humo aya صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ. Basi msiwe kama wale waliopoteza nuru ya macho yao na kikapotea walichokuwa nacho. Ole wenu! je, ipo hoja nyingine baada ya Kurani au pamebaki pa kukimbilia? Je, akili yenu inakubali kwamba Mola wetu Atubashirie katika

---

[35] Basi Uliponifisha. (Al-Maaida 5:118)

[36] Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume wote. (Aali 'Imraan 3:145)

[37] Mtaishi humo na mtafia humo. (Al-A'raaf 7:26)

[38] Ni wafu, si wazima. (An-Nahl 16:22)

dua hii kwamba Atainua maimamu kutoka katika umati huu kwa wale watakao njia ya mwongozo, ambao watakuwa mfano wa manabii wa wana wa Israeli kwa kuchaguliwa na kuteuliwa, na kutuamuru tuombe dua kwamba tuwe kama manabii wa wana wa Israeli wala tusiwe kama wenye bahati mbaya wa wana wa Israeli, kisha baada yake Atufukuze na kututumbukiza mashimoni mwa bahati mbaya na kutuletea mtume mmoja wa Kiisraeli na kusahau kabisa ahadi yake? Huu ni udanganyifu dhahiri usioweza kunasibishwa kwa Mungu Manani. Mwenyezi Mungu Ametaja katika Sura hii makundi matatu: walioneemeshwa, Mayahudi na Manasara. Na Ametuhamasisha kujiunga katika kundi la kwanza katika hayo na Ametukatazia mengine mawili; bali Ametuhimiza kuomba dua, kunyenyekea na kulia ili tuwe ndani ya kundi la walioneemeshwa sio kundi la walioghadhabikiwa wala la waliopotea. Naapa kwa Yule aliyenyesha mvua kutoka mawinguni na kutoa matunda kutoka katika matumba. Pasipo shaka, haki imedhihirika kutokana na صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ na hataishuku aliyepewa hata chembe ya elimu. Mwenyezi Mungu Ametufanyia hisani kwa kutufafanulia vizuri mambo haya na kutudhihirishia na kutuondolea taklifu ya kutafakari. Basi wanawajibika watoao nje ndimi zao na kuzitikisa, kama swila na wanaokazia macho kama furukombe anavyolitazama windo lake kwamba wasiipuuzilie mbali neema hii wala

wasiwe kama wanyama. Jambo hili limeimarika moyoni mwangu kwamba Sura Al-Faatiha huyaponya majeraha yao na kuijaalia mikono yao mabawa. Hamna Sura yoyote ndani ya Kurani Tukufu ila hukadhibisha itikadi yao hii (uzima wa Masihi[as]). Basi, usome katika Kitabu cha Mungu popote utakapo, patakuonyesha njia ya ukweli na unyofu. Je, huoni kwamba Sura Banii Israaili inamzuia Masihi[as] kupaa mbinguni,[39] na kwamba Sura Aali 'Imraan inamwahidi kwamba Mwenyezi Mungu Atamfisha kifo cha kawaida[40] na kumhamisha kwenye wafu kutoka katika wazima. Kisha Sura Al-Maaida yamtandazia tandiko la chakula (***maaida***) cha kifo. Soma 'uliponifisha'[41] kama una shaka. Tena sura Az-Zumar inamweka katika makundi (***Zumar***) ambao hawarudi kwenye dunia hii duni. Ukitaka basi uisome فَيُمْسِكُ الَّتِيْ قَضٰى عَلَيْهَا الْمَوْتَ[42]. Na ujue kwamba kurejea duniani ni haramu baada ya mauti. Na ni haramu kwa mji Alioungamiza Mungu kufufuka kabla ya siku ya ufufuo. Ama kuhuishwa kimuujiza basi hakuna pia kurejea kwenye dunia iliyo mahali pa dhuluma na uongo. Tena kifo cha Masihi[as] kilipothibitika kwa nususi dhahiri ya Kurani basi

---

[39] (Banii Israaiil 17:94)

[40] (Aali 'Imraan 3:56)

[41] (Al-Maaida 5:118)

[42] Basi Huzizuia zile Alizozikidhia mauti. (Az-Zumar 39:43)

Mwenyezi Mungu Akaondolea mbali wasiwasi wa kushuka kwake kutoka mbinguni kwa maneno bayana. Na katika Sura An-Nuur na Al-Faatiha Ameashiria kwamba umati huu utawarithi kwa njia ya kivuli wana wa Israeli. Kwa hiyo, imewajibika kwamba Masihi aje katika zama za mwisho kutoka katika umati huu huu kama alivyokuja Isa[as] mwana wa Mariamu mwishoni mwa dini ya Musa[as]. Basi Musa[as] na Muhammad[saw] hufanana kwa nususi ya Furkani, rehema za Mungu ziwe kwao wawili. Na kwa hakika mlolongo wa ukhalifa huu unashabihiana na mlolongo huo jinsi ilivyotajwa katika Kurani Tukufu na humo hahitilafiani mtu yeyote yule. Karne za silsila ya makhalifa wa Musa[as] zimeishia kwa Isa[as] inazofanana idadi yao na siku za mwezi mpevu. Kwa hiyo ilikuwa hakuna budi Masihi wa umati huu adhihiri katika muda ulio kiasi hicho hicho. Na Kurani Tukufu imeashiria kwenye hiyo katika aya لَقَدْ نَصَرَكُمُ اللّٰهُ بِبَدْرٍ وَّ اَنْتُمْ اَذِلَّةٌ[43] . Bila shaka Kurani Tukufu ina maana zenye jiha mbalimbali jinsi maulamaa wakubwa wanavyojua. Basi hapa maana ya pili ya aya hii ndiyo kwamba Mwenyezi Mungu atasaidia waaminio kwa njia ya Masihi kudhihirika katika karne ambazo idadi yao ni kama siku za badiri kamili na katika zama hizo waaminio watakuwa wanyonge. Basi utafakari

[43] Bila shaka Mwenyezi Mungu Aliwasaidieni katika (vita vya) Badri hali ninyi mlikuwa dhaifu. (Aali‘ Imraan 3:124)

ndani ya aya hii jinsi inavyoashiria kwenye udhaifu wa Islam. Tena aya hii inaashiria kwenye hilali kuwa badiri katika muda uliowekwa na Mungu Mjuzi kama vile neno badiri linavyomaanisha. Basi sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu tu kwa fadhili na neema hii. Na matokeo ya tuliyosema kuhusu habari hii ni kwamba Sura Al-Faatiha inatoa habari njema ya Masihi kuwa kutoka katika umati huu ni fadhili ya Mlezi wa walezi wote. Basi tumebashiriwa katika Sura Al-Faatiha ujio wa maimamu kutoka miongoni mwetu walio kama manabii wa wana wa Israeli, na hatukubashiriwa ushukaji wa nabii kutoka mbinguni. Basi uzingatie hoja hii. Na umeshasikia hapo kabla kwamba Sura An-Nuur imetubashiria kuhusu silsila ya makhalifa itakayofanana na silsila ya makhalifa wa Musa[as]; na mfanano huu utatimiaje bila kudhihiri Masihi katika mwisho wa silsila ya Musa[as]. Na tumeamini ahadi hii kwani hii imetoka kwa Mola wa watumishi wake; na Mwenyezi Mungu Haihalifu ahadi. Na ni ajabu juu ya kaumu hii kwamba hawakuzingatia ahadi ya Mwenyezi Mungu. Ahadi ya Mungu hakuna budi kutimizwa na kutekelezwa. Basi yawapasa kutafakari kwa takwa na haya. Je, hii ni njia ya uadilifu kwamba Masihi ateremshwe kutoka mbinguni na ihalifiwe ahadi ya mfanano wa silsila ya kuweka Khalifa? Mshabaha wa silsila hizi mbili umewajibika kwa hukumu ya Mungu Mwenye ghera kama vile ifahamikavyo kutokuana na neno ‘kama’ katika Sura An-Nuur.

MLANGO WA SABA

Kuhusu غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّالِّينَ

Mwenyezi Mungu Akujaalie bahati njema, ujue kwamba katika Sura hii Mwenyezi Mungu Amegawa Mayahudi na Wakristo katika aina tatu. Na Ametuhamasisha tuwe katika aina yao moja na kututolea habari yake njema kwa fadhili na ihsani. Na aina nyingine mbili zilizobakia, hizo ni za walioghadhibikiwa yaani Mayahudi na waliopotea yaani wenye msalaba. Basi Ametuamuru kujikinga Naye katika kuungana nao kwa bahati mbaya na kuasi. Basi imedhihirika kutokana na Sura hii kwamba jambo letu limeachwa baina ya hofu na matumaini, neema na majaribio, kulazimika kushabihiana na manabii au kujinywea kutoka ndani ya kikombe cha wenye bahati mbaya. Kwa hiyo, Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye onyo lake ni kali na ahadi zake zina shani kubwa. Na yule asiyefuata mwongozo wa manabii kwa fadhili ya Mungu Wadudi, huhofiwa kwamba atakuwa kama Wakristo au Wayahudi. Sasa haja ya mifano ya manabii na mitume imezidi ili nuru yao iondoe giza la walioghadhibikiwa na shaka za waliopotea. Kwa hiyo imewajibika kudhihirika kwa Masihi Mau'udi katika zama hizi kutoka katika umati huu. Kwa kuwa wapotovu wamekithiri, kwa hiyo haja ya kukabiliana nao ilimtaka Masihi aje. Nanyi mwaona makundi kwa makundi ya makasisi waliopotea. Basi, Masihi yupo wapi atakayewafukuzilia mbali – ikiwa

mnajua. Je haikudhihiri athari ya dua au mmeachwa katika usiku wenye kiza totoro? Je mlifundishwa dua ile ya "njia ya walioneemeshwa" ili majuto yenu yazidi na muwe kama walionyimwa? Basi ukweli ni huu – nami nasema ukweli tu – kwamba Mwenyezi Mungu Aligawa makundi ya aina tatu katika Sura hii baada ya kutayarisha kila mfano kutoka miongoni mwao ndani ya umati huu. Na mnaona walioghadhibikiwa wamekithiri na waliopotea wamekuwa wengi. Basi, yuko wapi aliyekuja juu ya mfano wa manabii na mitume waliopita. Mmekuwaje hamzingatii jambo hili na mnapita mkighafilika. Tena ujue kwamba Sura hii imehabarisha kuhusu mwanzo na mwisho na imeashiria kwenye kaumu ambayo ni mwisho wa kaumu zote na kilele cha ufisadi, kwani Sura hii inaishia kwa الضَّآلِّيْنَ (waliopotea) na ndani yake mna ishara kwa watafakario. Kwani Mwenyezi Mungu Ametaja makundi haya mawili mwishoni mwa Sura hii, lakini hakumtaja dajali aliyeahidiwa wazi wazi wala kwa kuashiria juu ya kwamba sehemu hii ilihitaji kutajwa kwa dajali. Kwani, Sura hii imeashiria katika kauli yake الضَّآلِّيْنَ kwenye fitina ya mwisho na fadhaa kubwa kabisa. Lau kama fitina ya dajali ingekuwa kubwa kuliko fitina hii katika elimu ya Mungu, Yeye Angehitimisha sura hii kwenye fitina ya dajali sio kwenye kundi hili (la waliopotea). Kwa hiyo, tafakarini moyoni mwenu kwamba je Mola wetu Jalali Alisahau jambo la msingi na

kawataja 'waliopotea' ambapo paliwajibika kutaja 'dajali'. Na kama jambo lingekuwa kama vile majahili wanavyodhani, basi Mwenyezi Mungu Asingekuwa na budi kusema katika sehemu hii غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَ لَا الدَّجَّالِ . Na unajua kwamba Mwenyezi Mungu Amekusudia katika Sura hii kwamba Auhamasishe umati huu kufuata njia za manabii na kuwatahadharisha kushika njia za makafiri waovu. Basi Alitaja kaumu Aliowakamilishia fadhili zake na kuwatimilizia neema zake na kuahidi kwamba Atamtuma kutoka katika umati huu atakayeshabihiana na manabii na kufanana na mitume. Kisha Akataja kaumu nyingine walioachwa gizani na Akafanya fitina yao kuwa fitina ya mwisho na msiba mkubwa mno, na Akaamuru watu wote wajikinge Kwake katika fitina hizi mpaka siku ya kiama, na waombe kwa unyenyekevu ndani ya sala katika nyakati tano kwa kuondolewa fitina hizi. Hakuashiria hapa kwenye dajali na fitina yake kubwa. Basi kuna uthibitisho gani mkubwa zaidi kuliko huu juu ya kubatilisha itikadi hii. Tena miongoni mwa hoja zingine zinazounga mkono uthibitisho huu ni kwamba Mwenyezi Mungu Amewataja Wakristo mwishoni mwa Kurani kama vile Alivyotaja mwanzoni mwa Furkani. Kwa hiyo utafakari katika لَمْ يَلِدْ وَ لَمْ يُوْلَدْ na katika الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ . Hao ndio Wakristo tu. Basi ujikinge kwa Mola wa watu katika fitina za mapadri wao. Na Mwenyezi Mungu kama vile Alivyomalizia Sura Al-Faatiha kwa الضَّآلِّيْنَ (waliopotea)

ndivyo Alivyohitimisha Kurani Tukufu kwa kutaja Manasara. Na bila shaka 'waliopotea' ndio Manasara kama vile ilivyosimuliwa kutoka kwa Nabii wetu[saw] katika '*Addurrul Manthuur*' na katika '*Fat'hul Baarii*'. Kwa hiyo usipuuze kauli thabiti mashuhuri inayokubaliwa na umma.

MLANGO WA NANE

Maelezo ya Al-Faatiha kwa ujumla

Ujue kwamba Mwenyezi Mungu Ameanzia Kitabu Chake kwa حمد (hamdu) sio kwa شكر (shukurani) wala kwa ثناء (sifa), kwani neno 'hamdu' ni timilifu na kamilifu zaidi kuliko maneno mengine mawili na linayajumuisha hayo ndani yake. Tena hili linawapinga waabuduo mahuluku na masanamu, kwani hao huwahimidi miungu wao na wanawawanasibishia sifa za Rahmani. Na ndani ya 'hamdu' kuna ishara nyingine pia nayo ndiyo kwamba Allah Ta'ala Mwenye mibaraka Amesema: Enyi watumishi wangu, nitambueni kwa sifa zangu na niaminini kwa sifa zangu kamilifu. Zitazameni mbingu na ardhi; Je mwakuta mithili yangu Mola wa walimwengu na Mrehemevu kuliko warehemu wote na Mmiliki wa siku ya malipo. Isitoshe, ndani ya 'hamdu' kuna ishara pia kwenye jambo hili kwamba Mwabudiwa wenu ndiye Mwabudiwa Aliyejijumuishia aina zote za hamdu naye ndiye wa pekee katika uzuri na sifa zake. Na pia humo kuna ishara kwamba shani yake imeepukana na kila upungufu, badiliko na kupatwa na aibu kama mahuluku. Bali, Yu kamili msifiwa, hana mipaka, anayo hamdu katika mwanzo na mwisho na tangu azali mpaka abadi. Ndiyo sababu Mwenyezi Mungu Akamwita Nabii wake jina Ahmad. Kadhalika Masihi Mau'udi naye kaitwa jina hili ili kuashiria kwenye makusudio yake. Mwenyezi Mungu Ameweka

hamdu mwanzoni mwa Al-Faatiha kisha Akaashiria kwenye hamdu mwishoni mwa Sura hii hii, kwani mwishoni mwake kuna neno الضَّآلِّيْنَ (waliopotea) na hao ndio Manasara wanaojitanibia hamdu ya Mwenyezi Mungu na wakampa mmoja wa viumbe haki hii. Hivyo uhakika wa upotevu ndio kuachana na Mungu Msifiwa Anayestahiki hamdu na sifa zote kama vile Manasara walivyofanya na wenyewe wamejitengenezea msifiwa mwingine na wakapita kiasi kumsifu na wakafuata matamanio. Wakaenda mbali na chemchemi ya uzima na wakaangamia kama vile anavyoangamia aliyepotea jangwani. Na Mayahudi waliangamia mwanzoni mwa wakati wao na kurejea kwa ghadhabu ya Mungu Kahari. Na Manasara walisonga mbele kidogo kisha wakapotea, wakakosa maji, hivyo wakafa jangwani katika hali ya kushurutika. Kwa neno zima, Mwenyezi Mungu Aliumba ma-Ahmad wawili, mmoja mwanzoni mwa Islam na mwingine katika zama za mwisho. Na Akaashiria kwenye hao wawili kwa kurudia neno hamdu mwanzoni mwa Sura Al-Faatiha na mwishowe kwa watambuzi wa mambo ya kiroho. Na Akafanya hivyo kuwakanya Manasara. Na Akateremsha ma-Ahmad wawili kutoka mbinguni ili wawe kama kuta mbili kwa kuwahami walio wa mwanzo na wa mwisho. Na hili ndilo jambo la mwisho tulilokusudia kueleza katika mlango huu kwa kuwezeshwa na Mungu Rahimu Wahabu. Twamshukuru Mungu kwa kuwezeshwa

na kujaaliwa. Na hii ni fadhili Yake kwamba ahadi yetu imetimia. Tusingeweza kuandika hata herufi moja kama kusingekuwa msaada wa Mungu Aliye Mkuu. Yeye ndiye Aliyeonyesha ishara na kuteremsha hoja zilizo wazi na kulinda kalamu yangu na kauli yangu isikosee na kuhifadhi heshima yangu dhidi ya maadui. Akajikalia nyumbani mwangu na Akanidhihirikia katika utukufu na Akaja katika sebule yangu na kuniteua kwa Ukhalifa wake. Na Akajiwekea mahususi malisho yangu. Akanitakasa na kunitakasa vizuri sana na kanilea na kunilea vizuri mno na kanitunza kwa njia bora sana. Akanidhihirikia na Akaniathiri kwa mapenzi hata kwamba sijali uadui wa watu na huba yao wala mahuluku kunisifu au kunilaumu. Sasa ni mamoja kwangu mtu kunijia au kunichukia, kutaka miliki yangu au kunitupia mawe. Na dunia hii imekuwa kwangu kama kijakazi aliyeshikwa na ndui na uso wake ukawa mweusi na sura yake imeharibika, urefu (wa kwenda juu) wa pua yake umebadilika kuwa ufupi na mashavu yake mekundu yamepata madoa meusi. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu nimejiokoa katika nguvu na mamlaka ya dunia. Na nimelindwa na shambulizi la ghuli yake na mashetani zake. Nami nimeshatoka katika watu wanaoliacha shina na hutafuta tawi. Hupoteza takwa kwa ajili ya dunia hii na huuza mazao mabichi ya shambani. Na wanataka kauli zao ziimarike mioyoni mwa watu ingawa hawakujitakasa katika uchafu. Na yatarajiwaje maji safi

kutoka katika kiriba kinukacho, na ikhlasi na dini kutoka katika tabia iliyo chafu! Awezaje mfungwa kuhesabiwa kama aliyeachiliwa huru katika kifungo? Na mwovu ataingiaje katika waungwana, watu watajumuikaje kwake ilihali yu habithi na ni baya linalotoka mdomoni mwake. Kalamu yangu imetakaswa katika matamanio ya nafsi na kuchongwa kwa kupata radhi ya Mola. Ndani ya kalamu yangu mna alama za mema yabakiayo sio kama alama za kwato za farasi bora (zifutikazo). Sisi tu mashujaa, hatuanguki kutoka mgongoni mwa farasi. Tu pamoja na Mola wetu mpaka mauti yatufikie. Na farasi zetu wanawarukia maadui jinsi furukombe amrukiavyo shore au kama kozi kumrukia panya aliyetishika. Enyi maadui zangu, achaneni na baadhi ya madai yenu; msijidai shibe juu ya kuwa na tumbo tupu. Je, mnasimama kupigana vita mkiinua mikuki yenu wala hamwoni mapazia yenu na minyororo mizito mliyotiwa. Mnaona taabu za majuto hata hivyo mnajiingiza humo, na mnakabili huzuni za dhila hata hivyo mnaelekea kwazo. Mfano wenu ni kama mfano wa mbuzi ambaye mara anakula majani makavu na mara majani mabichi na hamtii mchunga bila kumwasi. Na elimu mliyonayo ni kama rundo la nafaka lililokafuliwa ambalo halijapepetwa na humo vimechanganyika kinyesi cha ng'ombe na vitu vingine vyenye madhara. Hata hivyo mnasema hatuhitaji Mwamuzi kutoka mbinguni. Hii ndiyo bahati mbaya, kwa hiyo tafakarini enyi wenye akili. Nami

najuja kama kujua vitu vitambulikavyo kwa kuona, kusikia na kuonja, na mambo yaliyo dhahiri shahiri yenyewe kwamba nimetumwa na Mola wangu kwa kujaaliwa miongozo na ishara. Nami nimefunuliwa wahyi kwa muda ule ulio muda wa wahyi wa Hadhrat Khatamun Nabiyyiin[saw] (miaka 23). Nilianza kufunuliwa kabla ya kufikia miaka arobaini hadi kukaribia miaka sitini. Je, inajuzu kumkadhibisha mtu ambaye muda wake wa kufunuliwa wahyi ni sawa na muda wa Nabii wetu Mteule[saw]? Na Mwenyezi Mungu Ameufanya muda huu kuwa dalili ya ukweli wa Mtume wake Mteule[saw]. Na nimesikia baadhi ya watu wameikatalia dalili hii; hawakukubali daili hii kwa wasiwasi wa shetani. Kwa hiyo sikuweza kupata usingizi usiku kucha na kutoka machoni mwangu mlitiririka chemchem ya machozi. Hapo Mola wangu Akaongea nami kwa rehema yake kubwa na Akasema: "Waambie, mwongozo wa Mungu ndio mwongozo hasa." Basi sifa zote njema zinamhusu Yeye, Naye ndiye Mola wangu katika dunia hii na katika siku watakapokusanywa watu wote ili walipwe. Ee Mola wangu, nishukie moyoni mwangu na ujidhihirishe kutoka kifuani mwangu baada ya kujifia kwangu na kunijazia fuadi yangu nuru ya maarifa. Ee Mola wangu, U muradi wangu, basi nipe muradi wangu. Ee Mola wa mabwana, kwa heshima yako usinifishe kifo cha aibu. Ee Mola wangu, nimeshakuchagua Wewe, basi Unichague mie; Uangalie

moyo wangu kwa rehema na unijie. Bila shaka U Mjuzi wa siri na Mwenye habari ya yale yanayofichwa wasijue wengine. Ee Mola wangu, kama unajua kwamba maadui zangu ndio wakweli na wenye ikhlasi basi nihilikishe kama wahilikishwavyo makadhabu. Na kama unajua kwamba mimi nahusiakana Nawe, nami nimetoka Kwako, basi usimame kunisaidia, kwani mimi nahitaji msaada Wako. Na usiwakabidhi jambo langu maadui wapitao wakinifanyia mzaha na unihifadhi na maadui na wenye hila. U raha yangu na utulivu wangu na Pepo yangu na kinga yangu, basi nisaidie katika jambo langu na nisikie kilio changu na msalie Muhammad[saw] Mbora wa Manabii na Imamu wa wamchao Mungu na mpe daraja ambazo hukuwapa Manabii wengine. Ee Mola wangu, mpe Mtume[saw] neema zote ulizozikusudia kunipa. Kisha nighofirie kwa heshima yako; U Mrehemevu zaidi kuliko warehemevu wote. Na sifa zote zinakuhusu wewe kwamba kitabu hiki kimechapwa kwa fadhili Yako katika muda wa idadi ya herufi ‘Ain (yaani siku sabini) katika siku ya Ijumaa na ndani ya mwezi mtukufu baina ya Idi mbili. Ee Mola wangu, ukifanye kwa fadhili Yako kiwe chenye baraka na manufaa kwa watafutao haki na mwongozo kwenye njia sahihi, Ee Mwenye kuwapokelea dua waombaji. Amin thumma amin. Na dua yetu ya mwisho ndiyo hii kwamba sifa zote njema zinamhusu Mungu, Mola wa walimwengu.

♦♦♦

KWA FADHILI YA MUNGU MUUJIZA MKUBWA UMEDHIHIRIKA

Maelfu ya shukurani kwa Mungu Mweza wa Pekee Aliyenijaalia ushindi katika uwanja huu wenye shani adhimu, na juu ya kuvikabili vizuizi vya aina aina katika siku hizo sabini – mara chache nilishikwa vikali na maradhi, baadhi ya jamaa wakawa wagonjwa – hata hivyo maelezo haya (ya Sura Al-Faatiha) yakakamilika. Yule mtu atakayezingatia kwamba haya ndiyo maelezo yaliyoandikwa baada ya kuwatupia mwito maelfu ya wapinzani, yeye mtu huyo hatakuwa na budi kuyakini kwamba huu ndio muujiza mkubwa. Ebu, niulize kwamba kama huu si muujiza, basi nani aliwazuia wasiandike maelezo wakati wa shindano hili ilihali masheikh wapinzani walitupiwa mwito kwa maneno ya kuchochea ghera yao; na ni nani aliyempa mtu – yaani mimi wanayenidhania jahili nisiyejua hata neno moja la surufi maumbo – uwezo wa kuandika maelezo yenye ufasaha yasiyo na kifani juu ya kuugua maradhi na kupata taabu kimwili. Hata kama masheikh wapinzani wangedhurika akilini wakiendelea kujaribu, hata hivyo wasingeweza kuandika maelezo mithili yake. Na kama masheikh wapinzani wetu wangalikuwa na uwezo au Mwenyezi Mungu Angaliwasaida, ingaliweza kuchapishwa wakati huu kwa akali vitabu elfu moja vya maelezo. Lakini sasa watajibuje kwamba kwa kuweka kuandika maelezo kuyakabili maelezo yangu kuwa msingi

wa uamuzi niliwatupia mwito masheikh wapinzani na muda waliopewa wa siku sabini haukuwa kidogo, nami nilikuwa peke yangu na hao walikuwa maelfu wajiitao wajuzi wa Kiarabu na wataalamu, hata hivyo walishindwa kuandika maelezo. Kama wangeandika maelezo na kuleta uthibitisho dhidi yangu kutoka katika Sura Al-Faatiha, hapo watu wote wangewakimbilia. Basi kuna nguvu gani ya siri iliyozuia mikono ya watu maelfu na kuyafanya mabongo yao finyu na kutwaa elimu yao na ufahamu wao na kwa ushahidi wa Sura Al-Faatiha ikapiga mhuri juu ya ukweli wangu na kwa mhuri mwingine kupumbaza mioyo yao na kuondoa ufahamu wao. Na ikadhihirisha mbele ya maelfu ya watu nguo zao chafu na kunivika joho jeupe la heshima lililong'ara kama theluji. Kisha ikanikalisha kitini mwa heshima. Na kutokana na Sura Al-Faatiha nikajaaliwa **jina la heshima**. Ni lipi hilo? Ni أَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ[44] . Na angalieni fadhili na rehema ya Mwenyezi Mungu kwamba kwa kuandika maelezo kulikuwa na sharti la juzuu nne[45] yaani kuandika juzuu nne katika muda wa siku sabini, lakini hao juu ya kuwa maelfu hawakuweza kuandika hata juzuu moja lakini mimi Mwenyezi Mungu Akanijaalia kuandika juzuu kumi na

[44] Uliowaneemesha.

[45] Juzuu katika istilahi ya uchapaji yamaanisha kurasa 16. Juzu nne ndiyo kurasa 64.

mbili na nusu badala ya juzuu nne. Sasa ningependa kuwauliza masheikh wapinzani kwamba je, huu si muujiza, na kwa nini usiwe muujiza? Hakuna mtu asiyetumia uwezo wake wote kuepukana na dhila. Basi, kama kuandika maelezo kulikuwa ndani ya uwezo wa masheikh wapinzani, kwa nini hawakuweza kuyaandika? Maneno haya yaliyochapishwa katika matangazo yangu kwamba lile kundi ambalo halitaandika maelezo katika siku sabini kwa kushindana atafahamika kuwa mwongo, je haya siyo maneno yamchocheayo mtu mwenye ghera kuziachilia mbali shughuli zote kwa kwa kutimiza kazi hii ili asiitwe mwongo? Lakini wangewezaje kukabiliana! Ingewezaje kutanguka Kauli ya Mungu كَتَبَ اللّٰهُ لَاَغۡلِبَنَّ اَنَا وَ رُسُلِیۡ[46] . Kwa kudumu mpaka mwisho wa dunia Mwenyezi Mungu Alitaka kuwakamilishia hoja hii kwamba juu ya kuwa na elimu na uwezo hali yao ni hii kwamba maelfu ya masheikh wao waitwao wataalamu hawakuweza kudiriki mbele ya mtu mmoja, hata hivyo wanajasiri kumwita kafiri. Je haikuwalazimu kukamilika kwanza kielimu kisha wangekufurisha. Hali yao ni kwamba hawakuweza kuandika juzuu nne ya maelezo. Kwa kuwategemea hao kumpinga aliyetumwa na Mwenyezi Mungu anayeendelea kuonyesha ishara juu ya ishara ni kazi ya weneye bahati

[46] Mwenyezi Mungu Amekwisha andika: Bila shaka Nitashinda Mimi na Mitume Wangu. (Al-Mujaadila 58:22)

mbaya sana. Hatimaye kuna sababu nyingine ya kumtolea Mwenyezi Mungu shukurani elfu kwamba wakati huu bishara moja ya Mtume Mtukufu[saw] pia imetimia nayo ndiyo kwamba katika muda huu wa siku sabini kwa sababu ya maradhi niliyonayo na kwa sababu ya kuandika maelezo siku nyingi katika hali ya kuugua nikawa dhaifu sana na nikalazimika kukusanya sala zinazoweza kukusanywa. Na hivyo bishara ile ya Mtume Mtukufu[saw] imetimia iliyopo katika vitabu vya Durri Manthuur, Fat'hul Baari, Tafsiri Ibni Kathiir na kadhalika, kwamba تُجْمَعُ لَهُ الصَّلٰوةُ yaani kwa ajili ya Masihi Mau‘udi sala zitakusanywa. Sasa, maulamaa wapinzani watuambie pia kwamba je wanakubali au la kwamba kwa kutimia bishara hii alama ile pia ya Masihi Mau‘udi imedhihirika; na kama hawakubali, basi walete mfano wowote kwamba mtu yeyote baada ya kudai kuwa Masihi Mau‘udi alipata kukusanya sala kwa miezi miwili au leteni mfano hata bila kudai.

Salamu iwe kwa afuataye mwongozo.

Mtangazaji:
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
20 Februari 1901.

KUTIMIA BISHARA NYINGINE YA MTUME[SAW] WA MUNGU

قَالَ رَسُوْلُ اللّٰهِ صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ اِنَّ اللّٰهَ يَبْعَثُ لِهٰذِهِ الْاُمَّةِ عَلٰى رَأْسِ كُلِّ مِائَةِ سَنَةٍ مَنْ يُجَدِّدُ لَهَا دِيْنَهَا

Mtume[saw] wa Mungu alisema kwamba lazima kabisa Mwenyezi Mungu Atamtuma kwa umati huu mwanzoni mwa karne zote mtu (Masihi Mau'udi) atakayejadidisha kwa umati huu dini yake. Hadithi hii Takatifu imefikia daraja ya *tawatur* (*kufululiza*) na ijima. Ingawa wafasiri muhaddithina na masufii waifasiri kwa njia yoyote lakini maana yake Aliyonifundisha Mwenyezi Mungu ndiyo hii kwamba Hadithi hii inamhusu Masihi Mau'udi, kwani wajadidi waliopita kabla au watakaokuwa baadaye wanadhaniwa tu na kwa ujumla twaamini kwamba mwanzoni mwa kila karne mjadidi alitokea lakini kwa kirefu na kwa yakini hatuwezi kusema kwamba ndani ya karne zilizopita nani walikuwa wajadidi. Kwani, Mtume Mtukufu[saw] hakutoa orodha ya wajadidi, lakini kuhusu Masihi Mau'udi twaweza kusema kwa dalili za kuyakinisha zilizo za kweli na rai iliyo sahihi kwamba yule mujadidi ambaye Mtume Mtukufu[saw] alimtaja baada yake akisema kwamba umati ule unawezaje kuhilikika ambao mwanzoni mwake nipo mimi na mwishoni atakuwa Masihi Mau'udi na zama za katikati ni ya upotevu, kwa hakika ndiye Masihi Mau'udi ambaye alama ya kutumwa kwake Mtume[saw] akatuambia ni kwamba atakuja katika

zama mianzo ya karne zote itakapokutana. Sasa tunapoona kwa makini tunakuta kwamba zama zile ni zama hizi tu ambapo Mjadidi Mkuu aliinuliwa na akapata mianzo ya karne zote, yaani 1318 Hijria na 1901 A.D. na 1307 Fasli na 1957 Bikrami na vilevile alipata mama ya karne yaani elfu ya saba. Basi kwa mianzo ya karne za kalenda zote kukutana bishara ya عَلٰى رَأْسِ كُلِّ مِائَةِ سَنَةٍ ikatimia na Hadithi ya kupatwa kwa jua na mwezi na aya ya Kurani Tukufa وَ اٰخَرِيْنَ مِنْهُمْ zaisadikisha. Hivyo basi, yule Masihi Mau'udi na Mjadidi wa ahadi ndiye Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.

Kwa hiyo Alhamdulillahi.

Mwandishi:
Muhammad Sirajul Hak Nu'mani